MBINU ZA KULEA WATOTO KIMILIONEA

Venerando J. Milinga.

Mwenye hakimiliki ya kusambaza Kitabu hiki ni:
Remili Enterprises Company

P.O. Box 2311, Ihila Street Buhongwa Mwanza, Tanzania.
Phone: +255 767 285 417
Email: venerandojmilinga@rocketmail.com

ISBN 978-9987- 9797-3-8

Mhariri Mkuu: Imeandaliwa na Kuchapwa Tanzania
Prosper Printing Company (PPC)
S.L.P. 72635, Dar-es-Salaam
Mkurugenzi: +255 713 212 440
Meneja: +255-715-964536; +255-756-964536
Barua pepe: fadhilijuliasi@gmail.com

Kava na Fadhili +255 683 776 860

ONYO:
Haki zote za kitabu hiki zimehifadhiwa kwa mujibu wa sheria ya haki miliki. Hairuhusiwi kuchapisha kitabu hiki, kukinakiri kwa namna yoyote ile, hairuhusiwi kukitangaza wala kukisambaza popote bila idhini ya mwandishi au msambazaji wake Remili Enterprises Company.

YALIYOMO

Kuhusu Mwandishi.....v

Shukrani.....vi

Ungulizi.....vii

Ujumbe wa Mwandishi wako.....xii

Mbinu ya -1-.....1

Mbinu ya -2-.....5

Mbinu ya -3-.....11

Mbinu ya -4-.....17

Mbinu ya -5-.....21

Mbinu ya -6-.....25

Mbinu ya -7-.....26

Mbinu ya -8-.....29

Mbinu ya -9-.....31

Mbinu ya -10-.....34

Mbinu ya -11-.....37

Mbinu ya -12-.....39

Mbinu ya -13-.....42

Mbinu ya -14-.....44

Mbinu ya -15-.....45

Mbinu ya -16-.....48

Mbinu ya -17-.....52

Mbinu ya -18-.....54

Mbinu ya -19-.....56

Mbinu ya -20-.....58

Mbinu ya -21-.....61

Mbinu ya -22-.....64

Mbinu ya -23-.....66

Mbinu ya -24-.....68

Mbinu ya -25-.....73

Mbinu ya -26-.....76

Mbinu ya -27-.....78

Mbinu ya -28-.....80

Mbinu ya -29-.....82

Mbinu ya -30-.....84

Mbinu ya -31-.....88

Mbinu ya -32-.....90

Mbinu ya -33-.....92

Mbinu ya -34-.....94

Mbinu ya -35-.....96

Mbinu ya -36-.....98

Mbinu ya -37-.....100

Mbinu ya -38-.....102

Mbinu ya -39-.....104

Mbinu ya -40-.....108

KUHUSU MWANDISHI

Venerando J. Milinga, alizaliwa mkoani Kigoma nchini Tanzania miaka 43 iliyopita. Aliandika kitabu hiki akiwa mfanyakazi katika shirika la hifadhi ya jamii **LAPF** linalojishughulisha na huduma za hifadhi ya jamii nchini tangu mwaka 2005 hadi anaandika kitabu hiki.

Mwaka 2012 Oktoba, alihitimu Shahada ya Uzamili katika maendeleo ya jamii na Uchumi katika Chuo Kikuu huria cha Tanzania (Masters in Community Economics Development).

Mwaka 2002 alihitimu Stashahada ya Juu katika fani ya Hifadhi ya Jamii kutoka chuo cha Usimamizi wa Fedha (Advanced Diploma in Social Security Administration) kilichoko jijini Dar es Salaam.

Ni mkurugenzi Mtendaji wa kampuni yake binafsi ya **"Remili Enterprises Company"** inayojishughulisha na biashara mbalimbali ikiwemo usambazaji wa vitabu vyenye kuchochea mabadiliko ya akili na mitazamo (mindset changing), kutoa mikopo kwa wajasiriamali pamoja na ufugaji wa kuku na kware. Venerando J. Milinga, pia hutoa elimu ya ujasiriamali kwa watu wa makundi mbalimbali ndani na nje ya nchi.

SHUKRANI

Natoa shukrani tele kwa kila mtu aliyehusika kwa namna moja ama nyingine kufanikisha kukamilika kwa kitabu hiki mpaka kuweza kuingia sokoni. Nawashukuru sana Wafanyakazi wenzangu wote wa **LAPF Pensions Fund** kokote waliko nchini kwa kuendelea kunitia moyo wa kuzidi kuandika vitabu vinavyohamasisha ubongo na akili kuelekea mabadiliko mpaka kuweza kuandika kitabu hiki. Wafanyakazi wenzangu wa LAPF wamekuwa mstari wa mbele Kununua vitabu vyangu huku wakihamasisha na watu wengine kuvinunua na kunifanya kutiwa moyo zaidi wa kuandika pamoja na kwamba kazi ya kuandika ni ngumu.

Namshukuru sana ndugu Shakuru Habuba Mohamed wa Dar es Salaam aliyefanyakazi ya kupitia ukurasa hadi ukurasa na kujitahidi kusaidiana na mimi kuona kuwa sasa kitabu kimekaa sawa kwa ajili ya uchapaji na usambazi.

Mwisho ingawa siyo kwa umuhimu, Natoa shukrani zangu za dhati kwa wanafamilia wangu wote kwa kunitia moyo muda wote wa kuandika kitabu hiki. Aidha, Nawashukuru wateja wangu wote wanaoendelea kuniamini kuwa ninaweza kuwapa mambo mazito yanayofaa kwa maendeleo yao na hivyo wameendelea kununua vitabu ninavyoviandika. Bila wao kununua vitabu vyangu siwezi kuendelea kupata moyo wa kuandika vitabu vingine. Nawashukuru mawakala wangu kote nchini wanaonisaidia kusambaza vitabu vyangu ili kuweza kuwafikia wateja wangu akiwemo Mwalimu Addylekson Mgallah wa kampuni ya Books Network Tanzania (B.N.T) ya Dar es Salaam kwa jinsi anavyofanya kazi na mimi kuweza kuwasambazia vitabu wateja kote nchini.

UTANGULIZI

Je, una watoto na ungependa wasiwe maskini maishani mwao? Je, wewe ni mzazi unayewapenda watoto wako wa kike au wa kiume na ungependa watoto wako wasiwe na maisha duni yenye ukosefu wa pesa na mahitaji muhimu?

Kama jibu lako ni ndiyo, na unawapenda watoto wako; hakika utawapa urithi ambao utawafanya waendelee kuishi maisha yao kwa raha mstarehe wakiwa mamilionea kwa miaka yao yote watakayoishi duniani hata kama wewe hutakuwepo tena duniani.

Hivi unajua kwamba asilimia 90 ya watu maskini kote duniani wametokana na jinsi walivyolelewa na wazazi wao wakati wakiwa na umri wa miaka 0-15? Hivi ulikuwa unaelewa kwamba mtoto ili aweze kuwa tajiri huandaliwa na mzazi kuwa tajiri? Je, unayo habari kwamba matamushi yako ya kila siku, vitendo vyako na kila unalolifanya mbele ya watoto ndiyo humwandaa mtoto wako kuja kuwa maskini au milionea?

Kwa kuwa mtoto hujifunza kwa kusikia, kutazama, kugusa, kunusa, na kuonja hakikisha kwamba unamlea kisaikolojia na kimtazamo wa kibilionea ili kumwepusha na maisha ya kimaskini na kifukara. Hilo lawezekana kwa kuanza kumlea hivyo tangu akiwa mdogo kuanzia akiwa na umri wa miaka kuanzia 0-15. ukikosea kwenye umri huo watoto wako watakufa masikini.

Lazima ukatae kuwalea watoto wako katika mweleko wa kifukara. Wazoeshe kutamka mamilioni ya pesa. Wazoeze kushika pesa nyingi wakiwa bado wadogo. Wazoeze watoto wako kufanya kazi. Wazoeze kumiliki miradi na biashara kubwa. Waoneshe kwamba wamezaliwa kwa ajili ya kumiliki pesa na mali za mamilioni popote Tanzania na duniani kote. Wazoeshe kusoma vitabu vya maswala ya pesa hata kama watakuwa hawasomi

shule au vyuo vya biashara na fedha. Nunua kila mara vitabu vinavyohusu mbinu za kupata pesa. Usisahau kamwe kununua vitabu vya elimu ya dini na maadili ili watoto wakue wakimjua Mungu pia.

Hakuna mzazi ambaye hangependa kuwaona watoto wake wakiwa na maisha mazuri na yenye furaha. Labda ni mzazi taahira au chizi tu ndiye anayeweza kuzaa watoto na kuwaacha bila msaada wowote wa kuwawezesha kuishi kwa furaha hapa duniani. Ni kweli kwamba kulea watoto wa kizazi cha leo mpaka na wao waje kufanikiwa kiuchumi na kifedha maishani mwao ni kazi ngumu sana. Kila mzazi kila kona utamsikia akisema watoto wa siku hizi hawasikii hawaambiliki wala hawana adabu. Wengine utawasikia wakisema kizazi cha sasa kina laana. Kila mmoja husema kulingana na jinsi anavyoyaona mambo yanakwenda. Ni wazazi wachache sana wenye furaha na matumaini kwa watoto wao kwamba wataishi maisha ya raha na furaha siku zote za maisha yao.

Ukweli ninaouona mimi kama msomaji, mchambuzi na mwandishi wa vitabu mbalimbali ni kwamba watoto wetu walivyo leo hii ni taswira au picha ya wazazi wa sasa. Watoto wa kisasa ni zao la wazazi wa kisasa. Hakuna mtoto aliyezaliwa akiwa hivyo alivyo kitabia au kihaiba bali ametengenezwa na mfumo wa maisha ya wazazi na jamii aliyoikuta tangu alipozaliwa.

Kwa hiyo, kabla hatujawahukumu watoto au vijana wa sasa tunapaswa kujihukumu kwanza sisi wazazi wa kisasa kuhusu tabia yoyote nzuri au mbaya waliyonayo watoto wetu. Nasema hivyo kwa sababu watoto wanazaliwa na kupandikiziwa ubongoni mwao na kwenye fikra zao kuwa na tabia za jamii iliyopo kwa sasa. Kwa mfano, watoto wanaoitwa wa mitaani au wa mazingira magumu au vyovyote utakavyowaita wamezaliwa

na sisi wazazi wa siku hizi. Watoto hawa waliopo hawakuzaliwa wala kulelewa na wanyama wa porini. Kwa hiyo makosa yafanywayo na watoto wa kisasa ni sura au kivuli (reflection) halisi cha makosa ya wazazi wa kisasa. Kama mtoto anamaliza kidato cha nne bila kujua kupika ugali au kukaanga mboga au kufua nguo zake mwenyewe na akawa hawezi hata kupika kwa ujumla, hilo siyo kosa lake, ni kosa la wazazi wake waliomlea hivyo alivyo. Wanaopaswa kulaumiwa ni wazazi wake wala siyo mtoto.

Kufuatia hali hiyo mbaya iliyopo katika jamii yetu ya Tanzania, mwandishi wa kitabu hiki anakuja na suluhisho au majibu ya jinsi ya kuwalea watoto siyo kibilionea tu bali pia kimaadili zaidi. Kitabu hiki kinatoa mwongozo mzuri wa jinsi ya kumlea mtoto kuanzia akiwa na umri wa mwaka 0 hadi miaka 15 kifedha, kimaadili, kisaikolojia, kielimu na kimajukumu zaidi. Kitabu kimefafanua mbinu Zipatazo 35 ambazo mzazi ukizitumia kwa mtoto wako wa kike au wa kiume hakika ataweza kuanza mapema kujitegemea kiuchumi kwa maisha yake yote ya baadaye. Bado hujachelewa hata kama watoto ulionano ni wakubwa tayari. Hata wewe ambaye hujapata watoto (wa kike au wa kiume) ni muda mwafaka ukawa na kitabu hiki nyumbani kwako ukakisoma na kukielewa kabla hujawapata watoto.

Kijana mwenye ndoto ya kuwa na familia, kitabu hiki ndicho ukombozi wako na watoto wako utakaowazaa. Kitakusaidia kupanga ndoto yako vizuri ya familia uipendayo kuipata. Kijana, ungependa kuwa na familia yenye furaha na utajiri wa kweli? Kama jibu lako ni ndiyo, Kitabu hiki ndicho mwokozi wako na mwongozo wako. Kitabu kimetoa mbinu mbalimbali zikiwemo zile muhimu za kuwasomesha watoto siyo kwa nia ya kuja kuajiriwa na serikali au mashirika makubwa bali kuweza kuajiriwa kwenye Makampuni na miradi yako wewe mzazi mwenyewe. Mbinu ya kuwazoeza watoto kuamka mapema nayo

imefafanuliwa. Mbinu ya kuwafanya watoto wawe wachapa kazi za mikono na zile za kutumia akili zimeelezwa kwa kina. Kuwatembeza wanao maeneo ya kujifunza maisha bora badala ya kuwapeleka maeneo ya starehe imepewa uzito sana katika kitabu hiki. Kuwafundisha watoto kujiwekea akiba ya fedha, kuwafundisha kusoma masomo yenye maana na tija kubwa kifedha na kiuchumi maishani mwao, kuwazoeza kujisomea vitabu mbalimbali vyenye kuwapatia akili, na nyingine nyingi zimefafanuliwa zote ndani ya kitabu hiki ili mzazi atakayesoma ahakikishe kuwa watoto wake hawawi mafukara kamwe kuanzia mzazi akiwapo duniani na hata siku ambazo mzazi hautakuwepo tena duniani.

Hiki ni zaidi ya kitabu cha malezi ya watoto. Ni kitabu chenye siri za matajiri watumiazo kuwalea watoto wao ili waendelee kuwa matajiri. Kila bilionea mwenye akili atawafundisha watoto wake mbinu za kuishi kibilionea ili waweze siyo tu kusimamia miradi na Makampuni ya wazazi bali pia kuanzisha Makampuni yao binafsi. Kwa hiyo kila mzazi wa karne hii ya sayansi na teknolojia, kila mzazi anayewapenda watoto wake anapaswa kuwa na kitabu kama hiki.

Kama unawapenda kweli watoto wako wa kike au wa kiume unapaswa kuwa na kitabu hiki siyo tu kikusaidie kuwalea watoto kwa mtazamo na mwelekeo wa wao kuwa mabilionea baadaye bali pia kwa mwelekeo wa kimaadili na kiusalama kabisa. Kumbuka maandiko yanasema ".....Mtu mwema huwaachia wana wa wanawe urithi….." Mithali 13:22.

Ndani ya kitabu hiki utajifunza na kusoma Mbinu zaidi ya 35 zitakazokufaa wewe mzazi kuweza Kumlea Mtoto wako Kibilionea. Mbinu hizo zitakupa mwanga mpana na upeo mpana wa jinsi ya kuwalea watoto wako hadi wafikie hatua za kuwa mabilionea. Utajifunza mbinu za kualea watoto wako katika

zama hizi za utandawazi. Utajifunza mbinu za kuwalea watoto wa kizazi hiki kisichosikia la mkuu. Utajifunza mbinu za kuwalea watoto wa kizazi hiki cha zinaa. Kizazi kinachopenda starehe kuliko kazi. Kizazi kinachopenda kompyuta na televisheni na simu za "soft touch". Jiulize leo ukiondoka duniani unawaachia wana wa wanao urithi gani? Unaiachia dunia jambo gani ambalo halitafutika kamwe? Unaacha kitu gani nyuma yako ili wa Tanzania wote wajivunie kuja kwako hapa duniani hasa kuzaliwa kwako hapa Tanzania? Tafakari sana na uchukue hatua sahihi sasa.

Ninaposema mtu fulani ni "Milionea" ndani ya kitabu hiki kwa mazingira ya Tanzania namaanisha kuwa ni mtu mwenye kipato endelevu kisichopungua wastani wa Tshs 300,000 kwa siku au Tshs 9,000,000 kwa mwezi yaani Tshs 108,000,000 kwa mwaka. Ni mtu ambaye anaweza kumiliki zaidi ya gari moja, moja, nyumba nzuri ya kwake binafsi na nyumb za biashara, simu nzuri yeye mwenyewe na wanafamilia wake, anakula chakula kizuri anachotaka tena chenye virutubisho muhimu kwa binadamu. Ana uwezo wa kifedha wa kupeleka watoto shule anayoipenda na kuwalipia ada za shule bila wasiwasi. Ni mtu awezaye kutekeleza majukumu yake ya kifamilia bila wasiwasi wa kuishiwa fedha.

Kwa upande wa Ubilionea, ninaposema kuwa mtu fulani ni bilionea namaanisha mtu mwenye kipato kisichopungua wastani wa Tshs 10,000,000 kwa siku sawa na Tshs 300,000,000 kwa mwezi au Tshs 3,600,000,000 kwa mwaka yaani bilioni 3 kwa mwaka. Mwandishi wa kitabu Ndugu Venerando J. Milinga, amefafanua kwa kina sana mbinu zipatazo 35 za kumlea mtoto kibilionea. Huwezi kusoma kitabu hiki halafu watoto wako wakaja kuwa maskini maishani mwao. Ukisoma kitabu hiki, utagundua taaluma ya muhimu sana ambayo ni nadra kupatikana kwenye shule zetu za msingi au za sekondari au vyuo vya elimu ya juu.

UJUMBE WA MWANDISHI KWAKO

Ndugu Msomaji, Hongera sana!! Nakupongeza kwa kununua kitabu ambacho kitakupa fikra chanya katika malezi ya watoto. Umejipatia kitabu ambacho huwa ni wachache huvinunua vitabu vyenye kuongeza akili na maarifa ya fedha. Kitabu hiki kitakuletea manufaa makubwa sana wewe na watoto wa watoto wako.

Kwa kujipatia kitabu hiki umejipatia semina kubwa inayohusu mbinu za kuwalea watoto kimilionea. Hii ni semina kwako. Ukisoma kwa umakini mbinu hizi 35 nakuhakikishia kuwa watoto wako watalelewa kimilionea na mara tu wawapo wakubwa watakuwa mamilionea. Sasa unaweza kuanza kusoma mbinu hizo moja baada ya nyingine hadi mwisho. Epuka kumwazima mtu kitabu hiki kabla hujamaliza kusoma aya ya mwisho iliyomo katika kitabu hiki:

Pesa uliyoitoa Kununua kitabu hiki hujaipoteza, umewekeza mahali ambapo utavuna faida kubwa!!!! Nakuhakikishia kwamba ukikisoma kitabu hiki, utaweza kuwarithisha watoto wako pamoja na watoto wa watoto wao utamaduni na maarifa ya fedha na biashara ambayo yatakuwa chachu ya wao kuondoka kwenye umaskini kizazi hadi kizazi. Ukiwalea watoto wako kwa kufuata falsafa zilizomo kitabuni humu, ninakuhakikishia kuwa watoto wako wakitimiza umri wa miaka kumi na tano na kuendelea watakuwa na uwezo wa kuwaza kibilionea. Watakuwa na mawazo chanya kuhusu maana ya maisha, maana ya fedha, maana ya kujiajiri, faida za kujitegemea,nk.

Endapo utawalea watoto kwa kufuata mbinu zilizofafanuliwa kwa uwazi na upana katika kitabu hiki, nakuhakikishia kwa mara nyingine kuwa watoto wako watakuwa mabilionea. Wewe amini tu na uanze kufuata kwa vitendo mbinu na falsafa za

kuwalea watoto wako kibilionea kama inavyoelezwa ndani ya kitabu hiki. Ukweli ni kwamba kama utawalea watoto wako kwa misingi ya kibilionea watapata maisha bora na utajiri mkubwa na Usiofilisika milele. Maana yake ni kwamba kizazi baada ya kizazi chao watakuwa wanaogolea kwenye pesa tu. Kwa kusoma kitabu hiki nakuahidi kwamba watoto wako na ukoo wako wote utakaouleta hapa duniani hautaingia kwenye umasikini kamwe. Kila mtoto atakayezaliwa kwenye ukoo wako hataishi maisha yenye ukosefu wa fedha, akili na mali.

Mwisho kabisa, narudia huwezi kusoma kitabu hiki halafu watoto wako wasiwe mabilionea kamwe!!! Hongera sana kwa kuchangamkia maisha yenye utofauti. Karibu sana.

Mbinu ya -1-

Anzisha Maktaba ya Vitabu Vya Kujisomea

Siri ya mafanikio ya nchi zilizopiga hatua kimaendeleo hasa Ulaya, Amerika na Asia ni utamaduni wao wa usomaji wa vitabu. Utamaduni huo umekuwa ukirithishwa mpaka kwa watoto wao. Huu ndio ukweli ambao hauna ubishi. Siyo kwa sababu wamezaliwa na akili nyingi sana au wana uwezo mkubwa wa akili walizopewa na Mungu zaidi ya waafrika.

Mimi kama ungeniuliza kwa nini nchi za Afrika hazisongi mbele haraka kiuchumi ningetoa sababu kuu moja tu kwamba, "waafrika hawasomi vitabu". Hii ndiyo sababu kuu ambayo ningeiweka kuwa ya kwanza inayofanya bara la Afrika kubaki nyuma kimaendeleo kwa sababu wananchi wake hawana msisimko wa maendeleo katika bongo zao. Bila kujisomea maandiko yanayosisimua ubongo na akili inakuwa vigumu kwa mtu kujitutumua kuyaendea mafanikio. Kusisimua ubongo vyaweza kufanywa kupitia kujisomea vitabu au kuhamasishwa kupitia vipindi vya redio na televisheni jambo ambalo Afrika ni nadra kuona likifanyika.

Katika nchi zilizoendelea usomaji wa vitabu uko juu sana. Kwa mfano kwa mujibu wa utafiti, bilionea mmoja wa Marekani husoma wastani wa vitabu 2 kwa wiki moja sawa na vitabu 8 kwa mwezi au vitabu 96 kwa mwaka. Matajiri wote wanaosifika kwa utajiri wao siri yao kuu ni kusoma vitabu mbalimbali kuhusu pesa, kuhusu utajiri, kuhusu afya, nk na wala siyo akili zao kubwa kuliko sisis waafrika. Kama watanzania kwa mwaka hata kusoma kitabu kimoja ni shida, ni vigumu sana kupata maendeleo. Wenzetu waliopiga hatua za maendeleo wanasoma vitabu karibu 100 kwa mwaka. Sisi watanzania ni akina nani hata tuweze kupata maendeleo bila kusoma vitabu?

Kutokusoma vitabu vyenye kusisimua akili zetu kunadumaza mawazo. Kunadumaza utendaji wetu wa kila siku. Kunadumaza akili kukosa ubunifu. Kutosoma vitabu kunadumaza vipaji vya vijana na wazee. Kutosoma vitabu kunadumaza utendaji wa watu maofisini. Kutosoma vitabu kunawafanya watanzania kufanya kazi kwa mazoea kwenye kilimo, maofisini, viwandani na kwenye kila Nyanja ya maisha.

Kutosoma vitabu vipya kunafanya watu wasiwe na akili za kuwaza kisasa. Kutosoma vitabu kunafanya akili za Wafanyakazi maofisini na viwandani kutokuwa imara katika kufanya uamuzi haraka na wa tija. Mkulima hawezi kulima kisasa kama hasomi vitabu. Kutosoma vitabu kunawafanya watoto na watu wazima wasiwe na akili zenye kuchanganua maswala mazito ya maisha. Kutosoma vitabu kunawafanya watoto wetu na kizazi chao kutokuwa na akili tunduizi. Akili tunduizi ndizo zenye uwezo wa kuchochea maendeleo. Akili zenye kudadisi na kutafiti ndizo zenye kuleta mabilioni ya pesa. Watoto na wewe pia huwezi kuzipata akili zenye utundu wa kutafiti kama husomi vitabu vyenye kukupa changamoto.

Kutosoma vitabu kunafanya kizazi kilichopo cha wazazi kutokuwa na uwezo wa kubuni teknolojia asilia. Waafrika wengi tunazaliana sana lakini hatuzai watoto wanaokuja na ubunifu wa teknolojia mpya. Watoto wetu hawawezi kuwa na ubunifu wa teknolojia mpya kwa sababu wazazi wao hatuna akili tunduizi na tunalazimika kuwalazimisha watoto wetu wawe kama sisi badala ya kuwaacha wao wawe kama wao kwa kizazi chao. Wazazi kwa sababu hatusomi alama za nyakati tunajikuta tunataka watoto wetu wawe na akili za kwetu. Hili ni tatizo kubwa kwa afrika. Kama unataka watoto wako waweze kuishi maisha ya kibilionea, huna budi kuwazoeza kusoma vitabu mbalimbali. Kusoma vitabu ni tabia inayoweza kujengwa toka utotoni. Kusoma vitabu lazima uifanye kuwa mazoea, ni iwe utamaduni wa familia yako. Mtoto

hawezi kuwa na utamaduni ambao hukuuona kwa wazazi wake. Watoto wetu hawawezi kuwa na utamaduni ambao wazazi wao hawakuwarithisha. Wazazi tunapaswa kuwazoeza watoto wetu kusoma vitabu. Mbinu pekee ya kuwazoeza watoto kusoma vitabu ni kwa sisis wenyewe kusoma vitabu. Wazazi wasiosoma vitabu wasitarajie kuona watoto wao nao wakiwa wasomaji wa vitabu. Naam wazazi tusitarajie kuona watoto wakiwa matajiri kama hawasomi vitabu tangu utotoni.

Wazazi wanaotaka watoto wao wawe mabilionea wasitarajie hilo kutokea kama hawatawazoeza watoto wao kusoma vitabu vyenye mwelekeo wa pesa. Mbinu mojawapo ya kuwafanya watoto wawe wasomaji wa vitabu ni Kununua vitabu vyenye mvuto kwao. Mzazi unapaswa kuwa msomaji wa vitabu na kuweza Kununua vitabu pia kwa ajili ya maktaba yako ya nyumbani. Hakikisha kwamba nyumbani kwako unavyo vitabu mbalimbali vyenye kuwahamasisha watoto wako kuelekea kujitegemea kimawazo na kifedha. Mzazi jitahidi Kununua vitabu na kuwahimiza watoto kutazama maisha kwa jicho la pekee. Nunua vitabu vyenye kuwatoa watoto wako kwenye lindi la utegemezi wa akili na mawazo.

Nunua vitabu vitakavyowafanya watoto wako kuwa wabunifu na wadadisi. Wawezeshe watoto wako kuwa wachangamfu na waelewa wa mambo mengi kwa kuwaletea vitabu vya kusoma na kujielimisha zaidi. Kwa kuwaletea vitabu vyenye kuwaongezea ujuzi na maarifa mbalimbali na kuwahamasisha kuwa na mitazamo chanya kuhusu maisha yao na utajiri. Naomba ninapokaribia kumalizia kipengere hiki kwa kukumbusha kwamba njia pekee ya kuwarithisha watoto wako ubilionea ni kuwapatia vitabu vya mabilionea. Wajulishe watoto wako kuwa ndani ya vitabu ndimo ulimo utajiri wao. Ndani ya vitabu ndimo ulimo ubilionea unaoutamani watoto wako waje kuwa nao maishani mwao. Kujali kusoma vitabu wewe mwenyewe ni kujali utajiri wa watoto wako. Ubilionea kwa watoto wako

chimbuko lake litakuwa ni kusoma vitabu tu. Usitarajie muujiza wowote zaidi ya kusoma vitabu. Hakikisha kwamba unayo Maktaba ya vitabu nyumbani. Maktaba yako kwa uchache sana inapaswa isheheni vitabu, majarida, magazeti jumla visivyopungua 100 vyenye mada mbalimbali zinazohusu afya, jinsi ya kutawala fedha, jinsi ya kuupata ubilionea, maendeleo ya sayanzi na teknolojia, kilimo cha kisasa kiletacho utajiri, nk.

Hakikisha kwamba ni maktaba yenye utulivu wa kutosha. Isiwe na vitu vitakavyowafanya watoto wakiingia washindwe kusoma vitabu. Vitu kama televisheni au redio ya mziki visiwepo ili kuwafanya watoto wasome. Labda kuwepo kwa muziki wa utulivu tu na siyo televisheni. Kwa wiki wazoeze kuingia maktaba kujisomea vitabu angalau mara tatu hivi au kila siku kama hawako shuleni hasa wanapokuwa likizo.

Wahimize watoto kusoma kila siku wawapo nyumbani. Wapangie ratiba ya kujisomea kwenye maktaba ya nyumbani. Usiwaache watoto wakawa ni watazamaji wa televisheni kiasi cha kuathiri ratiba yao ya kujisomea. Kusoma vitabu kutampa mtoto wako uwezo wa kujieleza na kujiamini mbele ya watu. Kusoma vitabu kutamwezesha mtoto wako awe mtu wa kuthubutu kufanya jambo hata kama ni gumu kwa mtazamo wa wengi. Kusoma vitabu kutampa mtoto wako kuwa mbunifu sana na mwenye uwezo wa kutafiti na kuchambua maswala mengi kwa muda mfupi.

Kama unapanga kujenga nyumba yako ya kuishi kumbuka kuweka chumba maalum cha maktaba ya vitabu kwa ajili ya watoto wako na wageni wanaotembelea familia yako. Hii ni muhimu sana kama unataka watoto wako wasome vitabu na wawe mabilionea. Usifanye makosa tena kama ya watu wengi wanaojenga nyumba na Kuweka vyumba vya stoo au vya kupaki magari na kusahau maktaba ya vitabu vya familia kujisomea. Maktaba ya vitabu ni muhimu sana.

Mbinu ya -2-

Mtamkie Mtoto Kuwa yeye ni Milionea

Ukimtamkia hilo kila siku, itampatia hamasa kuwa hata wale anaowaona kuwa matajiri nao waliwahi kuwa maskini. Matamshi yana nguvu sana. Neno ulitamkalo kwa mtoto lina nguvu kubwa sana baadaye maishani mwake. Hii ni mbinu au kanuni ya muhimu sana kwa mzazi. Kama kuna jambo ambalo laweza kumfanya mtu yeyote kuwa bilionea ni msimamo wa wazazi kwa mtoto awapo mdogo sana mpaka awapo mkubwa. Ninaamini kuwa kama wazazi wangu mimi wangeweza kunilea kwa kuzingatia kanuni kama hizi za maisha ninazoziandika leo ningeweza kuwa bilionea mapema tangu nikiwa na umri usiozidi miaka 35. Malezi waliyonipa wazazi wangu ndiyo pekee yangeniwezesha kuthubutu au kuanza harakati za kuwa bilionea tangu ujanani mwangu.

Toka nizaliwe Mwezi Mei mwaka 1972 sikuwahi kuambiwa kwamba kuwa bilionea inawezekana. Wala sikuwahi kuambiwa kuwa mtu yeyote (hata mimi) anaweza kuwa bilionea. Neno kuwa bilionea nimeanza kulisoma nikiwa mtu mzima tayari tena kwa kusoma vitabu vinavyohamasisha ubongo kubadilika na kuwa bilionea.

Kwamba inawezekana kuwa bilionea nikiwa mtoto sikulisikia. Hata hivyo, siyo kosa la wazazi wangu kwani wao wangewezaje kuniambia matamushi kama hayo wakati hata wao wenyewe walikuwa maskini wa fedha, maskini wa elimu, maskini wa fikra na mali? Wangewezaje kuniaminisha kwamba ningeweza kuwa bilionea wakati hata vitabu vya kusoma mbinu za kuwa bilionea hawakuwa navyo. Elimu ya shule hawakupata. Utajiri na mali nyingi hawakuvipata. Kutokana na hali hiyo ya wazazi wangu ni wazi kwamba nisingeweza kupewa malezi ya kuwa bilionea maishani mwangu. Kwa hiyo, mzazi mpendwa

unayesoma kitabu hiki unapaswa kuelewa kwamba malezi unayowapa watoto wako ndiyo yatakayoamua hatima ya maisha yao kifedha na kimaadili. Malezi ndiyo yatakayoamua watoto wako ama kuwa maskini au kuwa mabilionea. Matendo yako na Kauli zako kama mzazi kwa watoto wako hasa zile kauli za kila siku (routine words to children) ndizo zitakazowapa ujasiri wa kuumiliki utajiri. Naam, ndizo zitakazowafanya kuwa waoga kufanya kila watakalolitaka kulifanya liwe jema au baya maishani mwao. Wakiwa wakubwa rejea yao yote ya akilini mwao (future references in their subconscious mind) itakuwa ni ile ya kutoka kwako mzazi uliyowapa enzi za kuwalea wakiwa wadogo (miaka 0-15) na kuendelea hadi kujitegemea kwao.

Kila siku hakikisha kwamba watoto wako unawatamkia maneno yenye kuwatabiria mwisho wao mwema. Taja maneno ya kuwajenga kiakili na kifikra ya kwamba kuwa mabilionea maishani mwao inawezekana. Anapoenda shueleni, anapojisomea masomo ya ziada, anapotazama televisheni, nk mweleze hamu yako ya kutaka awe tajiri mkubwa. Hata kama wewe hujawahi kushika hata shilingi milioni moja na wala hutarajii maishani mwako kupata huo utajiri wa mabilioni ya pesa, wewe watamkie watoto wako mabilioni ya pesa.

Usiwaambie kwamba pesa ni mbaya. Usiwaambie kuwa pesa ni shetani. Usiwatamkie kamwe maneno mabovu kuhusu pesa. Waeleze uzuri wa pesa. Waeleze nguvu ya pesa katika kupata mahitaji na huduma maishani. Waeleze kuwa pesa ni nzuri sana lakini watu wenye tabia mbaya wanapopata pesa huzitumia kufanya mabaya yaliyomo mioyoni mwao au duniani kama vile ulevi, ujambazi, wizi, uchawi, mauaji, ukahaba, matusi, kuvaa nguo mbaya, nk. Lakini kwa watoto wazuri wenye tabia njema wakiwa na pesa nyingi huzitumia kusaidia watu wasio na uwezo kwenye jamii kama vile yatima, wajane, wakimbizi, wakoma, na wengine wenye majanga makubwa katika jamii.

Epuka kuwapa watoto maneno ya kukatisha tamaa kuhusu mafanikio yao kifedha. Unapokuwa huna pesa usiwaambie watoto wako kuwa pesa ni ngumu kupatikana. Waambie kuwa hujapata pesa sasa hivi lakini siku za baadaye unatarajia kupata pesa nyingi. Usiwaambie watoto, "hivi nyie watoto mnadhani pesa zinachumwa kwenye majani ya miti?", Nyie watoto hamuoni kuwa pesa ni ngumu kupatikana?" sentensi kama hizo usimtamkie mtoto wako unayetaka awe milionea hapo baadaye atakapokuwa mtu mzima au kijana kuanzia miaka 21.

Neno kuwa milionea au bilionea(hata kama wewe siyo milionea wala bilionea kwa sasa) lisiwe zito au gumu kutamkwa ulimi mwako. Hata kama wewe siyo milionea wala bilionea kwa sasa haikuzuii kuwaza kibilionea na kutamani wanao kuwa mabilionea. Unaweza kuwatamkia watoto wako maneno ya wao kuwa mabilionea baadaye. Mfano waweza kusema, " … mwanangu nataka usome sana uje kuwa bilionea mkubwa Afrika…." Au waweza kumwambia, "…..mwanangu mzuri pamoja na kwamba mimi siyo tajiri sana kwa sasa nakuombea wewe na kukutakia maisha ya kitajiri zaidi ya haya ya kwangu, ndiyo maana nafanya kila niwezalo kukufanikisha wewe, Mwanangu najitahidi kukusaidia uwe bilionea, nataka baadaye ukiwa mkubwa uwe tajiri sana kama Reginald Mengi. Nataka baadaye mwanangu ukiwa mkubwa uwe bilionea kama Said Salim Bakheresa, n.k.

Waeleze watoto wako kuwa una ndoto ya kuwaona wao wakiwa mabilionea miaka ijayo panapo uhai. Mwambie mtoto asome sana shule aje kuwa bilionea. Mzazi badala ya kumwambia mtoto wako asome sana akiwa mkubwa aje kuajiriwa kama Daktari, mwalimu, Rubani, Rais, Mbunge, Waziri, nk mwambie asome sana apate maarifa na uzoefu utakaomsaidia kuwa bilionea. Kamwe, usiwatamanishe wanao hata wana wa wanao maisha ya kuajiriwa kama unatamani wawe mabilionea. Watamanishe watoto wako kuwa na maisha kibilionea. Usiwatamanishe

watoto wako kuwa Wafanyakazi wa kuajiriwa tu na wengine au serikalini. Katika karne ya sasa epuka kuwahimiza wasome sana shule ili waje kupata kazi nzuri za kuajiriwa. Sisemi kuwa kuajiriwa ni vibaya, lakini jitahidi sana kila unalowahimiza kufanya lilenge kuwafanya kuwa matajiri mabilionea maishani mwao. Fanya hivyo hata kama wewe mzazi siyo tajiri wala bilionea kwa sasa. Kama wataajiriwa na mtu au serikali watafanya hivyo kama mlango wa kuanzia tu kuelekea safari yao ya kuwa mabilionea.

Elewa kuwa kile unachomuotesha na kumtabiria mwanao ndicho kinajengeka kuwa ndoto yake ya baadaye. Unachojenga kichwani mwake tangu akiwa bado mdogo ndicho kinaendelea kutunzwa katika ubongo wake au fikra zake ambazo waingereza husema, ***"subconscious mind or brain writes the words to be used in many future reference and decisions".***

Ukweli ni kwamba kile kilichotunzwa na ubongo wa mtoto wako tangu utotoni, hasa kile alichosikia kutoka kwa wazazi au walezi wake ndicho kitakachokuwa kinamsukuma akifikie na awe nacho maishani mwake. Mapambano yote atakayokuwa anayafanya maishani mwake yatategemea mzazi alivyomjenga mtoto wake kuyaona maisha kuwa ni mapambano. Kama hukumjengea fikra na utamaduni wa kuyaona maisha kama mapambano hataweza kupambana na umaskini. Mapambano dhidi ya umaskini lazima iwe kama vita ya kudumu maishani.

Kumbuka kuwa hapo baadaye mtoto wako hataweza kuwa bilionea kama ubongo wake utakuwa unakataa uwezekano wa hilo kutokea maishani mwake. Hii inakuwa sahahi zaidi kwa watoto ambao kamwe hawakuwahi kupandikizwa mbegu au ndoto za kuwa bilionea maishani mwao tangu walipokuwa wadogo. Kwa hiyo kama ubongo wa mtoto akingali mdogo ulijazwa ndoto za kuwa tajiri bilionea mkubwa maishani mwake, hakika ndoto hiyo itatimia kwake kuwa hivyo hivyo.

Elewa kwamba wewe unapaswa kuwalea watoto vyema ili nao wasifanye makosa kama yako wewe mzazi uliyoyafanya kwani nafahamu kuwa hakuna mzazi ambaye hakufanya makosa fulani. Sisi wazazi, Maisha magumu tuliyoyaishi kamwe tusitake na watoto wetu wayaishi au wayarithi. Kama wewe mzazi ulikuwa unatembea miguu peku peku mitaani au shuleni usitake na watoto wako waishi maisha kama hayo. Kama ulikuwa unavaa nguo za midabwada au masempele usitake na watoto wako nao wavae hivyo. Kama uliishi kwenye nyumba isiyokuwa na umeme, nyumba isiyokuwa na maji wala vyoo vya kisasa usiwalazimishe watoto wako kuishi kwenye nyumba ya hivyo.

Usitake watoto wako wajenge juu ya msingi wako hata kama msingi wako huo ulikuwa mbovu ambao hautawawezesha kuwa mabilionea. Kilichokufanya wewe mpaka ukawa siyo bilionea tangu ukiwa na miaka 25 hadi sasa unaposoma kitabu hiki kisikufanye leo uwazuie watoto wako kuwa mabilionea katika enzi zao watimizapo miaka 25 au zaidi. Hata kama wewe siyo bilionea leo fursa zilizopo na zitakazokuwepo kwenye uso wa dunia zitawawezesha watoto wako kuwa bilionea. Kinachotakiwa kwako ni kuwaonesha ukweli kwamba wao wanaweza kuwa mabilionea hata kama wamezaliwa katika familia maskini. Akili yao inapaswa kufunguka kulingana na malezi au maneno ya busara unayowatamkia ukiwa nao au ukiwa mbali nao.

Watamkie Baraka tu. Watabirie ubilionea. Watabirie na Watakie maisha yenye heri na utajiri mkubwa wenye amani na utulivu mpaka wajukuu wao. Epuka kuwalaani watoto wako. Epuka kuwasema vibaya. Watamkie maneno mema. Maneno na Matendo yako ya kila siku yaoneshe watoto wako kwamba wao wanapaswa wawe na maisha tofauti na ya kwako. Kama wewe siyo bilionea, hali hiyo haiwazuii watoto wako kuwa mabilionea maishani mwao. Kama wewe unayesoma kitabu hiki tayari ni tajiri kwa kiasi fulani (iweleweke kuwa ninaposema mtu fulani ni tajiri milionea hapa nina maana ya mtu mwenye kipato kisichopungua wastani wa Tshs 150,000 kwa siku sawa na wastani wa kipato cha shilingi 4,500,000 kwa mwezi.

Aidha,ninaposema bilionea namaanisha kuwa ni mtu mwenye kipato kisichopungua wastani wa Tshs 10,000,000 kwa siku yaani wastani wa shilingi 3,000,000,000 kwa mwezi) Kila unalolifanya kwa ajili yao unapaswa kuwalenga wao ili waje kuwa matajiri na mabilionea kukuzidi wewe hata zaidi ya kizazi chao cha nne. Kwa hiyo kama unakubaliana na mimi, hata vipindi vya televisheni unavyovipenda kuvitazama kila siku ukiwa na watoto wako, magazeti unayoyasoma mbele yao, vitabu unavyonunua kila siku ili uvisome au wao wavisome, jitahidi vyote vilenge kuhakikisha kuwa ni vya kuwajenga kisaikolojia na kuwahamasisha kuwa mabilionea watakapokuwa wakubwa. Ninaposema watakapokuwa wakubwa naamanisha watimizapo umri wa miaka 21 na kuendelea hadi uzeeni.

Jinsi wewe mwenyewe unavyojituma kwenye kazi za mikono, kazi zako au miradi yako uliyonayo sasa, je zinawapa mwanga na ujasiri wa kwamba unataka na wao waje wawe wachapa kazi matajiri? Je unawahimiza kujituma kwenye kazi zao za mikono na za akili kwa mifano? Neno bilionea, neno milionea, neno tajiri, na mengine yanayofanana na hayo yanapaswa yasiwe magumu kutamkwa ulimi mwako mbele ya watoto wako au mbele ya watu au mbele ya wageni wanaokutembelea nyumbani. Usionea haya wala aibu kuwatamkia mbele ya watu mfano wa sentensi kama hii, “nataka watoto wangu wawe mabilionea maishani mwao ndiyo maana nafanya hivi…….” Ukifanya hivyo kwa watoto wako tangu wakiwa na umri wa miaka 0 hadi 15, hakika watakuwa watoto wa kipekee, naam watakuwa matajiri wakubwa wa fikra huru, fikra tunduizi, fikra kubwa na pana na kwa kuwa na fikra pana hivyo, itawapandisha kifedha hadi kuwa mabilionea. Zingatia kuwa hakuna mtu tajiri duniani aliyezaliwa akiwa bilionea. Wala hakuna watu ambao Mungu aliwaumba wakiwa mabilionea. Mabilionea ni watu kama wewe. Mabilionea ni watu waliowahi kuwa masikini kwa namna mmoja ama nyingine.

Mbinu ya -3-

Wajengee Watoto Msimamo wa Kujitegemea

Kuwajengea msimamo wa kuwa matajiri, watoto wako lazima wawe na msimamo wa kujitegemea tangu wakiwa wadogo sana. Kujitegemea ni swala la kisaikolojia zaidi kuliko uwezo wa kiuchumi au kifedha. Mtu yeyote asiyejitegemea kifedha hufanya hivyo kwa sababu ya malezi aliyoyapata toka kwa wakubwa zake. Hakikisha kila siku unawatayarisha watoto wako waje kujitegemea siyo kiuchumi tu bali hata kifikra.

Tanzania iliwahi kuanzisha sera ya ujamaa na kujitegemea kati ya miaka ya 1960 na 1970. Hata hivyo sera hiyo iliendelea kukosa mashiko miongoni mwa wananchi na watendaji serikalini hasa kuanzia miaka ya 1990 ambapo taifa liliacha kukumbatia sera hiyo ya ujamaa na kujitemea kwa vitendo hasa baada ya kuanzishwa kwa siasa za mlengo wa kuendekeza kuomba misaada kutoka mataifa matajiri duniani.

Serikali ya Tanzania iliendelea kuegemea na hata sasa bado imeendelea kuwa egemezi kwenye sera ya kuomba misaada ya maedeleo ni mikopo kutoka mataifa yaliyostawi kifedha na kiuchumi ili kuweza kusaidia watu wake kielimu, kiafya, miundombinu ya umeme na barabara, bandari na usafiri wa anga. Ukichunguza kwa makini utagundua kuwa hali hii ilisababishwa na watanzania kwa asilimia kubwa kuangukia kwenye utamaduni wa kupenda kusaidiwa.

Utamaduni huu pia umeendelezwa na waumini wa madhehebu ya dini kubwa zilizopo Tanzania yaani Ukristo na Uislam. Madhehebu mengi ya dini hizi yameendelea kufanya mabo yao ya maendeleo kwa kutegemea kupata misaada kutoka kwa mataifa ya nje. Miradi mingi ya ujenzi wa majumba ya kuendeshea

ibada zao, miradi ya maendeleo ya waumini wao sehemu kubwa hufanyika kwa kutegemea misaada ya mataifa yaliyoendelea. Waumini wa madehebu ya dini hizo wameendelea na utamaduni huu wa kuwaomba misaada wazungu au waarabu ili wasaidie jamii zao masikini kama vile yatima, wajane, walemavu, wakimbizi, nk.

Mashirika ya dini yakaendelea kutuma na kutoa misaada kwa kila hali. Waumini wakafurahishwa sana na misaada kutoka kwa waumini wenzao walioko nchi tajiri. Waumini wakaendelea kupokea misaada ya nguo, chakula, fedha, magari, utalaam, nk. Hali hii ikazidi kushamiri tangu uhuru hadi sasa. Hadi sasa bado madhehebu mengi ya dini hizi kubwa Tanzania yanaishi kwa kuomba omba misaada kutoka mataifa yanayotuzidi kiuchumi. Maaskofu na Mashekhe bado wanazunguka huku na kule kwa kuandika barua au miradi na kuiombea misaada. Bado kuna watu makanisani na misikitini wanaona fahari kusaidiwa.

Hali hiyo ni hatari sana kwa taifa ambalo halijapiga hatua kubwa kiuchumi hadi kuwa linalojitegemea. Tatizo kubwa ni kwamba utamaduni huo uliondelezwa na madhehebu ya dini hapa Tanzania umepokelewa na watendaji wa serikali. Watendaji wa serikali karibu wote wamajaa mawazo ya kupenda kusaidiwa.

Wengi hawana mipango mikakati ya kujitegemea kama ilivyo kwa mashekhe na wachungaji wa madhehebu yetu ya dini. Kuanzia ngazi ya juu hadi ya chini, viongozi wengi bado wanajiskia fahari kuomba misaada kutoka sehemu mbalimbali duniani na kuleta misaada hiyo kwa wananchi. Kila kiongozi anapigana kumbo na mwenzake kujaribu kwenda kuomba misaada huku na kule. Wengi wao hakuna mwenye mkakati wa kujitegemea kifedha na kiuchumi. Tatizo hili waweza kulikuta kuanzia kwa mfanyakazi, mkuu wa kitongoji, mtendaji wa kijiji, mtendaji wa kata, mkuu wa Idara, mkurugenzi, diwani, mbunge, waziri hadi Rais. Utamaduni wa kuwategemea wengine ndio watuletee

pesa za maendeleo umeendelea kuathiri watu wengi makanisani, misikitini na serikalini. Kutokana na kuathirika huko, hata wazazi wengi pia huwalea watoto wao kwenye mwelekeo huo huo wa kusubiri kusaidiwa. Watoto wa kike wamelelewa kutaka wasaidiwe na watoto wa kiume. Mtoto wa kike anajiona hawezi kufanya jambo fulani linaloonekana kufanywa na wanaume. Mtoto wa kike anapenda asaidiwe pesa na wanaume.

Kwamba mwanamke hawezi hata kumpenda mwanaume mpaka eti apewe kitu fulani au pesa za matumizi. Kwamba wanawake ni watu wa kusaidiwa na wanaume ndipo waweze jambo fulani kulitenda. Kwamba mwanamke hata kama anacho kipato chake binafsi eti anapaswa kuendelea kusaidiwa na mwanaume!!! Hii ni hatari sana kama itaendelea kushamiri kwenye kizazi na kizazi chetu na cha baadaye.

Kama unataka kizazi chako kiwe cha tofauti, wafundishe watoto kuwa wajasiri hata kama ni watoto wa kike au wa kiume. Jinsia ya watoto wako usiiweke mbele kama kizuizi chao cha kuweza kufanikiwa baadaye hadi kuweza kuwa mabilionea. Makosa ya malezi ya utegemezi yaliyopo makanisani, misikitini na serikalini usiyafanye wewe na wala usithubutu kuyarithisha watoto wako.

Watoto wako wafundishe kujiamini, kujitegemea, kuwa na miradi na makampuni yao binafsi, kumiliki mali na ardhi zao, wafundishe kutoa misaada badala ya kuomba misaada. Wafundishe kujitegemea kiakili badala ya kutegemea akili za wengine. Wafundishe kujitegemea kifedha na siyo kutegemea kupewa pesa na watu. Watoto wako kama ni wa kike wazoeze kuishi kwa kujitegemea kiuchumi na wala wasiwe wategemezi kwa namna yoyote kwa wanaume. Wafundishe na wazoee kuona kuwa kuna kupata na kukosa maishani. Wajue na kuzoea kuishi huku wakizingatia kwamba kuna watu maskini na matajiri. Kuna wakati wa furaha na wakati wa huzuni duniani. Kuna wakati wa

kustarehe na kuna wakati wa kuchapa kazi. Waeleweshe watoto wako kuwa kuna watu wanyonge na kuna watu wenye nguvu. Waelewe kwamba duniani kuna njaa na kuna wenye shibe. Watoto wako waelewe kuwa kuna wakati wa kuzaliwa na wakati wa kufa hivyo wajiandae kwa kila tukio. Wajulishe watoto wajue sana kuwa kuna nyakati za ujana na nyakati za uzee. Yaani wafundishe kuona pande mbili za maisha. Wasiozoee upande mmoja wa maisha.

Ukiwafundisha watoto wako kuwa kuna pande mbili za maisha hawatakuwa na majivuno wala kiburi maishani. Hawatakuwa na dharau kwa watu maskini wala hawatawatambia watu wengine kuhusu utajiri walio nao. Kwa sababu watajua kwamba kuna watu wenye utajiri mkubwa kuwapita wao. Kitu muhimu kwao watoto wafundishwe kuchagua upande wa mema badala ya mabaya. Watoto wafundishwe kujua kuwa kama maisha yana pande mbili za mema na mabaya wao wafundishwe kuchagua mema. Ubilionea ni jambo jema, hivyo wafundishwe kulichagua hilo. Usione aibu kuwatabiria ubilionea maishani mwao.

Watoto wako wanapaswa waelezwe waziwazi kuhusu hali halisi ya maisha tangu wakiwa wadogo yaani kuanzia wakiwa na umri wa mwaka 1 hadi 15. Usisubiri mtoto wako ameshakuwa mkubwa na amemaliza masomo ya shule ya msingi au sekondari au chuo kikuu eti ndipo uanze kumweleza maana ya maisha.

Usisubiri amemaliza darasa la saba ndipo umwambie jinsi ya kuwa bilionea. Ni hatari sana kwa maisha yake ya baadaye. Maswala yote yahusuyo afya ya uzazi, mabadiliko ya maumbile kwa kijana au binti anapaswa awe anaambiwa tangu akiwa na umri mdogo wa miaka 2 hadi 15. Mwambie kuhusu maswala yote ya fedha, mahusiano ya kijinsia, maisha ya ubilionea, nk vyote hivyo ni vyema mtoto aanze kuambiwa mapema kabla ubongo wake haujaanza kujazwa vitu visivyofaa kutoka katika jamii inayomzunguka.

Kwa hiyo; mzazi hakikisha kuwa msimamo wa kujiajiri badala ya kuajiriwa ndio unakuwa msimamo wako tangu akiwa mdogo. Usimpandikizie mawazo ya kuajiriwa kama vile ndiyo njia pekee itakayomkomboa maishani. Usimwambie kila siku kazi za kuajiriwa bali mwambie kila siku kazi za kumiliki makampuni ya biashara, makampuni ya na viwanda, nk.

Mpe ndoto ya kuwa tajiri bilionea mkulima wa kisasa badala ya kumpa ndoto ya kuwa afisa kilimo. Mpandikizie mtoto ndoto ya kuwa mfugaji mkubwa wa kisasa badala ya kumpachika ndoto za kuwa Afisa Mifugo wa serikali. Mpandikizie ndoto ya kumiliki Hospitali kubwa na ya kisasa badala ya kumwambia asome sana aje kajiriwa kama daktari.

Mwambie asome sana ili aje kuwa mmiliki wa shule nzuri na ya kimataifa badala ya kumhimiza asome sana ili awe mwalimu. Mwambie kuwa anatakiwa asome shule sana ili baadaye aje kumiliki meli kubwa za uvuvi badala ya kumwambia asome sana aje kuwa afisa uvuvi. Mwambie asome sana ili aweze kumiliki ndege yake ya biashara badala ya kusoma sana Ile awe Rubani. Mwambie asome sana shule ili aje kuwa mmiliki wa chuo kikuu chake binafsi badala ya kumwambia asome sana aje kuwa Mhadhiri wa Chuo kikuu. Mwambie asome sana siyo aje kuwa mwalimu bali aje kumwa mmiliki wa shule yake binafsi.

Mhimize mtoto wako kusoma sana uandishi wa habari siyo aje kuwa mwandishi wa habari bali aje kumiliki kituo binafsi cha Televisheni na Redio au gazeti lake binafsi, au studio yake binafsi. Usimhimize mtoto kusoma ili aje kuwa mtumishi wa kuajiriwa kwenye taasisi zilizopo bali mhimize asome sana ili aje kuanzisha na kuwa mmiliki wa taasisi inayoajiri wengine badala kusaka elimu ili aje kuwa mwajiriwa wa taasisi zilizopo. Malezi kama haya yakisambaa sana, ndipo uchumi utakapostawi sana kuanzia ngazi ya mtu mmoja mpaka ngazi ya taifa zima. Tatizo kubwa lililopo Tanzania la kutopiga hatua kubwa za kimaendeleo

ni malezi ya utegemezi yaliyopo au ambayo yamekuwepo tangu enzi za Mwalimu Nyerere hadi sasa. Mifumo ya elimu yetu Tanzania kuanzia chekechea hadi chuo kikuu inawanafundisha watoto wetu kukariri maneno na kufaulu mitihani badala ya kuwafundisha kuwa wadadisi na wachambuzi wa mambo kwa upana. Hakuna wanaofundishwa kupenda kuandika vitabu wala kujisomea vitabu baada ya kuhitimu masomo. Shule na vyuo vinatoa wahitimu wasiosoma vitabu tena baada ya kuhitimu. Shule zetu zinawafanya watu wajengewe fikra za kuajiriwa tu. Akili na fikra zao zimejengwa kutegemea kusaidiwa zaidi badala ya kuwawezesha kuwa na fikra huru, tunduizi na udadisi ambao ungewawezesha kujiajiri na kutajirika zaidi.

Kumbuka kwamba watoto wanawaamini sana wazazi wao kuliko mtu yeyote. Kama unamwambia mtoto kuwa kwa kumiliki vitu kama hivyo nilivyoeleza hapo juu kwenye aya iliyopita ndipo atakuwa na maisha bora duniani, kwa nini mtoto ubongo wake usiyatunze hayo hivyo hivyo. Kwa nini akili na maarifa yote anayoyapata asiyaelekeze huko. Hakika mtoto atafuatilia na kupambana na vikwazo vyote mpaka atakapomiliki chuo kikuu chake binafsi kama ndoto yake ilivyokuwa tangu utotoni.

Je, mtoto wako wewe hupendi aje kuwa ndiye mmiliki wa chuo kikuu fulani hapo baadaye? Je, hungependa kumwona mtoto wako ana miliki kiwanda cha kutengeneza magari badala ya kuwa dereva wa magari ya watu wengine? Hupendi mtoto wako amiliki kituo cha televisheni badala ya kuwa mtangazaji wa kituo cha televisheni? Unaonaje mtoto wako akimiliki shule kubwa ya kisasa inayofundisha watoto wengi badala ya kumona mtoto wako akiwa mwalimu wa watoto wengi? Je, wewe ungependa awe mwalimu au mmiliki wa shule?

Mbinu ya -4-

Nunua ardhi Kubwa kwa ajili ya Wajukuu wako

Hii ni mbinu ya nne ambayo wazazi wenye akili kubwa huifanya. Hii itakusaidia kumpatia mtoto wako na watoto wa watoto wake pia kuishi maisha ya kibilionea. Ni mnyororo wa fedha usiokatika katika ukoo wako. Ifahamike kuwa hapa Tanzania swala la ardhi bado liko vizuri kisheria na kikatiba kwamba kila mwananchi anaruhusiwa kumiliki ardhi.

Hii ni fursa nzuri kwa wazazi kuhakikisha kwamba watoto wao wanamiliki au kununuliwa ardhi mapema kabla ardhi yenyewe haijanunuliwa na watu wachache wenye pesa nyingi. Nunua ardhi kwa sasa kabla ardhi haijakwisha Tanzania. Kumbuka watanzania wanaongezeka kila siku mamia kwa mamia lakini ardhi ni ile ile haiongezeki tangu enzi za mkoloni na haitaongezeka milele. Kwa hiyo kwa kasi iliyopo ya ongezeko la watu Tanzania, hitaji la ardhi litaendelea kuwa kubwa sana na huenda itafika kipindi ardhi itaadimika na kuwa kama dhahabu.

Kumbuka kuwa endapo matajiri wachache watahodhi ardhi kubwa Tanzania itakuwa vigumu kwa wazazi wasiokuwa na pesa nyingi tena kuweza kupata ardhi ya kuwapatia watoto kuwa urithi wao wa baadaye. Kumbuka kuwa bila kumiliki ardhi itakuwa vigumu kuweza kumiliki utajiri mkubwa sana kwa miaka ijayo. Huwezi kuwa bilionea bila kuwa na ardhi miaka ijayo. Watoto wako hawataweza kuwa mabilionea kama hautawaachia urithi wa ardhi kubwa na elimu kubwa.

Kama wewe ni mzazi mwenye watoto; acha utamaduni wa kujipenda sana hadi kuwasahau watoto wako kuwanunulia viwanja na mashamba yatakayowasaidia kuwa mabilionea hapo baadaye. Usijitazame wewe bali watazame wanao. Huo ndio

upendo wa kweli kwa watoto wako. Ukweli ni kwamba itakuwa ni vigumu watoto wako kuwa bilionea kama hawamiliki ardhi iwe ya kwao au ya kukodi. Narudia kusema, miaka mingi ijayo Tanzania, swala la ardhi litakuwa tatizo kubwa sana.

Hii itaendelea kuwa hivyo kwa sababu ongezeko la watu Tanzania haliendani na ukubwa wa ardhi ya nchi yetu. Na ukweli ni kwamba kwa Kadri watu watakavyoongezeka kila mwaka ndivyo na ardhi iliyopo mikononi mwa watu maskini itakavyozidi kuwatoka kuelekea ka watu wenye utajiri mkubwa. Kwa hali hiyo kila mzazi ajue kuwa kuuza ardhi yoyote ni sawa na kuuza utajiri wa watoto wake kwa watu wengine. Kuuza ardhi ni kuuza umilionea wako na wa watoto wako.

Kwa hiyo, miaka mingi ijayo mwenye mali au tajiri atamnyang'anya ardhi asiyekuwa na mali. Inakisiwa kwamba Tanzania itakuwa na watu wapatao milioni 80 ifikapo mwaka 2050 yaani miaka 35 ijayo kuanzia mwaka 2015. Hii ndiyo kusema kwa mfano, mtoto mwenye miaka 5 kwa sasa 2015; ifikapo mwaka 2050 atakuwa ndiyo kijana mwenye umri wa miaka 30 tu. Huu ni umri ambao utakuwa ndiyo wa kumiliki utajiri mkubwa kama wewe mzazi utamwekea msingi bora wa elimu na ardhi.

Kumbuka ifikapo mwaka 2050 ardhi Tanzania itakuwa adimu sana kama ongezeko la watu litaendelea kwa kasi kubwa kama ilivyo sasa. Hakikisha kwamba unanunua mashamba kwa sasa kabla hujaondoka duniani ili watoto wako wasiwe na taabu kupata ardhi. Nunua ekari tano, kumi, ishirini, sitini, mia moja, n.k yaani nunua ardhi kadri uwezavyo. Nunua hata kama ni mbali na mji unaoishi kwa sasa. Kwa mfano; ukiweza Kununua ardhi ipatayo ekari 10 au zaidi ndiyo kusema kwamba hata kama una watoto wanne (4) kila mmoja wa watoto wako atakuwa na umiliki au urithi wa wastani ekari 2.5. Ukiwaachia

urithi wa ardhi ya ekari 10 wanaweza kuitumia kwa uchumi wao na watoto wao hata watoto wa watoto wao. Hata wakisema wajenge na kumiliki chuo kikuu chao binafsi au taasisi yoyote ya biashara au majengo ya biashara kwenye ardhi hiyo swala la ardhi kwao halitakuwa tatizo tena. Wapo wazazi wasemao kwamba watoto wenyewe watajitafutia ardhi. Huku ni kuwa na ubinafsi na uvivu wa kufikiri. Ni ubinafsi na utamaduni mbaya sana wa kutofikiria kesho ya watoto wetu na watoto wa watoto wao. Ni kukosa upendo kwa watoto wetu tunaowazaa kwani hawakujileta wenyewe duniani.

Wazazi wanaosema hivyo, kusema ukweli ni ujinga tu umewafunika bongo zao. Mzazi asiyependa watoto wake utamgundua kwa jinsi anavyotumia pesa zake kuelekea kesho ya watoto wake. Wazazi wa tabia hiyo mbaya wanatumia fedha yote waipatayo kwa sasa na hawana hata mpango kabisa wa Kununua ardhi hata kama siyo kwa ajili ya watoto wao basi hata kwa ajili yao wenyewe.

Ikumbukwe kwamba, Kununua ardhi kwa ajili ya maendeleo ya watoto wako siyo dhambi wala watoto wako hawatakudharau kwa sababu tu uliwanunulia mashamba mbali na Mwanza, mbali na Dar es slaam, mbali na Arusha, mbali na Mbeya, mbali na Tanga mjini, mbali na Morogoro mjini au mbali na hapo unapoishi kwa sasa. Kwanza watoto wako watakusifu sana. Watakuwa na faraja sana na watajisikia fahari kuwa baba au mama yao alikuwa anawaza mbali sana kwa ajili yao. Jina lako halitafutika kamwe kwenye bongo zao milele.

Kwa mfano, hata kama unaishi Dar es salaam usiogope kwenda Kigoma Kununua ardhi kwa kadri uwezavyo kwa ajili ya watoto wako kama hapo Dar es salaam unapoishi hapana tena ardhi. Na kama unaishi Kilimanjaro au Arusha usiogope kwenda Dar es salaam na hata Kigoma au Katavi kununua viwanja kama

fursa hiyo imepatikana. Kama unaishi Jijini Mwanza usione shida kwenda Sumbawanga au Tunduma Kununua ardhi na mashamba yatakayosaidia watoto wako na watoto wa watoto wako. Kama unaishi Mbeya usiogope kwenda Kununua ardhi mkoani Manyara, Mara, Arusha, Kagera, nk. Kumbuka kuwa sera na sheria za nchi ya Tanzania zinaruhusu mtu yeyote kwenda mahali popote na kuanzisha maisha huko ili mradi havunji sheria za nchi. Inasikitisha sana kuona kwamba bado kuna wazazi hawawajali watoto wao kwa kuwatafutia ardhi popote pale nchini hata kama ni nje ya miji wanayoishi kwa sasa hata kama ni nje ya Tanzania kama fursa imepatikana nakushauri ufanye hivyo.

Hakika hautajutia uamuzi wako huo baada ya miaka mitano au kumi. Usiseme kwamba hawataweza kwenda kuishi huko eti kwa kuwa ni mbali na hapo unapoishi kwa sasa. Nunua viwanja na mashamba kwa kadri uwezavyo nina hakika kabisa kwamba watoto wako watakufurahia sana maishani mwao. Watakuwa mabilionea kwa sababu uliwaandaa kuwa mabilionea. Watasimama juu ya mabega yako kama mkuu wao uliyewawezesha kufika hapo watakapokuwa wamefika. Hakika watakiri kwamba kama siyo wewe hawangeweza kufika hapo walipo. Ardhi ndiyo utajiri mkubwa unaoweza kuwaachia watoto wako na watoto wa wato wao. Anza sasa Kununua viwanja na ardhi huku na kule uwaachie watoto wako urithi wa kibilionea. Kama una watoto au mtoto usifanye kosa.

Mbinu ya -5-

Anzisha Kampuni Kwa Ajili ya Watoto Wako

Mbinu hii wamefunuliwa zaidi matajiri, maskini bado hawajafunuliwa siri na mbinu hii. Ndiyo maana watoto wa maskini wanaendelea kuwa maskini huku watoto wa matajiri wakiendelea kuwa matajiri. Na kwakweli hii ndiyo siri ambayo matajiri hawapendi kuitoa kwa watu jinsi wanavyozidi kutajirika kila siku. Ukweli ni kwamba, kumiliki taasisi yako binafsi, shirika au kampuni yako ya huduma au biashara ndiyo siri pekee inayowafanya mabilionea kuendelea kuwa mabilionea mpaka kizazi na kizazi. Wanaanzisha Makampuni ya biashara au huduma na kuwarithisha watoto wao mapema.

Pamoja na kuajiri watalaam wazuri nje ya ukoo au familia, matajiri wanafanya hivyo huku wakilenga kuwaweka watoto wao baadaye. Ni ukweli ulio wazi kwamba matajiri waliofanikiwa huajiri watu makini wenye ujuzi na uzoefu. Matajiri wengi huunda timu ya watu yenye kuleta tija kwenye kampuni zao. Kabla watoto hawajakuwa wakubwa au hawajamaliza masomo yao matajiri wengi huajiri watalaam wenye uwezo mkubwa. Matajiri wengi waliofanikiwa ni lazima wawe na timu yao inayosimamiwa kwa umakini kuelekea lengo mahususi la ndoto yao.

Hata inapotokea kifo cha mzazi, watoto wanaendeleza Makampuni ya wazazi wao kwa sababu hata watalaam wanaoajiriwa na wenye kampuni wanajua kuwa Makampuni hayo ni ya watoto wa wenye kampuni na wanajua kuwa mzazi akifariki dunia watoto wao wataendelea kuwa wamiliki wa kampuni hizo za matajiri. Kwa hiyo, kama unataka mtoto wako akimaliza shule au chuo asihangaike mtaani kutafuta ajira hapo baadaye, ni wewe mwenyewe kumwandaa. Wewe mwenyewe mwandae mtoto wako kutokukosa ajira mara tu atakapohitimu chuoni au shuleni.

Utamaduni wa kumwambia mtoto kwamba asome sana ili apate ajira nzuri ni utamaduni ambao umepitwa na wakati. Ni utamaduni wa enzi za viwanda na enzi za kilimo cha mkono (agriralian and industrial age). Katika enzi hizi za teknolojia ya habari (information Age), watoto hawapaswi kupelekwa shule ili waende kuajiriwa na serikali au mashirika ya umma. Ukitaka mwanao awe milionea baadaye wewe fungua kampuni zako za biashara ya madini, biashara ya mafuta, biashara ya gesi, biashara ya supermarkets, biashara ya hotel, biashara ya kilimo cha kisasa, biashara ya migahawa ya chakula, n.k ili kampuni hizo zije kumwajiri watoto wako baadaye. Fungua miradi mikubwa ya kiuchumi. Wekeza zaidi na zaidi kwenye miradi ambayo italeta faida kubwa na tija zaidi. Fungua kampuni zako za biashara ya aina mbalimbali.

Fungua kampuni za ufugaji kuku, ufugaji ng'ombe au ufugaji wowote wenye tija. Fungua kampuni za Ushauri au Utalaam (Consultation or professional Firms). Fungua kampuni za usafirishaji, fungua kampuni za bidhaa yoyote au huduma yoyote endelevu siyo tu kwa ajili ya watoto wako bali pia kwa jamii yako yote, nk. Ikiwezekana kampuni zako uziite majina kwa kufuata majina ya watoto wako kama ikiwezekana na kila mara mtoto awapo kwenye likizo yake ya shule mzoeshe kufanya kazi kwenye kampuni zako hata kama akiwa bado mdogo wa umri wa miaka 12. Mwelekeze na umwambie kwa nini unataka afanye hivyo unavyomwambia afanye. Mfundishe kwa upendo, kwa vitendo na kwa maelekezo.

Mfundishe kusimamia fedha za kampuni yako. Mfundishe kwa vitendo kusimamia miradi au biashara yako. Mpeleke huku na kule unakofanyia biashara zako au miradi yako. Mfanyie njia ya kuzoea kufanya biashara unazofanya kwa sasa. Mpatie maelezo ya kile unachofanya ili akielewe. Usifanye mambo mbele ya mtoto wako bila kumwambia kwa nini unafanya hivyo

unavyofanya kama unataka kumwandaa aje kuwa msimamizi wa miradi au kampuni zako za biashara au miradi yako. Huku ndiko kumrithisha mtoto wako aje kumiliki mali zako. Fanya hivyo kwa watoto wako wote wa kike na kiume. Usibague mtoto kwa sababu ya jinsi yake. Ni ujinga na umaskini wa fikra kusema kwamba mtoto wa kike ataolewa na kwenda kwa mume wake na kuamua kuacha kumfundisha kumiliki uchumi wake hapo baadaye.

Kwa hiyo, kabla zamu yako ya kuishi duniani haijaisha, hakikisha umesajili kampuni zako kisheria na ufanye hivyo ukiwa na lengo kwamba endapo wewe hautakuwepo duniani mtoto wako bila kujali ni mvulana au msichana ataendeleza kampuni zako na miradi yote. Usibague mtoto kwa sababu ya maumbile yake. Hata kama ni watoto wako wa kulea au watoto wa kambo hakikisha umeweka mpango wa uhakika ambao utawasaidia kuendelea kuishi vizuri hata kama wewe haupo tena duniani. Waandae watoto kuendelea kuishi ukiwa haupo. Ukifungua kampuni za biashara na miradi mbalimbali na ukawafundisha watoto wako kusimamia ukingali uko nao hakika miradi na kampuni zako vitaendelea kuwepo kama vile wewe bado upo duniani. Wataendeleza kampuni zako na watazisimiamia kwa ufanisi zaidi hata ikiwezekana kwa ubora zaidi yako wewe mzazi ilimradi tu ulishawapa mwanga na kuwalea katika mfumo wa kuweza kuwa na fikra huru, tunduizi na endelevu.

Makabila au mataifa ambayo yamefanikiwa kutokomeza umasikini, ni yale ambayo wazazi katika ngazi ya familia huwafundisha watoto wao kusimama kidete, huru na imara kuweza kusimamia miradi ya kampuni za wazazi wao. Mataifa au makabila kama hayo huwezesha watoto wao kuendeleza makampuni yalioyoasisiwa na wazazi wao na hivyo kuendelea kuwa mabilionea kuliko mataifa au makabila ambayo hayalei watoto wao kwa mfumo huo. Makabila au wazazi wasio wafungulia

na kuwafundisha watoto wao kusimamia miradi ya makampuni yao mara tu waondokapo duniani makampuni yao, biashara zao na miradi yao hufa pamoja nao.

Hakuna kampuni au biashara inayoendelea baada ya mzazi mwanzilishi kufariki dunia. Kama mzazi alikuwa na kampuni ya mabasi ya kusafirisha abiria na yakawa yamevuma sana mji mmoja hadi mwingine mara tu mzazi huyo afarikipo na mabasi hayo hufa pamoja naye. Biashara ya mabasi iliyokuwa inavuma sana ghafula hupotea baada ya mmiliki wake kuondoka duniani. Ukweli ni kwamba biashara hiyo hupotea kwa sababu mwanzilishi wake hakuwa amewaandaa watoto wake wa kuzaa au wa kulea kuendesha miradi yake mara tu yeye atakapoondoka duniani. Hali hii haifai kabisa. Watoto wako uliowazaa wanajisikiaje kumiliki uchumi mkubwa watakaokuwa wameachiwa na wazazi?

Mbinu ya -6-

Wazoeze watoto wako kuamka mapema asubuhi

Sababu mojawapo inayowafanya watanzania wengi waendelee kuwa masikini, ni utamaduni wa kulala sana bila sababu. Watanzania tunapenda kulala sana. Ni kweli kwamba usingizi una utamu wake hasa kwa mtu mvivu. Inakera kuamka mapema kabla ya usiku kwisha au kabla ya usingizi kwisha. Ni kweli kwamba mtoto bado anakua hivyo anahitaji muda mwingi wa kulala na kupumzika ili afya yake ya akili na mwili iweze kukua. Kutokana na hali hiyo, ni vyema kumzoeza kuamka mapema kufanya kazi za nyumbani au kufanya kazi za miradi ya familia au kampuni zako.

Wote tunajua kuwa watanzania wengi hujitahidi kuamka mapema wawapo mashuleni, vyuoni au jeshini. Lakini wawapo kwenye maisha ya kawaida wengi hupenda kulala sana. Kumbuka kuwa kulala sana mavuno yake ni umasikini. Ukilala sana utavuna umasikini wa kukutosha maishani mwako. Kwa hiyo, wazoeze watoto wako kuamka mapema hataka kama wako likizo yao ya shule au hata kama inaonekana kama usumbufu kwao kuamshwa mapema kwa ajili ya kazi za miradi ya familia. Wakumbushe kwa maneno na vitendo kwamba hakuna mtu alaliyetajirika kwa kulala usingizi tu bila kujihami na maisha ya baadaye.

Mzazi hakikisha kwamba watoto wako hawapendi kulala ovyo ovyo kama siyo lazima kwa ajili ya mapumziko ya lazima. Kuamka mapema kwa ajili ya kazi za nyumbani, kazi za bustanini, kazi za jikoni, kazi za usafi, kazi za ufugaji, nk ndio utakaokuwa msingi wa watoto kuzoea kuamka mapema kwa ajili ya maisha yao ya baadaye. Usiwaache watoto wako wapende kulala mpaka saa tatu asubuhi. Ukiawaacha hivyo, itawadumaza sana kifikra

Mbinu ya -7-

Wazoeze watoto kusoma vitabu vya Kibilionea

Hapo awali nilikueleza kuwa uanzishe maktaba ya vitabu vya kujisomea nyumbani. Pamoja na kuanzisha maktaba yako ya nyumbani, usipowazoeza kusoma vitabu, watoto wako hawatasoma vitabu hivyo. Ni vyema Kuweka utamaduni au utaratibu kwenye familia wa kuwazoeza watoto wasome vitabu siyo tu vya shule au akademiki, bali pia vya kuhamasisha akili kujua pesa ni nini na zinapatikanaje.

Baada ya kuanza kusoma vitabu vya mabilionea mwaka 2013 Desemba, mimi binafsi ninayeandika kitabu hiki nilibadilika kabisa kifikra. Fikra zangu kuhusu utajiri na mafanikio endelevu vilibadilika kabisa. Kitabu changu cha kwanza nilichosoma kikanibadilisha mitazamo ya maisha ni kitabu kiitwacho, "GUIDE TO INVESTING What the Rich Invest In, That the Poor and Middle Class Do Not" kilichoandikwa na mwandishi maarufu duniani Robert Kyosaki. Baada ya kuanza kusoma vitabu kama hivyo fikra zangu zilibadilika kabisa.

Hata watoto wangu nao pia wamebadilika kifikra kutokana na vitabu ninavyonunua na kupendelea kuvisoma nyumbani kwangu. Najutia miaka mingi niliyoimaliza bila kusoma vitabu kama hivyo. Nimekaa muda mrefu bila kupiga hatua yoyote kifedha. Natamani ningerudi ujana wangu wa miaka 25. Nimeanza kubadilika kifikra nikiwa nimeshatimiza umri wa miaka 42 ambao ni umri mkubwa sana. Pamoja na kusoma sana mpaka kupata digrii ya pili (Masters Degree) mwaka 2012 bado sikuwa na fikra sahihi za kuwekeza kwa usahihi kila pesa niliyoipata. Lakini, nilipoanza kusoma vitabu hivyo vyenye kubadilisha fikra na mitazamo hasi ya kimaskini na vinavyoongeza fikra dadisi na tajiri, fikra tafiti, fikra huru, fikra tajiri, fikra tunduizi

na vinavyoongeza uwezo mpana wa kusimamia maamuzi, hakika nilianza kuona mabadiliko makubwa kifedha. Baada ya kuwa msomaji wa vitabu vyenye fikra sahihi kifedha, maamuzi ninayoyafanya kuhusu maisha yangu na watoto wangu ni tofauti na zamani kabla sijaanza kuwa mdadisi na msomaji wa vitabu vya ujasiriamali na vya maarifa ya fedha. Nilianza kuona mbali sana na kufanya maamuzi ya busara hasa kuhusu kila fedha iliyokuwa inapita mkononi mwangu kuliko nilivyofanya miaka yote 20 ya ujana iliyopita.

Kuanzia mwaka 2013 mwezi wa Desemba nilipoanza kusoma vitabu vyenye kubadilisha fikra zangu kifedha (financial literacy and entrepreneurship inspirational books) naweza kuuita kuwa ndio mwaka niliopata ukombozi wa fikra zangu kuelekea kuwa mtu huru kifedha na kuwa tofauti kabisa kifikra na kifedha. Nina uhakika kuwa baada ya miaka mitano kuanzia 2013 nitakuwa mtu wa tofauti kabisa. Yaani natarajia kuwa nitakuwa milionea ifikapo mwaka 2018. Na ifikapo mwaka 2025 (kama tukiwa hai) nina imani ya kufikia kwenye hatua za ubilionea. Kutokana na uwekezaji ninaendelea kuufanya kwenye vitega uchumi mbalimbali naamini baada ya miaka kumi kuanzia sasa 2015 nitakuwa na hatua ya tofauti kifedha.

Hoja yangu hapa ni kwamba, bila watoto wako na wewe pia kujizoeza kusoma vitabu vya kukupa changamoto na maarifa ya kifedha, huwezi kubadilika kifikra kamwe. Watoto wako pia hawatabadilika kisaikolojia na kifikra kama hawaoni wewe mwenyewe ukisoma au Kununua vitabu vyenye fikra chanya kuhusu maisha. Kama utaendelea kusoma vitabu vya hadithi za kawaida tu au ukaendelea kujisomea vitabu vya dini yako tu au ukaendelea kusoma vitabu vya afya tu na magazeti ya kawaida tu na ukaacha kusoma vitabu vya elimu ya fedha na biashara, vitabu vya ujasiriamali, vitabu vyenye kusisimua ubongo na akili yako na ya watoto wako kifedha na kiuchumi hakika hautapiga hatua yoyote kifedha wala kiuchumi wewe na watoto wako

na wajukuu wao. Hautakuwa na fikra chanya kuhusu fedha. Utaendelea kuyaona maisha katika mwanga hafifu sana. Hali hiyo itawakuta watoto wako pia kama hukuwazoeza kujisomea vitabu. Watoto wasiosoma vitabu vyenye kuwafikirisha sana hawatakuwa na fikra chanya kuelekea maisha yao ya baadaye. Watakuwa mazezeta wa fikra. Hawataweza kuuliza maswali wala kujiuliza maswali yenye kuwaletea matokeo makubwa kifedha. Hawatakuwa na fikra tunduizi na endelevu. Kuanzia leo nunua vitabu vyenye akili ya kibilionea. Nunua vitabu ambavyo ukivisoma vinakubadilisha mtazamo wa maisha ulio nao sasa.

Kila uonapo kitabu chenye kutoa elimu ya fedha, ujasiriamali na biashara usiache kukinunua. Kisome kitabu hicho mbele ya watoto wako wakuone kuwa na wewe unasoma vitabu. Hapo utakuwa unawafundisha kwa vitendo kusoma vitabu. Anzisha maktaba ya vitabu nyumbani kwako kama nilivyosema hapo awali. Au nunua kabati ya kuwekea vitabu katika mpangilio unaovutia mtu yeyote kuchukua kitabu na kusoma. Epuka kuwa mzazi ambaye hasomi vitabu na wala hana kitabu hata kimoja nyumbani. Epuka kuwa mzazi ambaye kila siku jioni yuko baa na anakunywa pombe mpaka saa sita usiku.

Achana na utamaduni wa kunywa pombe kila siku. Anzisha utamaduni wa kusoma vitabu. Kamwe utamaduni wa kunywa pombe kila siku hautakuruhusu kusoma vitabu. Kila siku ukitafuta muda wa kujisomea vitabu utaukosa kwa sababu ya pombe zako. Kwa kutokusoma vitabu wewe mwenyewe unawarithisha watoto wako pia utamaduni wa kutokusoma vitabu wawapo nyumbani au nje ya shule. Utamaduni wa kusoma vitabu mtu awapo shuleni tu na kuacha kusoma vitabu awapo nje ya shule ni utamaduni wa kijinga na kimaskini kabisa ambao unaitafuna Tanzania. Utamaduni huo wa kijinga na kimaskini utafutwa tu na wazazi wenye kuona mbali zaidi ya kizazi cha sasa hadi cha nne kijacho.

Mbinu ya -8-

Jenga nyumba za kudumu kwa ajili ya watoto

Kuwalea watoto kibilionea inahitaji mzazi ajipange kimkakati. Kama unazaa watoto ukidhania ni Baraka kutoka kwa Mwenyezi Mungu pekee na kwa hiyo wewe kudhania huna haja ya kujishughulisha na hatima yao, utakuwa umekosea sana. Ukweli ni kwamba watoto tunaowazaa, tunawazaa kwa ridhaa yetu na mapenzi yetu. Hawazaliwi kwa mapenzi yao au kupenda kwao. Hakuna mtoto anayetuma kwanza maombi kwa wazazi wao kuwaomba wamzae. Mimba ya mtoto hutungwa bila mtoto mwenyewe kupenda. Ni matokeo tu ya wazazi wawili kukutana kwa hiari yao na kusababisha watoto kuzaliwa. Watoto uliowazaa au utakaowazaa watakuwa ni matunda ya matendo yako wewe na mwenzi wako. Mahaba yako na mwenzi wako uliyafanya bila kusukumwa na mtu.

Tendo la ndoa ulilifanya wewe mwenyewe kwa raha zako na kwa hiari yako. Naam, watoto waliozaliwa siyo wao waliokusukuma kukutana na mwenzi wako ili uwazae. Ulisukumwa na tama zako au mapenzi yako mwenyewe mpaka ukakutana na huyo mwenzio na kujikuta anabeba mimba na kuzaa mtoto. Kwa hiyo, wazazi tunanawajibika au tunapaswa kuwajibika kwa matendo yetu.Kulea watoto kibilionea inapaswa kuwa wajibu wetu wazazi ili nao wafurahie kuja duniani na waione dunia kuwa siyo mahali pa mateso kisaikolojia, kifedha na kimazingira.

Kutokuwajibika hivyo itakuwa bahati mbaya iliyo kubwa sana kwa watoto wetu. Watoto wetu watakosa raha maishani mwao na kulaani kuja kwao duniani naam, watatulaani mpaka kwenye makaburi yetu. Kwa hali hiyo sasa, hakikisha kwamba haujengi nyumba kwa faida yako tu. Usijitazame wewe unapojenga nyumba. Tazama watoto wako kama unao na hata kama hauna

watoto kwa sasa jenga kwa mtazamo wa kizazi kijacho. Usiwaze kujenga nyumba kwa sababu wewe ndiye utaishi humo, la hasha; jenga nyumba imara na ya kudumu sana si kwa ajili yako tu bali pia kwa ajili ya watoto wa watoto wa watoto wako kufaidika kifedha na kiuchumi. Tatizo la wazazi wengi wanajipendelea wao tu. Wanajiwazia wao tu. Na ili kuthibitisha kuwa mzazi unajipenda na huwapendi watoto uliowazaa wewe mwenyewe, ni pale ambapo huweki mpango mkakati wa kuwaachia urithi watoto wako hata kama umezaa watoto wa kike tu ambao mapokeo ya wengi Afrika ni kwamba watoto wa kike siyo warithi wa mali za wazazi wao.

Wengi hudhani kuwa kwa sababu watoto wa kike huenda kuishi kwa waume zao hawawezi kuwa warithi tena wa mali za wazazi wao. Hiyo ni fikra potofu. Kuzaa watoto wa kike pekee isikuzuie kufanya mikakati ya kuwaachia urithi wa nyumba na ardhi ya kutosha. Nayasema hayo kwa sababu wazazi wengi wakizaa watoto wa kike huamua kuwatelekeza kwa makusudi kwa visingizio kwamba hawajazaa watoto wa kiume watakaorithi mali zao zisizohamishika hasa majumba. Ukweli ni kwamba kama umezaa watoto na unawapenda kwa jinsia zao kama walivyozaliwa ni hakika kuwa utawapenda na kuwapa kila hitaji linalopaswa kwa kadri ya uwezo wako hata kama wote ni watoto wa kike tu na watakuja kuolewa na kwenda kuishi kwa waume zao.

Epuka kuwa mzazi mbaya anayekuwa mbaya mpaka kwa watoto wake hasa wa kike. Wajengee nyumba watoto wako bila kujali ni watoto wa kike au wa kiume kwani nao watafurahia kuwa na mzazi mwenye busara sana kama wewe bila kujali walizaliwa wanaume au wanawake. Jenga nyumba siyo za makazi tu bali pia nyumba za biashara pia. Jenga nyumba za kuwawezesha kuendelea kujipatia mapato hata kama wewe mzazi hautakuwepo tena. Weka mkakati wa kujenga nyumba za biashara kama vile nyumba za kulaza wageni mijini, hoteli za kitalii, nyumba za maduka ya biashara, nk. Yote hayo uyafanye kwa lengo kuu la kuwafanya wanao wasije kuishi maisha duni duniani.

Mbinu ya -9-

Usizae watoto Wengi zaidi ya Uwezo wako

Katika nchi nyingi za Afrika, inashangaza sana kuona jamii kubwa ikiwa na mtazamo kuwa ni fahari kubwa sana kuzaa idadi kubwa ya watoto tena kwa mke mmoja au baba mmoja bila hata tahadhari ya ardhi kuwa haitawatosha watoto hao au rasilimali walizonazo kuwa hazitoshelezi au siyo endelevu. Inatafsiriwa na imekubalika sana na jamii nyingi za Afrika kuwa mtu akizaa watoto wachache ni kama ana laana hivi.

Mama mwenye mtoto mmoja au watoto wawili tu kila mtu Afrika anamwonea huruma mama huyo kwa kuzaa watoto wawili au mmoja tu. Kila mtu katika jamii kubwa ya Afrika anamshangaa sana mama mwenye watoto wachache. Kutokana na kuzongwa na jamii nzima mzazi mwenye watoto wachache kisaikolojia hajisikii vizuri kuzaa watoto wawili tu au watatu tu. Kutokana na kuzongwa na jamii yote kwamba haipendezi kuwa na watoto wachache, kutokana na imani na sababu nyingi zitolewazo na jamii yenyewe; wazazi wengi hujikuta wakilazimika kukubaliana na matokeo ya kuzaa sana watoto na hawana mkakati wowote wa kupanga idadi ya watoto wanaolingana na ardhi iliyopo pamoja na uwezo wa kiuchumi wa kuwarithisha maisha bora hapo baadaye. Kupanga uzazi linakuwa swala lisiloingia akilini mwao kwa hoja kwamba hilo ni swala la Mungu.

Wanasema unawezaje kumpangia Mungu watoto unaowataka? Wanasema, Mungu ndiye anayepanga siyo mwanadamu. Kwa jamii kubwa kama ile ya Kinyarwanda, Burundi, Kigoma, Kagera wao husema kuwa anayezaa ni Mungu na siyo binadamu yaani , “Havyalimana” au “Bikorimana” kwa lugha ya kienyeji inayojulikana katika ukanda huo. Upande wa nchi tajiri au zilizopiga hatua kubwa kiuchumi, mitazamo na imani ni tofauti na Afrika kabisa. Ukienda kwenye nchi hizo ambazo kwa

sehemu kubwa ndizo zinazosaidia Afrika kifedha na kiteknolojia au tuwaite wahisani wetu, jamii yao hawaoni ufahari kuwa na idadi kubwa ya watoto. Kwao kuzaa watoto wengi inatazamwa kama ni mkosi na bahati mbaya. Kwenye nchi hizo ni nadra sana kwa mwanamke mmoja kuzaa watoto 8 au 12? Hii kwa wenzetu walioendelea kifedha na kiuchumi itakuwa mkosi mkubwa na inakuwa kama ni laana vile. Lakini kwa huku Afrika ni kinyume chake kabisa. Mataifa yaliyoendelea zaidi wananchi wake ni matajiri kwa kiwango kikubwa sana lakini hawana uzao mlundikano kama nchi maskini. Ukifuatilia takwimu za uzazi kwa mfano Ulaya au Amerika utakuta wastani wa watoto kwa kila mwanamke si zaidi ya watoto watatu au wanne.

Taifa la China nalo pamoja na kuwa na idadi kubwa ya watu duniani, bado sheria na sera yake ni mtoto mmoja kwa kila mwanamke. Kuzaa zaidi ya mtoto mmoja nchini China ni kinyume cha sheria kabisa. China ndilo taifa la pili ukiacha Amerika kwa wananchi wake kuwa matajiri. Siri ya wenzetu wa mataifa ya Ulaya au Amerika na China kuwa na familia zenye uwezo mkubwa kifedha ni pamoja na hili la kuzaa watoto kulingana na hali halisi ya uchumi. Kila familia inajipanga kulea watoto wanaolingana na hali halisi ya uzalishaji na upatikanaji wa fedha kwa kila familia. Ndiyo maana familia nyingi za mataifa hayo zinaweza kutoa misaada mingi kwa mataifa ya Afrika yasiyoendelea kiuchumi na kiteknolojia kama Tanzania.

Hapa Tanzania bado hakuna sera ya idadi ya watoto kwa kila familia au kila mwanamke. Kila familia inajipangia idadi ya watoto wake bila hofu ya sheria au sera za kitaifa zinazomzuia kuzaa idadi aitakayo. Hata hivyo, hali hii inaendelea kusababisha hali mbaya kiuchumi na kiafya kwa mama zetu wengi Afrika. Wanawake wengi huzaa watoto wengi kuliko uwezo wao kiafya na kiuchumi wakati mwingine kuna wanawake huzaa watoto 12 au zaidi. Katika nchi nyingi za Afrika inakuwa fahari wanawake kujisifu mbele ya watu kuwa na idadi kubwa ya watoto. Bado

hulka ya wataanzania wengi ni kujisifia sana kuona wakiwa na idadi kubwa sana ya watoto. Unaweza kukutana na watu wanajisifu kuwa na watoto lukuki huku hali ya kiuchumi ya watoto hao ikiwa mbaya sana. Familia au mkuu wa familia anajivunia idadi kubwa ya watoto ambao hawana elimu, watoto hawana afya njema, watoto hawana raha ya maisha, watoto hawana mavazi ya kuwatosha, watoto hawana malazi mazuri, watoto hawana matumaini ya baadaye, watoto hawana hata cha kurithi kuweza kuwasaidia baadaye maishani mwao.

Inakuwaje mzazi ujisifie kuwa na idadi kubwa ya watoto ambao hawana raha wakati uliwazaa ukiwa kwenye raha zako? Kwa nini uwalete duniani kuwaachia majonzi maishani mwao? Kwa nini usizae watoto kulingana na uwezo wa kiuchumi ulionao? Haina maana kuzaa idadi kubwa ya watoto ambayo haina nguvu kifedha, kiafya, kielimu na kiuchumi. Kama mchambuzi wa maswala ya kijamii na kiuchumi, mimi sidhani kama ni fahari kuwa na idadi kubwa ya watoto ambao hawatafurahia maisha kama wenzao ambao wazazi wao walijipanga kikamilifu.

Mtazamo wangu ni kwamba ni vyema kuwa na idadi ya watoto kulingana na uwezo alionao mtu ili kuweza kuwarithisha mali na utajiri utakaowawezesha kuishi maisha yenye matumaini kizazi hadi kizazi. Idadi yoyote utakayoweza kuipata ya watoto iwe kwa bahati mbaya, kwa bahati nzuri ya kupata watoto wapatao 2, 3, 4,6, au 10 hakikisha unapambana kama mzazi wao kuwaachia maisha yenye matumaini maishani mwao na siyo kuwatelekeza. Usiwe miongoni mwa wazazi wanaoamua kukimbia familia zao kutokana na ugumu wa maisha unaotokana na idadi kubwa ya watoto kuliko uwezo wao kiuchumi. Huu ni woga wa maisha, wewe pambana mpaka uweze kuwapatia maisha bora. Soma kitabu hiki pamoja na vitabu vingine vya waandishi wengine vyenye mwelekeo wa kuhamasisha ubongo wako kujitambua na kubadilika. Walee watoto kibilionea tangu wakiwa wadogo sana na hakika watajitegemea maishani mwao.

Mbinu ya -10-

Usizae Watoto wa Uzeeni

Katika taaluma ya hifadhi ya jamii, watalaam wanapotaka kupanga matarajio ya baadaye kifedha na kiuchumi kwa kizazi kijacho hutazama vitu vingi ikiwa ni pamoja na maswala yote ya uzazi kama vile umri wa kuishi, hali ya vizazi na vifo, Kipato cha watu, jinsia, hali ya afya na hata siasa na sera za nchi. Maswala hayo ndiyo miongoni mwa mambo muhimu sana kutathimini unapotaka kuwa na familia yenye matumaini kifedha na kiuchumi.

Kama unatamani kuwa na familia makini na yenye mwelekeo mwema kizazi baada ya kizazi hata utakaopoondoka duniani ni vyema kuhakikisha kuwa hauzai watoto ukishatimiza umri mkubwa hasa kuanzia umri wa miaka 45 au zaidi ya umri huo. Lengo la hoja hii, siyo kwamba ni dhambi kupata mtoto kwenye umri huo ni ushauri wangu tu kwako wewe msomaji wa kitabu hiki kuelewa kwamba watoto unaowaleta duniani nao wana haki ya kufurahia maisha yao duniani ukiwepo wewe mzazi au hata utakapokuwa haupo tena.

Natoa ushauri huo kwa sababu ukizaa watoto ukiwa kwenye umri wa zaidi ya miaka 45 uwezekano wa kuwawezesha kufikia umri wa kuanza kujitegemea na kuwa mabilionea utakuwa mdogo sana hasa kama hukuwekeza kwenye vitegauchumi endelevu kwa ajili ya watoto hao. Hata hivyo, ushauri huu nauelekeza zaidi na kwa kweli unawafaa watu wote ingawa unawafaa zaidi kwa watu walioajiriwa. Kama umeajiriwa kwenye sekta mbalimbali za ajira na wewe unalenga kufanya kazi za kuajiriwa mpaka uzeeni utakapostaafu kazi ushauri huu ni wa muhimu sana. Kwa hiyo, kama unadhani utafanya kazi ya kuajiriwa mpaka utakapostaafu kwa umri wa miaka 55 au 60 kwa mujibu wa sheria

za Tanzania, nakuomba kabisa usifanye makosa ya kuzaa watoto ukishatimiza umri wa miaka 45 kwani utatimiza umri wa miaka 55 mtoto wako akiwa bado mdogo sana wa umri wa miaka 10 tu. Hutaweza kumwezesha mwanao kuwa tajiri kamwe kwani katika umri huo wewe utakuwa umeanza kupungukiwa nguvu za kuwalea watoto wako. Na kama utastaafu ukiwa na umri wa miaka 60 mwanao au binti yako atakuwa na umri wa miaka 15 tu. Umri huu ni mdogo sana kwa mtoto wako kiasi kwamba atakuwa hajamaliza hata Kidato cha nne au kupata elimu hata ya Chuo ili kuweza kuanza kujitegemea.

Utajikuta unashindwa kumwendeleza mtoto wako hasa kielimu na kimtaji kwani utakuwa umezeeka na hauna kipato kikubwa tena baada ya kustaafu. Huu ni ushauri wangu kwako hasa wewe uliyeajiriwa na hauna mpango wa kuacha kazi uende kujiajiri. Ushauri huu wa kutozaa watoto ukishatimiza umri wa zaidi ya miaka 45, unatokana na uzoefu wangu wa miaka 10 wa kuhudumia Wafanyakazi wa serikali wanaostaafu. Nikiwa nafanya kazi kwenye mfuko wa Hifadhi ya Jamii wa LAPF nimeshuhudia wastaafu wengi wakistaafu wakiwa na watoto wadogo wenye umri chini ya miaka 15 na wamekuwa wakihangaika sana kuweza kuwasomesha au kuwapatia mitaji ya kuwainua kifedha au kiuchumi. Wengine wanaamua kuwatelekeza watoto wao wajijue wenyewe Huzuni.

Kuna wazee wengi wanastaafu kazi ya ajira serikalini au kwenye mashirika binafsi na yale ya umma wakiwa na watoto wadogo wapatao 3 au 4 wenye umri wa chini ya miaka 15. Nimekutana na watumishi wa serikali wanaostaafu kwa umri wa miaka 60 huku watoto wao wa mwisho wanasoma darasa la tatu au kidato cha tatu!! Hali hii haileti afya kabisa kwa mtoto mwenyewe na mzazi pia. Mtumishi huyo wa serikali aliyestaafu analipwa kiinua mgongo kutoka kwenye mfuko wa pensheni zaidi ya milioni 60 au 80 lakini pesa hiyo inashindikana kuitumia kwa maendeleo

yake binafsi uzeeni na kujikuta akizitumia kusomesha watoto na mambo mengine madogo tu. Baada ya muda mfupi mzee huyo unakutana naye akiwa amechoka sana kiafya na kifedha.

Ushauri kama huu siyo tu unawafaa walioajiriwa serikalini, bali pia kila mtu unamfaa kuutumia kujipanga kifamilia kwani haina raha kuhangaika kulea watoto wadogo ukiwa na umri mkubwa. Kiafya na kiuchumi haipendezi pia. Haitapendeza kuona mwanamke mwenye umri wa miaka 45 akiwa anaambatana na wanawake vijana kwenda kuhudhulia kwenye kliniki huku yeye ndiye anayeonekana mzee. Haipendezi kabisa. Haina tija kifya. Haina tija kiuchumi na wala haina tija kifedha.

Haina uzuri wala haifai mwanamke mwenye umri wa miaka 42 kuendelea kuzaa watoto. Kwanza kiafya siyo vizuri kwani inahatarisha afya ya mama na mtoto. Pili, haipendezi mama mwenye umri mkubwa kujichanganya na wanawake vijana ambao bado wanazaa watoto. Kisaikolojia inaweza kumchanganya sana mama mwenye umri mkubwa ambaye bado anazaa watoto. Mama mwenye umri mkubwa siyo tu atakuwa anachekwa na wauguzi au wamama wenzake au jamii yake yote bali pia dhamira yake itakuwa inamhukumu kwamba ameshavuka umri wa kuzaa watoto.

Mbinu ya -11-

Usiwanunulie Zawadi za Pipi Watoto Wako

Wazazi wengi huwaletea zawadi watoto wao ambazo haziwasaidii kiafya wala kiakili. Wengi huwaletea biskuti na pipi. Utamaduni wa kuwaletea pipi na biskuti kama zawadi ni utamaduni wa kuendekeza ujinga na afya mbovu ya meno kwa watoto wako. Badala yake nakushauri kuendeleza utamaduni wa kusoma vitabu kwa kuwaletea zawadi ya vitabu. Mwambie mtoto nimekuletea zawadi nzuri. Ifunike zawadi hiyo kwa bahasha na aifunguapo akutane na kitabu. Mwambie umemletea zawadi itakayomfaa maisha yake yote.

Ukichunguza waafrika tulio wengi siyo kwamba hatutaki kusoma vitabu. La hasha, ni kwa sababu wazazi wetu na mababu zetu hawakutuzoesha sisi watoto wao kusoma vitabu tangu enzi zao. yaani mababu zetu walikuwa hawana vitabu vya kusoma ili hata sisi tuweze kuwaiga au kurithi tabia ya kujisomea vitabu. Ukweli ni kwamba kama wazazi wenyewe hawasomi vitabu mbele ya watoto wao itakuwa vigumu watoto nao kusoma vitabu. Nchi nyingi za Ulaya na Amerika watu wake wengi wanaosoma vitabu kwa sababu wamezoezwa kuona wazazi wao wakisoma vitabu tangu enzi za wazazi wao hadi wao wenyewe kuweza kuendeleza utamaduni wa kusoma.

Hata hapa Tanzania kama tunataka kizazi kijacho kiweze kuwa cha watu wanaosoma vitabu ni lazima sisi wenyewe kama wazazi wa leo tujioeze kusoma vitabu. Kwa kujizoeza kusoma vitabu sisi kama wazazi tutawarithisha au kuwaambukiza watoto wetu utamaduni wa kusoma vitabu. Kwa hiyo, kama unataka uwalee watoto wako kibilionea hakikisha kuwa unawahimiza kusoma vitabu vyenye mada za fedha. Uwahimize kusoma kwa vitendo vitabu vyenye elimu ya biashara. Uwahimize Kwa vitendo kwa

maana ya wewe mwenyewe kuonekana unasoma vitabu vya fedha na Kununua vitabu vya elimu ya fedha ili wazoee kuona siyo tu unavisoma wewe bali wewe pia uwahimize kuvisoma. Uwahimize kusoma vitabu vyenye maarifa ya usimamizi wa fedha ili kama maarifa hayo hawakuyapata shuleni au vyuoni wayapate kutoka kwenye vitabu. Wahimize kusoma vitabu vya elimu ya biashara ili wawe na maarifa na stadi za biashara kivitendo. Kwa kukuona wewe ukisoma vitabu vya biashara na fedha watavutiwa sana na utamaduni wako huo nao atakuwa wanasoma vitabu enzi za ukubwa wao. Hili ni swala la muhimu sana.

Hakikisha kuwa unahimiza watoto wako wa kike au wa kiume kujisomea vitabu vyenye kuongeza au kusisimua akili na ubongo wao. Wahimize kusoma vitabu vya maarifa ya fedha ili wahamasike kutafuta fedha. Kumbuka kuwa elimu ya utawala na uongozi wa fedha huwa haipatikani mara nyingi mashuleni au vyuoni. Elimu ya kusisimua mtu avutiwe kutafuta fedha mara nyingi hupatikana kwenye machapisho, vitabu, semina na makongamano yahusuyo fedha na biashara. Hakikisha unawahamasisha watoto wako kusoma vitabu vya fedha na biashara tangu wakiwa na umri wa miaka 2 hadi 15. Ukiwazoeza kusoma vitabu katika umri huo hakika hawataiacha desturi hiyo hadi wakiwa wazee. Wakisoma vitabu vya kuwapatia mabilioni ya fedha, wakisoma vitabu vya jinsi ya kuongoza biashara kubwa na makampuni makubwa hakika watahamasika kuwa mabilionea tangia wakiwa na umri mdogo.

Mbinu ya -12-

Epuka Kuwaonesha Watoto Picha za Umaskini

Picha zina nafasi kubwa sana ya kutoa elimu kwa mtazamaji. Picha watoto wako wanazozitazama kila siku zinaweza kuwafanya mabilionea au mafukara. Mtoto anatazama nini kila siku ndilo jambo la muhimu sana katika kumjengea taswira (imagination) ya utajiri mkubwa. Mtoto anachotazama kila siku ndicho kitajengeka katika ubongo wake tangu akiwa mdogo sana hadi akiwa mkubwa. Kama picha zitakazokuwa zinapita mbele yake ni zile za ukatili, picha za vita, picha za ulevi, picha za ngono, picha za ugumu wa maisha; hakika ubongo wake utajaa picha za ukatili. Naam, ubongo wake utajazwa picha za mauaji. Ubongo wake atakuwa na taswira za mauaji kila siku hadi ukubwani mwake.

Mtoto akitazama kila mara picha za mapenzi au ngono ubongo wake utakuwa umejaa taswira za ngono na hatimaye mtoto anaweza kukubuhu kwenye tabia mbaya za umalaya na ukahaba kutokana na picha za ngono alizozoezwa kutazama tangu akiwa mdogo. Baadaye Usishangae mtoto wako kama atakuwa na tabia ya kufanya vitendo hivyo vya ngono kila mara. Siri ndiyo hiyo tu. Ubongo wake utamsukuma kutenda yale yaliyoandikwa au kujaa ndani ya ubongo wake.

Kinachowafanya watoto wawe na tabia njema mbele ya jamii au wawe na tabia mbaya sana ni picha mbaya au nzuri wanazokuwanazo akilini au kwenye ubongo wao tangu wakiwa wadogo sana. Kama watoto wakijazwa picha za ufukara na umaskini akilini mwao tangia wakiwa na umri wa miaka 2, wao pia watakuwa hawana uwezo wa kuwa na fikra kubwa na chanya za kuwaza kitajiri kwa sababu ubongo wao na akili zao za tangia utotoni (subconscious mind) hazikupewa taswira

wala picha za utajiri. Mzazi kama unataka watoto wako wawe na maisha ya kibilionea, hakikisha kuwa unawaonesha watoto wako mara kwa mara picha za waliofanikiwa. Jitahidi Watoto wako kuwaonesha picha za magari ya kifahari hata kama wewe mwenyewe hauna magari mazuri kama hayo. Watoto wako watembeze mara kwa mara kwenye miradi mikubwa ya watu waliofanikiwa. Wakitembelea miradi ya waliofanikiwa kama vile miradi ya viwandani, miradi ya kilimo, miradi ya ufugaji, miradi ya ushonaji, nk watajengewa picha fulani ya kutamani kuwa kama mtu huyo aliyefanikiwa. Akilini mwao na ubongo wao kutakuwa na picha ya mtu huyo mpaka na wao watakuwa wanatamani kufanikiwa kama huyo waliyemtembelea.

Watoto watembeze kwenye majumba mazuri na ya kifahari hata kama wewe huna jumba la kifahari. Watembeze wakiwa wadogo kuanzia umri wa miaka 2 hadi 15. Waoneshe picha za watu waliojiajiri hadi kuwa na mafanikio makubwa. Epuka kuwaonesha picha za watu wabaya au waliopata pesa kwa njia za kifisadi. Kama unataka watoto wako wawe na utajiri mkubwa kuzidi huo ulionao wewe jitahidi kila mara kuwatembeza kwenye familia zilizopiga hatua kuzidi familia yako.

Watembeze watoto kwenye maeneo ya kujifunza jambo jipya ambalo nyumbani kwako halipo. Ukifanya hivyo, utawapatia watoto wako changamoto kubwa ili wasijione kuwa wanaishi familia tajiri na wakaanza kubweteka. Wakiona kuwa kuna familia zenye kuwazidi viwango vya maisha watapata picha kuwa maisha yanazidiana na watakuwa wanyenyekevu na hawatakuwa na kiburi mbele ya watoto wengine. Epuka kuwatembeza watoto kwenye majumba ya starehe kama vile baa na kasino za ulevi au vilabu vya usiku. Kuwatembeza watoto maeneo ya starehe haiwapi picha yoyote ya mafanikio na utajiri wao wenyewe kwa baadaye badala yake huwajengea picha na utamaduni wa kupenda starehe na ulevi. Kuwatembeza watoto

kwenye maeneo ambayo hayawapatii changamoto za maisha ya kibilionea au kuwatembeza maeneo ambayo watapata kuona picha ambazo haziachi alama za kitajiri kwenye ubongo wao, haitawaondoa kwenye ufukara. Hakikisha kuwa unawaonesha picha za kitajiri ili ubongo wao ujazwe picha za kitajiri na siyo za kimaskini. Kama wewe una nyumba ya kawaida yaani siyo nyumba ya kifahari hakikisha kuwa watoto wako unawapeleka kutembelea familia zenye nyumba nzuri au ya kifahari kuliko ya kwako.

Kama wewe una gari la kawaida tu yaani lisilokuwa la kifahari jitahidi kuwaonesha watoto wako picha za magari ya kifahari ili nao waanze kuwa na ndoto za kuja kumiliki magari ya kifahari. Kama unataka watoto wako waweze kumiliki makampuni makubwa ya biashara, watembeze kwenye ofisi za watu waliojiajiri na kufanikiwa ili ubongo wao uweze kujawa na picha ya kujiajiri kwenye kampuni binafsi badala ya kuajiriwa na watu wengine. Epuka kuwaonesha watoto picha chafu au za kifukara kabisa kama unataka uwalee kwenye mwelekeo wa kibilionea.

Mbinu ya -13-

Wahimize watoto kuwa wachapa kazi

Siri ya mataifa tajiri kuzidi kuwa matajiri ni hii ya kwamba wananchi wake wote wameambukizwa utamaduni wa kupenda kazi. Taifa lolote lisilokuwa na wachapa kazi haliwezi kuendelea kamwe. Mbinu pekee ya kuwahimiza watoto kuwa wachapakazi ni kwa wazazi wenyewe kuwa wachapakazi kuanzia kazi za nyumbani, kazi za bustanini, kazi za kilimo, kazi za maofisini, na kwa kila kazi inayotakiwa kufanywa ifanywe kwa bidii. Watoto wasipozoezwa kuchapa kazi tangu wakiwa na umri wa miaka 2 hadi 15 itakuwa vigumu sana kuwazoeza kufanya kazi nyingi na ngumu wakishakuwa na umri zaidi ya huo.

Hata kama ni kazi za ofisini hawatakuwa na ari ya kazi kama hawakujengewa ari hiyo ya kazi tangu utotoni. Kama ni kuosha vyombo vya nyumbani mtoto wa kike au kiume anapaswa kuachwa afanye kazi hizo za kuosha vyombo bila kumzuia hata kama wewe umeajiri mfanyakazi (house girl). Kama ni kazi za nje ya nyumba kama vile kutunza mifugo, kufagia nje ya nyumba, kulima bustani za nyumbani, na kazi kama hizo; ni vyema kuhakikisha kuwa mtoto anazifanya kazi hizo bila kumzuia wala kubagua jinsi ya mtoto.

Kama unataka watoto wako waje kuwa mamilionea na mabilionea usiwazoeshe watoto wako kukaa bila kazi nyumbani. Kama unazo kazi za kufanya nyumbani au nje ya nyumbani hakikisha kuwa unawashirikisha watoto wako tangu wakiwa na umri wa miaka 2 kufanya kazi hizo. Tafuta kazi za kufanya uwapatie. Kama ni vijana wa shule (hasa shule hizi za kisasa) wapatie hata kazi za kutumia kompyuta hata kama ni kazi za ofisini. Mpe mtoto wako afanye kwenye kompyuta kazi hizo mpaka atakaposema amechoka. Kwakuwa watoto wa kisasa wanapenda kompyuta hakika ukimpatia mtoto kazi ya kufanya

kwenye kompyuta anafurahi sana. Badala ya kukaa muda mwingi akitazama televisheni vipindi visivyo na tija kwake ni vyema akawa na kazi za kufanya hapa na pale kwani inampa uzoefu na ujuzi zaidi siyo wa kutumia kompyuta tu bali hata kufanya kazi kwa hapo baadaye. Mimi mwenyewe nimekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa binti zangu Happiness mwenye umri wa miaka 14 na Neema mwenye umri wa miaka 7; wanafanya kazi za nyumbani hata za nje ya nyumbani ili kuwazoesha kuwa wachapa kazi.

Kila mara wawapo kwenye likizo zao za mwisho wa mwaka huwa nahakikisha kuwa nakaa nao ili kuwazoeza kufanya kazi siyo za nyumbani tu hata za nje ya nyumbani. Nakuwa nao binti zangu kwenye miradi yangu na ofisini kwangu wakinisaidia kufanya hili na lile mpaka wanaposema wamechoka. Ukweli ni kwamba watoto wanapenda kufanya kazi na wazazi wao. Hata kama kazi wanazofanya siyo kazi za ndoto zao lakini kule kushirikiana na wazazi kwenye kazi au miradi ya wazazi kunawapa ujuzi na maarifa mengi ya kujitambua na kuyatambua maisha ni nini.

Mimi nina uhakika kwamba kwa jinsi ninavyokuwa nao binti zangu kwenye kufanya kazi za ufugaji kuku, ufugaji kware, kazi za ofisini kwangu na kwenye kusambaza vitabu vyangu ninavyoviandika itawajenga kifikra na hakika itawasaidia baadaye kuwa wachapa kazi. Nikiendelea kufanya hivyo kwa muda mrefu nina uhakika kuwa hawatakuwa wavivu wa kazi yoyote. Watoto watakapoanza maisha yao baadae iwe kazi za ofisini au kazi za mikono nje ya ofisi itawasaidia kuwa na fikra chanya za kazi zaidi kuliko kuwaza starehe tu na kupiga soga sehemu za kazi. Wazoeze kuona na kujengeka kifikra kuwa kazi siyo mateso. Kazi siyo adhabu bali ni fahari ya manadamu. Watoto wafanye kazi kama vile wajibu na wazoeze hivyo kila siku. Wazazi tunapaswa kuwaonesha watoto wetu kuwa kazi ndiyo msingi wa maendeleo ya watoto tangu wawapo wadogo hadi ukubwani mwao.

Mbinu ya -14-

Wafundishe Watoto kuchukia Uzembe na Uvivu

Katika kuhakikisha watoto wetu wanakuwa na akili zenye kuchukia uzembe na uvivu, ni lazima tangu wakiwa wadogo sana tuwaoneshe kwa vitendo kuwa hata sisi wazazi tunachukia uvivu. Naam, tuwaoneshe kwamba uzembe kazini ni mwiko maishani mwao. Watoto wanapaswa kulelewa kwa vitendo kwa kuchukia uvivu wa kazi yoyote hata kama ni kazi ndogo wachukie kabisa kuwa wavivu, wachukie kuwa wazembe kwa lolote lile. Wazoeze kuepuka kuwa wapiga soga zisizokuwa na tija kwa maendeleo yao. Wafundishe watoto wako kujiepusha na mazungumzo yanayoharibu tabia zao.

Wafundishe kuwa kupoteza muda kizembe na kivivu ni hasara kubwa katika kujijengea uchumi imara kwao na kwa watoto wa watoto wao. Watoto wako wanapaswa kujua kuwa muda ni pesa. Kumbuka kuwa utamaduni wa kuwajibika kwa watoto wako kutategemeana na jinsi mzazi mwenyewe alivyomlea mtoto. Ukiwalea watoto kizembe na kivivu tarajia kuwa na watoto wavivu na wazembe, naam watoto mafukara wasiokuwa na mbele wa nyuma.

Mbinu ya -15-

Wafundishe Kuchukia Dhuluma na Rushwa

Kitabu hiki kinahusu malezi ambayo mzazi akiyafuata ataweza kumwambukiza mtoto wake utajiri mkubwa uliotunguka watanzania. Tanzania ni nchi yenye Baraka tele za mali asili na mali kale ambazo zitaendelea kuwa urithi wa vizazi na vizazi kwa Tanzania. Kila kona ya nchi hii ya Tanzania kuna kila aina ya mali ambazo zipo kwa ajili ya kuwaezesha watu wote waliozaliwa Tanzania waishi maisha ya amani, maisha ya raha, maisha ya starehe na maisha yaliyotulia.

Tanzania kuna vito vya thamani kama vile Tanzanite inayopatikana Tanzania pekee. Kuna madini ya chuma, kuna madini ya almasi, kuna madini ya dhahabu, kuna mafuta na gesi, kuna misitu ya asili, kuna mito na mabonde mengi yanayofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Kuna ardhi kubwa sana Tanzania ambayo haijatumika kwa kitu chochote ambayo bado itaendelea kuwa mali ya watoto wa Tanzania watakaoendelea kuzaliwa miaka mingi ijayo.

Kuna mambo mengi sana ambayo nikiyataja yote kitabu hiki kitajaa stori za aina hiyo tu. Kutokana na hali hiyo ya kuwa na mali tele za asili, hakika hakuna sababu ya watanzania kujihusisha na rushwa wala dhuluma kwa watu wanyonge, yatima na wajane. Kudhulumu watu wengine kile walichonacho au walichostahili ni utamaduni wa mwovu sana usiopaswa kuachwa uendelee kwa watoto wala kwa watoto wa watoto wetu. Kama mzazi fanya juhudi kuwaambia kila siku au kila unapokaa nao kuwa dhuluma ni uasi na uovu mbaya sana. Jamii yenye kukumbatia dhuluma haitafanikiwa kamwe. Ukiwalea watoto wako kwenye utamaduni wa kuchukia kula rushwa na ukawaeleza maana halisi ya rushwa kuwa ni kupokea zawadi au chochote kutoka kwa

mtu yeyote ili mtu huyo apewe huduma kwa urahisi na uharaka kuliko wengine, au ni kule kupokea malipo makubwa kutoka popote yasiyokuwa sawa na kazi unayoifanya au uliyomfanyia mtu, au wakaelewa kuwa rushwa ni dhuluma afanyiwayo mtu mnyonge kwa kuombwa atoe pesa fulani ili atendewe haki fulani, nk hakika wataikwepa rushwa na hawatafanya dhuluma kwa mtu yeyote.

Kama wazazi tukiwafundisha watoto wakaelewa madhara ya rushwa na dhuluma katika jamii wakajiepusha na tukawa na jamii iliyo huru dhidi ya dhuluma na rushwa hakika, watoto wetu wataishi kwa raha na starehe katika nchi ya baba na mama zao. Mzazi wewe mwenyewe unapaswa kuwa kielelezo cha kutokubali kuomba rushwa ya aina yoyote. Tenda wema kwa watoto wa wenzio. Ni uovu mkubwa sana kuona mzazi uliyeshikilia nafasi fulani katika taasisi ya serikali au taasisi ya binafsi unaanza kuomba chochote kwa mtoto wa mwingine ili uweze kufanya jambo fulani lenye kuweza kumletea maisha bora mtanzania mwenzio.

Wewe ni Afisa Utumishi au Afisa tawala sehemu fulani, unafanya mchakato wa kuajiri vijana kwenye idara yako au kampuni yako au taasisi ya serikali inakuwaje uanze kuwaomba vijana wakupe kiasi cha Tshs 500,000 kila mmoja ndipo upitishe maombi yao ya ajira. Kwa mfano, kwenye taasisi yako zimetangazwa nafasi 10 za kazi na kwa hiyo unahitaji vijana 10 tu wa kuajiri kwenye nafasi hiyo. Walioomba nafasi hiyo wapo 60. Waliokidhi vigezo vyote vilivyotangazwa wapo labda vijana wapatao 20. Wewe ndiye mwenye uamuzi ni nani aingie au nani asiingie. Unaamua sasa kuwaambia waziwazi au LIVE kama wengine wanavyosema. Unasema, “kama hauna Tshs 500,000 pamoja na kwamba vigezo vyote umetimiza sitakupitisha kwenye nafasi hii”. Kisha unaenda kutulia ofisini kwako.

Unakaa kwenye kiti chako. Vijana wanarudi kuwaambia wazazi wao au ndugu zao ujumbe huo uliowaambia. Mzazi mwenye uchungu na kijana wake kupata kazi anaamua kumpatia kijana wake hiyo pesa. Wewe mzazi uliyekalia kiti cha kuajiri watoto wetu unapokea pesa hiyo. Vijana wapatao 10 wanakuletea Tshs 500,000 kila mmoja. Unapokea bila hata aibu. Unajipatia Tshs 5,000,000 kwa urahisi kabisa bila jasho. Unapokea jasho la wazazi wenzio ndani ya siku 5 tu za kuajiri vijana 10 umejipatia milioni tano.

Napenda kukuhakikishia kuwa huo ni uovu mkubwa ambao wewe kama Afisa Mwajiri mahali ulipo hautakuacha uendelee kuishi kwa raha. Haiwezekani ukafanya uovu mkubwa namna hiyo ukatarajia kuwa utaendelea kuwa na raha maishani mwako wewe na kizazi chako. Never, never, on earth.

Haiwezekani. Uovu huzaa uovu na rushwa huzaa laana siyo kwako tu hadi kwa kizazi chako cha nne. Kushikilia nafasi sehemu fulani isikufanye kuwa kama wewe ndiye pekee unayeweza kushikilia kitengo hicho na kukufanya ujione mungu mtu hapo ulipo. Laana iambatanayo na kula rushwa na kufanya dhuluma kutoka kwa watu wanyonge ni kubwa sana ambayo haitaenda bure maishani mwako. Kila kosa maishani huwa lina malipizi yake. Kanuni ya ulimwengu ndivyo ilivyo.

Huweze kutenda maovu halafu dunia ikakuacha salama mbele ya watu wema. Kama unatenda maovu ya kiwango hicho cha kudhulumu vijana haki yao ya kupata ajira kulingana na uwezo wao wa kielimu na maarifa na kuhakikisha kwamba bila kulipwa au kupewa rushwa yoyote hupitishi maombi ya kazi, hakika kosa hilo litakurudia tu. Upende au usipende hata kama itachukua miaka kumi au zaidi lakini kanuni ya “action and its reaction” (yaani madhara ya kitendo utendacho)itatimia kwako. Kila tendo ulifanyalo liwe jema au ouvu kwa watu wanyonge linakurudia wewe mwenyewe. Epuka kutenda uovu ili usikurudie wewe.

Mbinu ya -16-

Wafundishe Watoto Kutoa Sadaka Kwa Jamii

Sadaka inatafsiriwa kwa namna nyingi sana katika jamii yetu. Lakini kwa ujumla inaeleweka kuwa sadaka ni chochote ambacho mtu anakitoa kwa watu au jamii bila kutegemea kupata malipo kutokana na kufanya hivyo. Sadaka pia yaweza kutafisiriwa kuwa ni pesa au mali itolewayo na mtu kwa kwa watu au mtu mwingine kwa nia njema ya kusaidia wasio na uwezo ili nao waweze kujikwamua kwenye matatizo au adha inayoweza kuwa imewapata kisaikolojia au kiuchumi au kifedha.

Sadaka siyo lazima iwe pesa. Hata kutoa ushauri bure kwa mtu na ushauri huo ukawa wa manufaa kwake kifedha, kiafya, kisaikolojia, kibiashara n.k inaweza kuwa sadaka. Atoaye sadaka siyo lazima awe ni mtu tajiri sana. Kwa upande wa madhehebu ya dini sadaka imekuwa ikitazamwa kuwa ni pesa au vitu vitolewavyo kwa ajili ya kusaidia kuendesha gharama za kazi ya Mungu. Pesa yoyote itolewayo kanisani au mskitini huhesabiwa kuwa sadaka. Kwa upande wa makanisa, sadaka hugawanyika sana katika aina nyingi za sadaka kulingana na mitazamo ya wahubiri wenyewe. Kwa mfano kuna sadaka ya changizo, sadaka ya fungu la kumi au zaka, sadaka ya harambee kuchangia harusi, ujenzi, nk. Kuna sadaka ya sindikiza injili, sadaka ya malimbuko, sadaka ya shukrani, sadaka ya mbegu, na nyingine nyingi. Kwa hiyo maana au tafsiri ya sadaka inategemeana na mtazamo wa jamii au mtu mwenyewe anayetoa sadaka.

Katika kitabu hiki cha malezi ya watoto wetu ambacho lengo langu kuu ni kubadilisha mitazamo isiyo kuwa sahihi, na kujenga jamii yenye mitazamo chanya; sadaka nitaitafsiri kuwa ni vitu, mali, muda, ushauri au pesa itolewayo kwa watu wenye uhitaji mkubwa kuliko watu wengine, watu wasio na mbele wala

nyuma kiuchumi, watoto yatima, wanawake wajane, wakimbizi wa vita, watu waliokumbwa na maafa, watu waliokumbwa na majanga makubwa, walemavu, viziwi, vipofu, mafukara hohehahe, na wote wanaofanana na hao. Hiyo ndiyo tafsiri ya sadaka kwa mtazamo wa kitabu hiki cha malezi ya watoto.

Kutoa pesa au chakula au mavazi au nyumba au gari au kulipa ada za shule au kuwasaidia nauli au kuwasaidia chochote watu wenye hali duni kabisa kiuchumi hasa hao niliowataja hapo juu ni sadaka ya pekee kabisa ambayo kwa wale wanaomwamini Mungu hata na wasiomwamini Mungu pia matokeo yake huwa ni makubwa sana. Ukitoa sadaka kwa makundi ya watu kama hao kubarikiwa kwa namna zote ni halali yako. Utapata Baraka tele duniani na hata mbinguni kwa wewe unayetoa.

Kanuni ya utoaji sadaka inapotekelezwa kwa moyo mweupe usio na kinyongo huleta matokeo makubwa sana kwa mtoaji. Hata kama angekuwa mtu asiyeamini kuwa Mungu yupo yaani siyo Mkristo wala Muislam akifuata kanuni hii ya utoaji anabarikiwa zaidi na zaidi. Masharti makubwa ya utoaji ni lazima utoe kwa nia njema kabisa isiyokuwa na lengo la kujinufaisha kibiashara wala usiwe na nia ya kupata sifa mbele ya jamii. Usitake sifa wala kutaka kujulikana kwa watu wanaokutazama au kukujua.

Ukifuata masharti hayo utapata thawabu hapa hapa duniani hata baada ya kuondoka dunia sifa zako zitaendelea kuvuma kwa miaka na miaka. Kama mtu alikuwa akiwatendea wema watu wanyonge na wasiokuwa na chochote cha kumrudishia hakika Mwenyezi Mungu humrudishia mtu huyo mara mia moja ya vile alivyotoa. Kuwazoeza watoto wako kutoa sadaka ya namna hiyo itawasaidia sana baadaye watakafanikiwa kiuchumi hadi kuwa mabilionea. Kanuni hii ya kutoa sadaka kwa watu wenye uhitaji wa hali ya juu ndiyo kanuni kuu inayoweza kukusaidia wewe kuendelea kuwa bilionea. Hii ndiyo siri kubwa ambayo matajiri hawasemi lakini inazidi kuwafanya waendelee kuwa

matajiri zaidi pamoja na kutoa sana mali zao kama sadaka kwa jamii yenye uhitaji mkubwa. Unaweza kwenda kwa tajiri mmoja kumwomba akusaidie mkopo wa pesa kama Tshs 100 milioni na asikupatie lakini baada ya siku tatu ukasikia kuwa tajiri huyo huyo ametoa msaada wa vitu vyenye thamani ya Tshs 100 milioni au amesaidia watu wenye ulemavu kiasi cha Tshs 100 milioni. Usishangae kwani yeye anachofanya ndiye anayekijua faida zake. Sisi wazazi tunapaswa kuwalea watoto wetu katika mtazamo huo kwamba kutoa siyo lazima uwe umeshakuwa na utajiri mkubwa sana bali ni kutii kanuni kuu ya kutuwezesha kuendelea kuwa matajiri.

Tajiri yeyote asiyetoa sadaka kwa jamii yenye uhitaji mkubwa kama vile yatima, wajane, walemavu, wakimbizi, watoto waishio maisha magumu, familia fukara, nk hawezi kudumu na utajiri wake kamwe. Huwezi kudumu na utajiri wako au miradi yako ikaendelea kukupatia pesa nyingi kama wewe hautoi sadaka kwa hiari yako kwa jamii fukara yenye uhitaji mkubwa hata kama unatoa sadaka kanisani au msikitini. Kutoa sadaka msikitini au kanisani peke yake haitoshi kabisa na wala haileti matunda mazuri sana ikilinganishwa na kutoa sadaka kwa watu ambao hawakujui wala hujawahi kuonana nao hasa jamii ya watu wasiokuwa na uwezo wowote katika jamii.

Watoto wetu wanapaswa kuzoezwa kutoa sadaka kwa makundi ya wahitaji katika jamii bila kushurutishwa na mtu wala bila kuombwa na mtu. Wazazi tunaweza kuwazoeza watoto wetu kufanya hivyo kwa kuanza sisi wenyewe. Wazazi tunaweza kufanya hivyo kwa Kununua vitu kadhaa kama vile unga, maharage, chumvi, mafuta, nguo, vitanda, sukari, maji, nk na kuvipeleka kwenye vituo vya watoto yatima au kwa kuvipeleka kwa familia maskini sana katika jamii. Kama utapeleka nguo, chakula, au unga kwa familia maskini sana kwenye mtaa wako au mtaa wowote unaoujua hakika wewe utabraikiwa sana.

Mfundishe mtoto kuhakikisha kuwa anapotoa sadaka asitake kila mtu ajue kuwa anatoa sadaka. Kama unataka Mwenyezi Mungu akubariki sana kwa utoaji wa sadaka hakikisha kuwa unajiepusha kutoa sadaka ukiwa na timu kubwa ya vyombo vya habari. Jiepushe kuambatana na waandishi wa habari unapoenda kutoa sadaka. Epuka kutoa sadaka kwa ajili ya kujitangaza mbele ya watu. Wakristo wanajua kwamba maandiko yanasema , "utoapo sadaka yako hata mkono wako wa kushoto usijue". Hii ndiyo kanuni kuu ya kubarikiwa na mwenyezi Mungu.

Kama mzazi ungependa watoto wako wabarikiwe na Mungu kwa njia ya utoaji hakikisha kuwa wanatoa sadaka kwanza kwa watu wenye uhitaji wa kweli, pili watoapo sadaka wasifanye hivyo kwa nia ya kutaka kupewa sifa na watu, tatu watoto wako wasifanye utoaji wa sadaka kuwa ndiyo njia au fursa ya kutangazia biashara au huduma zao au miradi yao. Kama ni maswala ya kufanya huduma na bidhaa zao zijulikane (marketing) wafanye hivyo kwa kutumia njia nyingine ya matangazo mitaani, redioni, magazetini na kwenye televisheni. Haifai kujitangaza kupitia utoaji wa sadaka. Haifai kwenda kutoa sadaka kwa yatima au vituo vya watoto yatima au kwa walemavu na wajane ukiwa na vyombo vya habari. Mtu anayefanya hivyo hawezi kujipatia thawabu ya utoaji wake. Hii ni kanuni ya maisha hata kama hukubaliani na mimi lakini ukweli ndio huo.

Mbinu ya -17-

Anzisha Miradi Endelevu Kwa ajili ya Watoto

Kama unawapenda watoto wako kweli na uliwazaa kwa upendo wa kweli kwa baba yao au mama yao, hakika utawaandalia mazingira yatakayowafanya wafurahie uumbaji wa Mungu. Hakuna jambo la kusikitisha kama kuwazaa watoto wako kisha wakaishi maisha duni yasiyo na mbele wala nyuma kifedha, kielimu na kiuchumi. Inasikitisha sana. Inasikitisha siyo watoto wenyewe tu bali hata jamii inayowazunguka itasikitika kuwaona watoto wako wakiwa na maisha magumu sana ambayo hayana sura ya furaha wala amani.

Kama unataka uepushe aibu ya watoto wako kuishi maisha duni hapa duniani kuanzia pale uwapo duniani hata utakapoondoka duniani, wawezeshe watoto wako kumiliki miradi endelevu. Miradi endelevu ni nini? Ni miradi ambayo inaweza kuendelea Kuzalisha fedha kwa muda mrefu sana hata kama wewe mwanzilishi utakuwa haupo tena. Miradi endelevu ni huduma au miradi ambayo inaweza kuendelea kuwepo huku ikileta mapato kwa wanafamilia wako ikiwezekana kutoka kizazi hadi kizazi kingine. Ipo miradi mingi sana inayoweza kuleta faida kwa wakati mfupi au wakati mrefu lakini si kila mradi ni endelevu. Miradi endelevu kizazi hadi kizazi ni ile pia inayoweka mfumo wa kudumu wa kuleta mapato hata kama mwanzilishi yupo kazini au hayupo kazini kwa kipindi kirefu.

Mfano wa mradi wenye mfumo uletao pesa bila kujali kama mwanzilishi yupo au hayupo ni mradi wa shamba la miti ya mbao za biashara. Kama mzazi wa watoto akiwa na shamba la miti ipatayo 20,000 sawa na hekari kama 20 hivi na shamba hilo likawa linazalisha mbao za biashara Zipatazo 100 tu kwa siku ikiwa ni wastani wa miti 2 tu kwa siku na ubao mmoja

ukauzwa Shs 5,000 tu itakuwa Shs 500,000 kwa siku moja tu. Kama shamba lina miti 20,000 na inakatwa tu bila kupanda miti mingine shamba hilo litaishiwa miti hiyo 20,000 baada ya miaka 30 hivi. Kwa hiyo kama ukipanda miti leo hii ukiwa na umri wa miaka 30 na ikakomaa ukiwa na umri wa miaka 45 hivi ukaanza kuvuna mbao za biashara ndiyo kusema kwamba utavuna mbao kuanzia ukiwa na umri wa miaka 45 hadi ukiwa na umri wa miaka 70 hivi. Na kama utakuwa na umri wa miaka 45 wakati unapanda miti ikakomaa ukiwa na miaka 60 hivi utaweza kuvuna mbao kwa miaka 30 au zaidi hadi utimizapo miaka 90.

Hata ikitokea ukaondoka duniania ukiwa na umri wa miaka 65 watoto wako wataendelea kuvuna mbao kwa kipindi cha zaidi ya miaka 25. Huu ni mfano tu wa mradi endelevu unaoweka mfumo endelevu wa kupata pesa kwa kipindi kirefu hata kama haupo duniani au hata kama haupo kazini.

Kama ungependa kujua aina za miradi unayoweza kufanya hadi kutajirika sana nakushauri ununue kitabu changu kiitwacho, “Mbinu za Kuapata Pesa Nyingi Hadi Kuwa Bilionea”. Ndani ya kitabu hicho nimetaja miradi zaidi ya 66 ambayo unaweza kuifanya na ukapata pesa nyingi sana hadi kuwa bilionea.

Miradi endelevu utaikuta humo kitabuni na utachagua ni mradi gani unaofaa kuufanya ili uweze kukuletea fedha wewe mwenyewe kama mzazi na mpaka wajukuu wako. Kuna miradi endelevu kama vile: mradi wa upandaji miti ya mbao, mradi wa miti ya matunda, mradi wa nyumba za kupangisha kibiashara, hoteli, mradi wa nyumba za wageni (Guest houses), Mradi wa shule au vyuo vya elimu, mradi wa kampuni za biashara au huduma, nk. Miradi kama hiyo unaweza kuisoma vyema ndani ya kitabu changu hicho nilichokudokezea awali. Kama mzazi inakupasa kusoma siyo kitabu kimoja tu kwani kitabu kimoja pekee hakiwezi kumaliza kiu ya kuelewa mambo mengi.

Mbinu ya -18-

Waepushe Kuwa na Maisha ya Kiburi Cha Pesa

Mtoto wangu mwanangu epuka Kiburi cha mali. Mwanangu utakapokuwa mkubwa na ukawa milionea epuka kiburi cha fedha, epuka kiburi cha uzima au afya. Ukiwa mkubwa na ukawa na fedha na elimu hakikisha unaepuka Kiburi cha elimu. Epuka Kiburi cha uzuri wa sura. Epuka Kiburi cha pesa na jeuri ya pesa utakapokuwa tajiri.

Mtoto akiwa na malezi kama hayo ataelekea kwenye utajiri endelevu. Mzazi ukumbuke kuwa kama mtoto atakuwa na vitu hivyo viovu hataweza kupata utajiri endelevu. Wewe mzazi ndiye pekee unayeweza kuwaepusha navyo. Kiburi cha pesa huwaangamiza watu wengi sana kifedha na kiafya. Kama watoto wako watakuwa matajiri katika maisha yao na wakawa watu wasio na kiburi cha pesa wala kiburi cha mali au kiburi cha uzuri wa sura hakika wataweza kujiweka kwenye nafasi nzuri ya kumiliki utajiri wao bila kufilisika.

Watoto wanaolelewa kwenye maadili ya kutokuwa na kiburi watakuwa watumishi wema kwenye jamii na wataweza kujiweka kwenye nafasi ya kumiliki utajiri bila kulalamikiwa na jamii inayowazunguka. Dalili ya kwamba watoto wako umewalea katika maadili yasiyokuwa na kiburi cha utajiri au kiburi cha mali ni hizi zifuatazo;

- Wanashiriki kwenye ibada makanisani au misikitini na kushiriki shughuli za imani.
- Wanaweza kushiriki kwenye sherehe za watu wenye utajiri na hata wasiokuwa na utajiri.
- Wanashiriki kwenye misiba mitaani bila kubagua misi ba ya watu matajiri au maskini katika jamii.

- Wanaweza kukaa na watu wa aina zote yaani matajiri au maskini bila kinyaa wala kiburi.
- Hawana jeuri waka hawatoi kauli za kejeli kwa watu maskini au kwa mtu yeyote kwa misingi ya hali zao za kipato.
- Wanaweza kusafiri kwa kutumia usafiri wa aina zote iwe usafiri wa kifahari au wa kawaida wao wanaweza kuutumia bila shida.
- Wanaweza kusaidia mtu yeyote kimawazo au kifedha bila dharau wala kiburi kila wanapoombwa kufanya hivyo ilimradi wana uwezo huo.
- Hawajioni kuwa wameshakamilika na kujiona kuwa hawa hitaji msaada wa mtu kwani wanajua kwamba hakuna mtu awezaye kufanikiwa bila kuwa na watu ny uma yake.

Mbinu ya -19-

Wafundishe Kuwa Waaminifu Katika Fedha

Kingine kinachosababisha ufukara sana Afrika na Tanzania yetu ni ukosefu wa watu waaminifu au waadilifu. Uaminifu ni swala ambalo limekuwa adimu sana kwa watu wengi. Uaminifu umekuwa ukikosekana katika biashara au maofisi mengi yawe ya serikali au ya binafsi. Mtu anapoanzisha biashara au kampuni yake anapata wakati mgumu sana kupata watu waaminifu wa kuajiri kwenye kampuni yake au biashara yake kwa sababu ya kukosa watu ambao ni waaminifu.

Kuwapata watu waaminifu kwenye pesa ni jambo adimu sana. Kuwapata watu wanaoweza kukufanyia kazi kwa uaminifu ni swala zito sana kwenye jamii ya sasa. Unampatia kazi mtu kisha anakuibia. Unampatia nafasi mtu fulani kwenye kampuni yako ashike nafasi ya kutunza fedha kisha anakuibia fedha. Hayo yote ni kukosa uaminifu. Mzazi nakushauri uwalee watoto katika hali ya uaminifu kwenye maswala yote ya mali na fedha. Wafundishe kuwa uaminifu kwenye fedha ni jambo ambalo litawapatia thawabu kubwa sana maishani mwao. Uaminifu kwenye nafasi yoyote ya uongozi na kuwa na utamaduni wa kuridhika na malipo au mishahara wanayoipata ni jambo la maana sana.

Kusema ukweli kila mzazi kuwarithisha watoto utamaduni wa umanifu ili waweze kuaminiwa kushika nafasi kubwa sana kwenye mashirika ya umma au Makampuni mbalimbali ya biashara ni jambo ambalo kila mzazi akilifanya litawasaidia sana watoto.Umainifu kwenye maswala yote ya fedha, mali na matendo ya kila siku iwe kwenye uongozi au kauli na ahadi ni tunu za pekee ambazo watoto wakiwa nazo wataaminiwa sana na kila mtu au jamii kwa kila kazi na kwa kila wadhifa atakaopewa. Utamaduni wa kupora mali za watu au jamii kwa sababu tu zinaonekana kama hazina mwenyewe ni utamaduni

mwovu ambao haupaswi kukubaliwa kabisa wala kuendelezwa katika jamii. Kama mtu anaajiriwa kuwa Daktari ni vyema akawa mwaminifu sana kwa nafasi hiyo. Mtoto aliyelelewa kuwa mwaminfu hataiba dawa za hospitali na kuzipeleka kwenye hospitali yake binafsi. Mwalimu wa sekondari au shule ya msingi mwenye uaminifu hataweza kushirikiana na watoto kuiba mitihani ya shule au kuiba mali za shule. Mfanyabiashara mwenye utamaduni wa uaminifu hataweza kuuza bidhaa bandia dukani mwake. Mtoto mwaminifu hataweza kuuza bidhaa dukani mwake zilizopitawa na wakati (expired). Uaminifu ni utamaduni unaopaswa kujengwa kwa watoto tangu wakiwa wadogo.

Njia pekee ya kuwakuza watoto katika utamaduni huo wa uaminifu ni kwa wazazi wenyewe kuwa waaminifu kwanza kwenye kila Nyanja ya maisha yao. Hata hivyo, kama mzazi unajijua kwamba wewe siyo mwaminifu kwa namna yoyote iwe kwenye fedha, mahusiano, kujali mali za kampuni au shirika au serikali na unajua kabisa kuwa huwa huridhiki kwa kile unacholipwa, jitahidi sana kutowarithisha watoto wako utamaduni huo. Fanya kila unaloweza kuwajengea utamaduni watoto wako ili wao waweze kupata maisha yenye heri duniani.

Mzazi kama unasimamia kitengo serikalini, kwenye kampuni ya mtu binafsi, kwenye taasisi binafsi au popote pale, hakikisha kwamba haujengi utamaduni wa kukosa uaminifu kwenye mali za watu wengine. Epuka ufisadi wa namna yoyote ile kazini kwako. Epuka kuwatapeli watu wanyonge hata wasiokuwa wanyonge. Epuka kumwibia mali au pesa mwajiri wako.

Epuka kujilimbikizia mali za wizi. Fanya kazi kwa uaminifu mbele ya jamii na watoto wako hakika utapata thawabu kubwa ya kuishi maisha marefu hapa duniani. Mzazi ukifanya kazi kwa uaminifu kwenye kazi za watu wengine waliokuajiri ni dhahiri kwamba utapata utajiri mkubwa sana utakaokusaidia kufanya mambo makubwa zaidi kwako na kwa watoto wako.

Mbinu ya -20-

Wazoeze Watoto Kuweka Akiba Ya Fedha

Hakuna mtu anayeweza kumudu kumiliki utajiri mkubwa kama haweki akiba ya pesa. Akiba ya pesa ndiyo pekee inayoweza kumfanya mtu kuweza kufikia lengo lake la kibiashara na kifedha kwa siku za usoni. Bila Kuweka akiba ni vigumu kupiga hatua kubwa kifedha na kiuchumi. Mtoto akifundishwa Kuweka akiba akiwa bado mdogo ataweza kuendeleza utamaduni huo hadi akiwa mkubwa.

Kama unatamani watoto wako wawe matajiri siku za usoni, hakikisha kuwa unawapa mazoezi ya Kuweka akiba. Mazoezi hayo waweza kuyafanya kwa vitendo kwa kuwapatia watoto wako kiasi chochote cha pesa na kuwaambia watunze pesa hiyo hadi utakapowaomba pesa hiyo. Mtoto anayeweza kuhimili kuvumilia Kutonunua chipsi au soda wakati ana pesa imetunzwa

mahali fulani nyumbani au benki huyo atakuwa ameshinda nguvu ya ushawishi wa matumizi yasiyo ya lazima au matumizi mabaya ya fedha. Mtoto anapaswa kujifunza kuvumilia kutotumia pesa kwa vitu ambavyo hakupangilia au havimo kwenye malengo yake ya muda mrefu au mfupi. Mtoto azoezwe Kununua kile kitu alichokusudia tu hata kama atakutana na mambo mengi matamu na mazuri kwa mvuto mbele yake.

Mzazi ukimfungulia akaunti maalumu katika benki yoyote mtoto siyo jambo baya. Hakikisha kuwa unafungua akaunti kwa ajili ya shule yake, kwa ajili ya kuanzisha biashara yake au kampuni yake. Hakikisha kuwa unaweka akiba kwa ajili ya kumjengea nyumba yake ya baadaye hata kama ni mtoto wa kike. Usiweke akiba bila malengo. Usiweke akiba kwa kufuata mkumbo wa watu wengine.

Weka lengo lako na ndilo likusukume kuwa unaweka akiba kila mara. Kama unaweka akiba kwenye mifuko ya hifadhi ya jamii kama vile **LAPF, NSSF, PSPF, PPF au GEPF** ni vyema ukajiridhisha kwamba akiba yako itakuwa salama kwenye mifuko hiyo. Tafuta ofisi za mifuko hiyo ili wakupe utaratibu wa kisheria wa kujiunga nayo ili uweze kuitumia Kuweka akiba yako ya sasa na baadaye. Unaweza Kuweka akiba kwenye mifuko hiyo kwa ajili ya maisha yako ya uzeeni au kwa ajili ya malengo yako mengine ya kiuwekezaji na maendeleo. Usijiunge na mifuko hiyo ya hifadhi ya jamii bila kujua lengo lako ni lipi.

Weka lengo kuu kama ni akiba ya uzeeni au kama ni mradi fulani unaoutaka uufanye baadaye, nk ndicho kikusukume kila siku Kuweka akiba. Kama huna msukumo wa kwa nini unaweka akiba kwenye mifuko ya pensheni au kwenye mabenki hakika hautaweka akiba kwa kipindi kirefu. Mpaka uwe na msukumo wa baadaye ndipo unapoweza Kuweka akiba kila siku.

Watu wengi hushindwa Kuweka akiba kila siku iwe kwenye M-pesa, Tigo-pesa, Airtelmoney, Easypesa, benki, mifuko ya pensheni, nk huwezi kufanikiwa Kuweka akiba kama huna msukumo wa kwa nini unaweka akiba. Watoto wetu wafundishwe kwa nini ni lazima au muhimu Kuweka akiba yao. Je, ni kwa ajili ya ada za shule, je ni kwa ajili ya nguo za siku kuu, je ni kwa ajili ya ujenzi wa nyumba, je ni kwa ajili ya matibabu, je ni kwa ajili ya dharura za uzazi, je, ni kwa ajili ya safari ya kwenda ng'ambo ya nchi, je ni kwa ajili ya gharama za harusi, je ni kwa ajili ya Kununua gari zuri, je unaweka akiba kwa ajili ya nini? Hakikisha kuwa una jambo linalokusukuma Kuweka akiba. Kama huna jambo linalokusukuma Kuweka akiba hautaweza Kuweka akiba kabisa. Watoto wako wakijua kwa nini wanaweka akiba hakika watakuwa na msukumo wa Kuweka akiba. Waeleze watoto wako kwa nini wewe mwenyewe unaweka akiba na kwa nini wao pia wawe na utamaduni wa Kuweka akiba. Watoto wajue kwa uwazi na kwa hoja inayoeleweka maana ya Kuweka akiba ya baadaye. Hapo ndipo wataweka akiba.



Ukitazama kibonzo hicho hapo juu, lazima ufikiri tofauti.

Mbinu ya -21-

Waepushe Watoto Wako na Ulevi wa Pombe

Ulevi wa pombe ni adui wa maendeleo Afrika. Sehemu kubwa Afrika inashindwa kupiga hatua za maendeleo kiuchumi, kiteknolojia na kifedha kwa sababu watu wake sehemu kubwa hawajajitambua kiasi cha kutoweza kujitawala kifikra. Huwezi kuleta au kurithisha maendeleo kwa watoto wako na familia yako kama wewe ni mlevi wa chochote kama vile sigara au pombe na ngono. Watoto wako wasipoepushwa na utamaduni wa kunywa pombe na uvutaji wa sigara hawataweza kuvuka vikwazo na changamoto za kufiliska. Hawawezi kukwepa kufiliska kama wataanza kuwa wanywaji wa pombe wakingali wadogo. Kama wazazi wenyewe ni walevi wa kupindukia huenda ikawaathiri watoto pia kuwa walevi kama wazazi wao.

Mzazi hakikisha kwamba huwapeleki watoto kwenye maeneo ya vilabu vya usiku. Epuka kuwapeleka kwenye maeneo ya pombe kwa nia ya kwenda kuwapa vinywaji vikali. Mzazi epuka kuwa mlevi wa kupindukia mbele ya watoto wako. Ukiendelea kuwa mlevi wa pombe itakuwa vigumu sana kwa watoto wako kukwepa kuwa wanywaji wa pombe.

Kuna wazazi wenye tabia mbaya na hawawezi kujizuia mbele ya watoto. Hata kama wewe una tabia ya kunywa pombe na unadhani huwezi tena kuacha kunywa pombe kali na huwezi kujizuia kunywa hadi ukalewa, hakikisha basi haulewi pombe na kuwaonesha watoto kwamba umelewa pombe. Hakikisha haunywi pombe kwa viwango vya kuwaudhi watoto kama umeshindwa kuacha kabisa pombe. Kama inawezekana tafuta msaada kwa watu wa makanisa wanaoombea watu wenye matatizo uweze kuombewa kwa tatizo hilo la ulevi, nina imani kabisa ukiombewa kwa imani kwamba Mwenyezi Mungu

anaweza yote, tatizo lako la ulevi litakwisha kabisa. Kama umeshindwa kuacha ngono, tumbaku au sigara pia fanya hivyo hivyo. Ukiombewa kwa imani kwamba Mungu yupo na anasaidia wenye matatizo kama hayo, hakika utashangaa jinsi Mwenyezi Mungu atakavyokusaidia. Utaacha pombe milele. Utaacha sigara milele na hautarudia tena kwa sababu utapata nguvu na uweza wa kukutoa kwenye ulevi na sigara.

kwa hiyo, mzazi mwenye upendo kwa watoto wake hataruhusu watoto wake warithi tabia mbaya alizozipata kwa bahati mbaya kutoka kwa wazazi wake au kutoka kwa ukoo wake. Kama wewe ulijifunza kunywa pombe kutoka kwa marafiki zako au kwa wazazi wako usitake na watoto wako warithi tabia hiyo. Kama wewe unafanya ufisadi wako na uovu mwingine hakikisha kuwa watoto wako hawarithi uovu wako. Kwepa kabisa kurithisha tabia mbaya yoyote uliyonayo kwa watoto wako. Warithishe watoto wako kila lililo jema peke yake.

Mzazi mwenye busara huwarithisha wana wa wana wake mambo mema, ndivyo maandiko matakatifu yasemavyo. Kama maandiko yanasema hivyo, wewe ni nani unayejisikia raha kuwalazimisha watoto wako kunywa pombe? Kwa nini unajisikia raha watoto wako wakiwa wamekusindikiza kunywa pombe? Hivi hujui kuwa ulevi na pombe ni adui wa maendeleo kwa kizazi chako.

Siyo kwamba nasema watu wasinywe, ninachosema ni kwamba watu wasiwe walevi mbele ya watoto ambao ni kizazi kinachochipuka na kukua. Usiwarithishe watoto utamaduni wa ulevi wa kunywa pombe kwa sababu hawajijatambua kwa kiasi kikubwa. Usinywe pombe hadi ukalewa mbele yao na kuwafanya watoto wako wajute kuwa na baba au mama kama wewe. Kama huwezi kujizuia kulewa basi acha kunywa kabisa. Na kama umeshindwa kuacha kujizuia kabisa, nenda

ukaombewe makanisani. Nenda ukamwone kiongozi wako wa kidini au kiongozi wa kiroho aliyeko karibu yako ukamsihi akuombee dua kali ambayo itakuwezesha uache kunywa pombe au uache kunywa zaidi ya uwezo wa ubongo wako kuhimili ulevi. Epuka kuwa sababu ya watoto kuja kuwa walevi wakubwa wasiojitambua kifikra.

Epuka kuwafanya watoto wako kuwa watumwa wa pombe na sigara. Jiepushe na hatari ya kuwaambukiza watoto wako utamaduni wa kunywa pombe kama vile wanakunywa maji. Kuna watu wanakunywa pombe utadhani wanakunywa maji ya Uhai au Kilimanjaro au maji ya Dasani. Kuna wazazi wanakunywa pombe na kisha wanarejea majumbani mwao na kufanya fujo kwa watoto. Kuna wazazi wa kike na wa kiume kwao kunywa pombe au bia ni kama kunywa chai ya asubuhi. Wazazi hao wakinywa bia au pombe wanakuwa wakorofi sana kwa watoto au kwa mama watoto au baba watoto na wanafikia hatua ya kutowasaidia watoto tena. Hadi hapo watoto wanajiona wanyonge mbele ya mama au baba mlevi. Wanakosa uelekeo wa maisha yao.

Mbinu ya -22-

Waepushe Watoto Wako Kuwa Makahaba

Kama kuna jambo wazazi tunapaswa kukwepa maishani mwetu ni kuwafanya watoto wetu kuwa makahaba mara tu wawapo wakubwa yaani kuanzia watimizapo umri wa miaka 15 na kuendelea. Kama una mtoto wa kike au wa kiume aliyekwishavuka umri wa miaka 15 yaani yuko kwenye umri wa miaka 17 hadi 25 lakini hajaanza kujihusisha kwenye vitendo vya ngono, hakika huyo amelelewa vyema alipokuwa na umri wa miaka 0 hadi 15. Mzazi kama una tabia mbaya ya uzinzi na ukahaba na umeshindwa kuuacha hebu jizuie kuionesha kwa watoto wako. Fanya uhuni wako mbali na watoto.

Kama madaktari wanavyosema tuweke dawa mbali na watoto dawa zote, nami nasema hivi, tabia zako za uzinzi na ukahaba ziweke mbali sana ambapo hata watoto wako hawawezi kuziona au kuzinusa kabisa.

Kama nilivyoeleza awali, ubongo wa mtoto huandika vitu avionavyo, avisikiavyo, avigusavyo, avinusavyo, na avihisivyo. Hakikisha kuwa ni marufuku watoto wako kukuona ukitoka na mwanaume ambaye siyo baba yao. Hakikisha kuwa hukai wala kulala na mwanamke ambaye siyo wa ndoa yako mbele ya watoto wako. Fanya ufanyavyo, lakini watoto wako wasinuse harufu yoyote ya uzinzi wako wala ukahaba wako. Epuka kufanya matendo ambayo watoto wako watajua kuwa unatembea na watu wasiokuwa mume au mke wako. Wakigundua tu watapoteza imani kwako. Hakikisha kuwa watoto wako hawawezi kurithi tabia yako ya ukosefu wa uaminifu kwa mwenzi wako wa ndoa. Ukifanya hivyo, utakuwa umewaepusha watoto wako kuwa makahaba na wazinzi. Kwa nini napendekeza kwa wazazi kuepuka kuwafanya watoto wao kuwa makahaba na wazinzi? Ni

kwa sabau uzinzi na ukahaba ni adui wa maendeleo kama ilivyo ulevi wa pombe. Utamaduni wa ukahaba na uzinzi hautawasaidia watoto kuwa wenye busara na hekima za kutawala fedha. Ni kweli kwamba maswala ya ngono hutokana na msukumo wa kibailojia ndani ya mwanadamu. Lakini, msukumo huo bado waweza kudhibitiwa na mila na desturi za watu, dini na au malezi na maonyo mtoto aliyopewa alipokuwa mdogo.

Huwa ni vigumu sana na ni mara chache sana mtoto awapo mkubwa kuwa kahaba kama hajapata msukumo kutoka kwa watu wengine wa rika lake au kama hakuna aliowaona wakifanya hivyo kwenye ukoo wake au kwenye familia yake. Ni hatari kwa watoto wetu kuwa makahaba. Tufanye wajibu wetu tuwaepushe na janga hilo la kimaadili.

Haiwezekani watoto wetu wakawa matajiri wakubwa kama watajitumbukiza kwenye tamaa za ngono na ukahaba na uhuni katika ujana wao. Haitakuwa na raha yoyote kwa mzazi awapo bado hai kuwaona au kuwasikia watoto wake kuwa ni makahaba na wahuni, wazinzi waliokubuhu au machangudoa mitaani. Mzazi huwezi kujisikia amani na raha duniani kama watoto uliowazaa ni makahaba na majambazi wahuni waliokubuhu. Utatamani ufe haraka ili kukwepa kuyaona maovu ya watoto wako.

Lakini, hebu fikiria kama wanao wote ni mabilionea, wenye utajiri mkubwa popote watakapokuwepo duniani na wewe ukawa ungali hai na ukashuhudia maisha yao bila kujali jinsi yao iwe ni watoto wako wa kike au wa kiume? Ni fahari iliyoje kwa watoto wako kuwa mabilionea badala ya kuwa na sifa ya makahaba mitaani? Ni fahari iliyoje kwa watoto wako kuwa matajiri wakubwa kutokana na malezi bora ya kibilionea uliyowajengea tangu utotoni mwao? Ni fahari iliyoje hata kama wewe hukufanikiwa kuishi kibilionea lakini watoto wako ukawaona wanaishi kibilionea? Hebu waepushe watoto wako na hatari ya wao kuwa wazinzi, makahaba na wahuni.

Mbinu ya -23-

Waepushe Watoto Kuwa Majambazi

Katika kukupatia mbinu za kuwawezesha watoto wako waje kuishi kimilionea hadi kibilionea ni lazima kujifunza mbinu zote ambazo zaweza kuwa kikwazo kwao. Ni hasara iliyoje kuzaa watoto badala ya kuwa matajiri, mamilionea na mabilionea wakawa majambazi wanaovamia watu na kuwapora mali zao!!! Hivi mzazi uliyezaa watoto wawili, watatu au watano au zaidi kisha ukawasikia huku au kule kuwa ni majambazi wanaovamia na kupora mali za watu utajisikiaje? Nina uhakika utatamani dunia ipasuke ufunikwe nayo ili kuepuka aibu hiyo?

Kama unataka watoto wako waepuke kuwa majambazi na wawe na maisha ya kifahari na kibilionea ni lazima uwaandae kuwa mawakili wa mali za dunia hii kwa faida ya kizazi chao, jamii na taifa. Ili watoto wako wasije kuwa majambazi hakikisha kuwa unawelea katika maadili ya dini yako tangu wakiwa wadogo. Wazoeze kupenda ibada za kwenye imani yako.

Waeleze umuhimu wa imani na uchaji wa Mungu katika maisha yao. Waambie faida watakazopata kwa wao kuwa wacha Mungu. Je watapata faida gani kiafya, kijamii, kiroho na kifedha wakiishi maisha ya uchaji Mungu wa imani yako. Waambie kuwa wakimcha Mungu wa imani yako watakuwa na afya bora kwani watakuwa na uwezo wa kujilinda dhidi ya maradhi yatokanayo na kula au kunywa bila kuwa na kiasi. Mtu anayemcha Mungu ni lazima aishi maisha yenye kiasi katika kila jambo.

Watoto wakimcha Mungu tangu wakiwa wadogo sana hakika hawataiacha njia ya Bwana au njia ya dini yao hata watakapokuwa wakubwa. Kifedha pia watazweza kuwa na fedha nyingi sana kwa sababu fedha na dhahabu vyote ni mali ya Mwenyezi

Mungu. Nao kwa kumcha Mungu ni wazi kuwa Mungu huyo huyo mwenye mali zote atawawezesha kupata mali za kumiliki katika uhai wao duniani. Ni raha na furaha iliyoje duniani kuwa mtoto mcha Mungu unayemiliki mali na utajiri kwa faida yako na jamii kubwa inayokuzunguka!!!

Hakikisha kuwa wewe kama mzazi unawarithisha watoto wako mila na desturi ambazo ni za uchaji Mungu. Siyo lazima wawe wenye imani kali sana kiasi cha kuweza kuifia imani hiyo. Ninachosema hapa ni kuhakikisha kuwa ile misingi ya imani yako iwe uislamu au ukristo watoto wako wailelewe wangali wadogo mpaka watakapokuwa wakubwa maishani mwao.
Kama watoto wataamua kuwa na imani kali au kuifia imani hilo liwe chaguo lao lakini lisiwe msingi wa kuachiwa kutoka kwa wazazi. Ukiwa mzazi wewe mweleze uzuri wa imani yako, mweleze mtoto wako ni kwa nini unamruhusu kuabudu Mungu huyo unayemwamini wewe.

Mwambie mtoto wako apende ibada, apende kusoma na kufuatilia maandiko matakatifu ya imani yako, apende kujali watu wote bila kubagua rika za watu au hali za kiuchumi za watu, mfundishe awe na utu na ubinadamu katika maisha yake hasa kwa watu wengine hata kama siyo wa kabila lake au taifa lake. Mtoto afundishwe kuepuke ufisadi, kuepuke ulaghai na unyang'anyi wa mali za watu wanyonge. Aepuke dhuluma na wizi wa mali za umma. Hakika kama utamlea mtoto katika uchaji Mungu nina hakika utamwepusha kuwa jambazi. Utamwepusha kuwa na dhuluma. Utamwepusha kuwa mwizi wa mali za umma. Utamwepusha kuwa fisadi asiyehurumia wanyonge. Utamwepusha na uwezekano wa kutojali watu wa hali za chini. Hakika utamfanya kuwa bilionea au milionea mcha Mungu.

Mbinu ya -24-

Wafundishe Watoto Kuyapenda Mazingira

Jambo lingine linalosababisha bara la Afrika lisipige hatua kubwa za kiuchumi na kifedha ni uharibifu wa mazingira. Kila mahali ni uharibifu wa mazingira. Watu wanakata miti na hawana hata mpango wala mipango ya kupanda miti zaidi. Watu wanajisaidia vichakani haja kubwa na ndogo bila kujali madhara yake kwa viumbe wengine kama vile wanyama na ndege. Barani Afrika ndipo utakuta watu bado wanakumbwa na magonjwa yatokanayo na uchafuzi wa mazingira kama vile kipindupindu, maralia, minyoo, maambikizi ya njia za mkojo (U.T.I), kuvu au fangasi, magonjwa ya ngozi, umba na vibarango, nk. Ni uchafu kila mahali.

Afrika ndipo kila aina ya magonjwa ambayo yangeweza kuepukwa na kutowapata watu kama mazingira ya makazi yangekuwa safi na endelevu. Afrika ndipo vimbunga vya kawaida tu vikitokea vinasambaratisha majengo mengi sana kutokana na kwamba majengo hayo hayakujengwa katika mazingira bora yenye uoto wa asilia au wa kutengenezwa kwa kupanda miti.

Haitakuwa rahisi sana watoto wetu kuwa mabilionea kama hawatakuwa rafiki wa mazingira yao. Mzazi ninakushauri uhakikishe kuwa unawawezesha watoto wako kuwa wapenda mazingira kwa namna ambayo itawawezesha kuwa mabilionea na wenye afya njema kwa kutunza mazingira yao.

Kama mtoto atakuwa mwenye kuyapenda mazingira hakika atakuwa na uwezo wa kuyatumia mazingira kwa maendeleo yake na kizazi chake hadi cha nne au zaidi. Huwezi kutegemea kuwa mazingira yatakulinda wakati wewe mwenyewe huyalindi. Huwezi kutarajia kuwa mazingira yatakuletea hali ya hewa

nzuri na kuleta mvua nzuri kama wewe mwenyewe huyatunzi na kuwaambukiza watoto wako utamaduni huo wa kutunza mazingira. Kutunza mazingira ni kutunza afya zetu. Afya zetu ndio utajiri wetu. Kutunza mazingira ndiko kutunza utajiri wetu. Huwezi kuendelea hadi kuwa bilionea kama hutunzi mazingira kwa kupanda miti, kwa kuotesha na kutengeneza bustani za kupumzikia, kwa kuwa na nyumba bora inayozingatia usafi wa mazingira na uhai wa viumbe wengine.

Kwa hiyo, ni vyema mzazi ukawa mstari wa mbele kuhakikisha kuwa watoto wako wanajifunza kwako au kwa wengine swala la kutunza mazingira yao ya makazi au hata ya mashambani ili kuhakikisha kuwa mashamba yanakuwa ni endelevu na yenye kuleta matunda mazuri kwa sasa na kwa kizazi cha baadaye.

Waambie watoto umuhimu wa kupanda miti mingi kwa hali na mali. Wakumbushe kila mara watoto wako kuwa usafi wa mazingira huwezesha familia kuepuka magonjwa ya mlipuko, familia huepuka magonjwa ya minyoo matumboni mwao, familia inayotunza mazingira hutajirika sana kutokana na mali inayopatikana kwenye mali zilizomo kwenye ardhi na mazingira yake. Utunzaji wa mazingira yetu husaidia kupunguza muda mwingi kupambana na maradhi yaambatanayo na kutokutunza mazingira.

Kama unapenda watoto wako wawe watunzaji wa mazingira yao kwa faida yao kifedha na kiuchumi hakikisha kuwa wewe mwenyewe mzazi unajitahidi kutunza hata mazingira ya nyumba yako. Hakikisha kwamba unafyeka majani yanayozunguka nyumba yako. Hakikisha kuwa unapanda hata miti michache kwenye ploti yako hiyo hiyo uliyonayo hata kama ni mjini sana. Unaponunua ploti yoyote kwaajili ya matumizi yako ya baadaye kitu cha kwanza kiwe kupanda miti ya kivuli na miti ya matunda. Panda miti kadri uwezavyo ili kuleta mandhari nzuri na ya

kuvutia kwenye nyumba zako. Inasikitisha kuona watu badala ya kupanda miti wao wanakimbilia kukata miti hata iliyokuwepo kwenye ploti zao na kisha hawapandi tena miti. Watu wanasahau kwamba miti ndiyo iletayo uhai kwa mwanadamu kwa kumletea hewa ya oksijeni ambayo ndiyo uhai wenyewe wa mwanadamu.

Haipendezi kuishi kwenye mazingira ambayo hayana hata mti mmoja. Hebu kuanzia leo unaposoma kitabu hiki amua sasa kwenda Kununua miche ya miti hata ya matunda au nenda porini ukatafute mbegu za miti kama vile mapera, maembe, nk upande hapo nyumbani kwako.

Ni aibu kubwa sana kuishi kwenye nyumba ambayo haijazungukwa hata na mti mmoja. Ni dhambi kubwa sana mbele za Mungu kukata miti bila kupanda miti mingine. Ni dhambi kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu kukata miti kwa ajili ya Kilimo halafu ukaacha kupanda miti mingine. Hebu jiulize kupanda mti hata mmoja hapo unapoishi karibu na nyumba yako inakugharimu pesa nyingi kiasi gani?

Kama unataka watoto wako na watoto wao hadi watoto wa watoto wao waje kuishi maisha ya kifahari na kibilionea hakikisha unatunza mazingira ya kuishi. Haitaingia akilini mwao kukuta maisha ni magumu na wako kwenye ardhi kame na kavu na isiyokuwa na hewa ya kutosha halafu ukategemea waendelee na maisha ya kifahari kwenye mazingira mabaya na makavu. Tunza vyanzo vya maji kwa kutovichafua.

Wafundishe na watoto wako umuhimu wa kuyapenda na kuyatunza mazingira kwa faida yao na faida ya watoto wao. Jisikie raha kamili kuwarithisha watoto wako mazingira tulivu na yenye raha kuishi. Haifai kuwarithisha elimu, mali na majumba huku kukiwa hakuna matumaini kwenye mazingira.

Wafundishe watoto kuwa wasafi nyumbani na nje ya nyumbani. Nunua chombo cha kutunzia takataka nyumbani kwako. Jikoni uweke chombo cha kuwekea uchafu. Sebuleni pia kiwepo chombo cha kutupia uchafu mdogo wa karatasi, mabaki ya chakula, nk. Nje ya nyumba yako uwe na pipa dogo la kutunzia uchafu wote wa Vyakula na makaratasi au mifuko ya Rambo na kuhakikisha kuwa uchafu unatupwa panapostahili kila mara. Wafundishe watoto kwa vitendo. Waambie watoto umuhimu wa usafi wa nyumba na vyumba vyao. Vitanda viwe safi na vitandikwe mashuka safi kila mara. Kwa kufanya hivyo, watoto wako wataendelea kuwa wasafi nje na ndani mpaka watakapokuwa wazee.

Watoto wako wakataze kujisaidia ovyo ovyo wawapo nje ya nyumbani. Wafundishe kutokojoa ovyo mahali popote. Wawapo safarini wasiwe wa roho wa kula na kunywa kila kitu kipitacho mbele yao kama vile karanga, mahindi, ndizi, nk. Ni aibu sana kwa mtu akiwa safarini yeye ananunua kila kinachopita mbele yake na kuchafua mazingira. Akiona mahindi ya kupikwa ananunua. Akiona karanga ananunua. Akiona ndizi, korosho, pipi, maandazi, nk anataka kika kitu akile.

Tabia ya kula ovyo ovyo kama hiyo siyo nzuri kwa watoto wetu. Haipendezi mtoto anayetarajiwa kuwa milionea akawa mwenye tabia kama hizo zinazochangia uchafuzi wa mazingira. Nunua chakula mahali penye uhakika wa usafi wa mazingira. Nunua chakula kwa nyakati maalumu tu. Kama unasafiri kwa mabasi hakikisha kuwa haunyi maji mengi sana kiasi kwamba utataka kujisaidia kila mara njiani. Acha tabia hiyo. Kujisaidia haja ndogo au kubwa uwapo njiani tena mahali ambapo hapajaidhinishwa kutumika kwa kujisaidia ni utamaduni wa kimasikini na kijinga. Epuka kujisaidia porini.

Epuka kuchafua mazingira kwa kutupa taka ovyo uwapo safarini. Uwapo ndani ya basi au gari lolote epuka kutupa uchafu barabarani. Epuka kurusha kitu chochote ambacho kitachafua mazingira ya miji yetu. Hakikisha kuwa miji yetu tunayoishi ni misafi kuanzia mahali unapoishi. Watoto wako wakue kila mara wakiona utamaduni wa usafi kuanzia majumbani, mashuleni na vyuoni. Wakiona usafi wa vyoo vya majumbani, vyoo vya mashuleni, vyoo vya vyuoni na maofisini hakika na wao watajenga utamaduni huo huo. Watayatunza mazingira ya majumbani, mijini na mashuleni na hakika nchi yetu itakuwa na miji iliyo misafi sana.

Kwa hiyo nakusihi sana kama una watoto uwafundishe kuwa wasafi sana. Wafundishe wayatunze mazingira kwa kupanda bustani nzuri za maua. Wafundishe kupanda miti ya mbao, wafundishe kupanda miti ya matunda, wahimize watoto wako kupanda kwa wingi miti ya mapambo. Waelekeze kupanda miti kila mahali wanapokaa pawe safi na pa kuvutia macho yao na ya wengine. Wafundishe watoto kutotupa uchafu au takataka ovyo. Wafundishe watoto wako kuwa wasafi siyo tu majumbani mwao bali hata kwenye maeneo ya umma (public areas). Huu utamaduni wakiurithi hakika wataweza kuwa matajiri siyo tu wa afya bora na njema bali pia wenye kumiliki mali zitokanazo na mazingira yenyewe.

Mbinu ya -25-

Wafundishe Watoto Kuwa Wazalendo

Uzalendo ni utamaduni wa kupenda nchi yako au nyumbani kwako yaani kuwa na uwezo au utashi wa dhati usioyumbishwa na lolote wa kutetea watu wa nyumbani kwako au nchi yako hata kwa gharama za kifo.

Ni utamaduni wa kupenda kilicho chako hata kama siyo kizuri sana ukikilinganisha na cha mwenzako. Kwa mfano, hata kama nyumbani kwenu hakuna nyumba nzuri sana ukilinganisha na nyumba ya jirani yako, huwezi kwenda kulala au kula chakula kwa jirani huyo kwa sababu tu wewe hauna nyumba nzuri au chakula kizuri kama cha jirani yako.

Kwa hiyo, utamaduni ni tabia za kila siku za watu katika jamii. Uzalendo unajengwa kutoka kwa kizazi kimoja kwenda kwenye kizazi kingine. Haiwezekani kamwe kupata uzalendo kwa kizazi cha leo kama kizazi kilichopita hakikujenga utamaduni wa uzalendo kwa watoto wao. Haiingii akilini kudhani kwamba utapata vijana wenye uzalendo kama wazazi wenyewe hawana uzalendo.

Kama unataka watoto wako wawe matajiri na waweze kujipatia utajiri endelevu hakikisha kuwa unawajengea utamaduni wa uzalendo. Wajengee utamaduni wa kupenda nchi yao ya Tanzania. Wajengee utamaduni wa kupenda bidhaa za Tanzania zinazozalishwa hapa hapa Tanzania. Wajengee utamaduni wa kupenda kuitumikia nchi kwa uzalendo wote. Waimarishe watoto wako kifikra na kimawazo waweze kuwa wazalendo kifikra na kifedha.

Watoto wetu wanatakiwa kuitumikia nchi yao kiuchumi, kisiasa, kijamii na kimazingira. Sisi wazazi ndio tunatakiwa tuwajenge watoto wetu waweze kuwa huru katika kufanya maamuzi sahihi na makini yahusuyo mstakabali wao wa baadaye.

Kutokuwa na kizazi chenye uzalendo kwa nchi yake ndiyo mwanzo wa kuwa na watu wanaodhani maandeleo na utajiri viko katika nchi za wengine kama vile Ulaya, Marekani, Uchina na Uarabuni. Badala ya kuwa na kizazi kinachofikiria jinsi ya kuinua taifa lao liwe kwenye viwango vya hali ya juu kiuchumi na kiteknolojia tunakuwa na kizazi kisichofanya lolote kuinua taifa liwe juu kiteknolojia wala kiuchumi. Tunakuwa na vijana wenye ndoto za kupaa kwenda majuu.

Tunakuwa na kizazi kinachowaza kuondoka nchini mwake na kwenda kuishi nchi nyingine za ng'ambo. Tunajikuta tuna kizazi ambacho hakina mizizi ndani ya nchi yao. Kila kijana anawaza kuondoka akaishi nchi nyingine. Huu ni ukosefu wa uzalendo kwa taifa. Huu ni ukosefu wa utamaduni wa uzalendo tulioukosa kutoka kwa wazazi wetu. Nasi kama wazaz wa sasa tujenge utamaduni wa kupenda nchi yetu na tuwarithishe watoto wetu kuipenda nchi yao na watoto wao pia wakute utamaduni huo ukiendelezwa kwa kizazi hadi kizazi.

Haiwezekani tukawa na vijana ambao akili na mawazo yao yote yamejaa Umarekani au Uafrikakusini, au wamejawa na mawazo ya Ulayaulaya halafu tukadhani kuwa tuna taifa la Tanzania. Hakika hatutakuwa na taifa kama wazazi hatutawaonesha watoto wetu kuwa taifa lao ndiyo hili na ni taifa lenye utajiri mkubwa ambao hawapaswi kuuacha na kukimbilia kuishi mataifa mengine kwenye utajiri wa kigeni. Kama tunataka watoto wetu wamiliki utajiri mkubwa wa maliasili zilizopo Tanzania ni lazima tuhakikishe kuwa watoto wetu tunawalea katika maadili na utamaduni wa kuwawezesha kumiliki na kutamalaki nchi.

Kwa nini watoto wako wasitajirikie Tanzania? Kwa nini uwaruhusu watoto wako waende kujenga mataifa mengine badala ya kujenga taifa lako ulilolikuta? Hakika wazazi wengi wamesababisha watoto wao kutokuwa wazalendo kwa taifa hili la Tanzania. Wazazi wengi wanajisikia fahari kuwa na watoto wanaoishi kwenye mataifa ya watu wengine.

Yaani unamkuta mzazi anajivunia kuwa na watoto waishio Marekani, Dubai, Korea, Uingereza, China, Kanada, Brazil, nk. Tangu taifa la Tanzania lizaliwe mwaka 1961; wazazi wengi walilirithi utamaduni wa ng'ambo au wa mataifa ya nje kwamba mambo mazuri yako kwenye nchi hizo. Utamaduni huo umeendelea kuliathiri taifa letu la Tanzania kiasi kwamba kila mtu anawaza ni lini ataondoka kwenye nchi hii aende kuishi mbali na Tanzania. Utakutana na vijana wako na pirikapirika (busy) wakihaha kutafuta upenyo wa kwenda nchi zilizoendelea. Wanatafuta kila njia halali na haramu ili tu waondoke Tanzania na waende nchi nyingine. Hali hii ni kukosa uzalendo kwa taifa letu.

Unaenda kutafuta kitu gani ambacho huwezi kukipata ukiwa Tanzania? Je unadhani maisha bora yako Ulaya na Marekani pekee? Hata hapa hapa Tanzania ukifanya kazi kwa kujituma unaweza kuwa bilionea. Mbona mabilionea wapo wengi tu Tanzania? Acha usaliti kwa taifa lako. Lipende taifa lako. Upende mkoa wako uliozaliwa. Endeleza mkoa wako na kijiji chako. Jenga nyumba nzuri kijijini kwenu ulipotoka. Wajengee wazazi wako nyumba nzuri hata kama ni kijijini. Tengeneza utajiri mkubwa hapa hapa Tanzania. Jenga familia yako na watoto wako kuwa wazalendo mabilionea wasioyumbishwa na lolote.

Mbinu ya -26-

Wazoeze Watoto wako Kuishi Peke Yao

Wazazi wengi wanashindwa kuelewa kwamba kuna kipindi hawatakuwepo tena duniani. Maandiko matakatifu yanasema, ".....mtu mwema huwarithisha mema wana wa wanawe..." Watoto wanatakiwa wajulishwe kwamba kuna kipindi wao ndio watashika madaraka ya kila kitu. Watoto wanatakiwa wajulishwe kwamba maisha ya wazazi yatakapofika mwisho wao ndio watapaswa kuendelea kushikilia madaraka kwenye miradi au Makampuni ya wazazi wao. Watoto wanapaswa kuzoea kufanya kazi kwenye kampuni za baba au mama hata kama baba au mama amesafiri kwenda mbali kwa kipindi kirefu na watoto waweze kusimamia kila kitu kwa ubora ule ule kama vile wazazi wapo.

Mzazi kama unataka watoto wako wawe mabilionea wazoeze kuishi peke yao siyo nyumbani tu bali hata kkwenye miradi ya familia. Mzazi ndiye unapaswa kuhakikisha kuwa unakuwa unawaachia nyumba watoto wako wakati mwingine unasafiri na kuwaacha peke yao ukiwa umewapa maelekezo ya lipi la kufanya na lipi siyo lazima walifanye. Watoto wakizoea kuishi peke yao nyumbani itawajenga kisaikolojia na kijamii kuweza kuhimili upweke wa kuishi peke yao hata kama wazazi watakuwa wameondoka duniani.

Mzazi hutakiwi kuishi na watoto wako bila kuwaeleza kuwa kuna siku utazeeka na kushindwa kufanya kazi tena. Watoto waelezwe na wafahamu kuwa maisha yana mwisho wake. Kila jambo lina mwisho wake hivyo na wazazi pia kuna siku watazeeka na kufariki dunia.

Wazazi wenye busara hujizoeza kuwazoeza watoto wao kuishi peke yao hata kama wao hawatakuwepo tena duniani. Wazazi wenye busara siyo tu kwamba wanaweka utaratibu ambao utawafaa watoto kuishi vyema kifedha bali pia huweka utaratibu wa kuweza kuwafanya watoto waishi vyema na kijamii pindi wazazi wakiwa hawapo tena duniani.

Aidha, washauri wengi wa mambo ya kijamii hushauri wazazi kuhakikisha kuwa tunaweka wosia kwenye maandishi ambao utakuwa wa kisheria utakaosaidia watoto waishi vyema bila kufarakana hasa pale wazazi watakapoondoka duniani au ikitokea kufarakana kwenye mahusiano yao kama wanandoa.

Mbinu ya -27-

Usiwe Mkali Sana Kwa Mtoto Wako

Kama unataka watoto wako wapate utajiri wa kweli na waishi maisha ya raha na furaha hakikisha kuwa unawalea katika utamaduni wa upendo, ukarimu na upole. Utamaduni wa kuwa mkali kwa watoto mpaka wanakuogopa wanapokuona ni utamaduni wa hatari sana. Utawasababishia watoto wako kuwa waoga wasiothubutu. Watoto wasioweza kuuliza wala kuhoji lolote lisilokuwa sahihi.

Watoto ili waweze kuwa mabilionea lazima uwape uhuru wa kukuuliza maswali au kuweza kumuuliza mtu yeyote maswali bila kuogopa matokeo ya kuuliza swali au hoja yoyote. Wazazi wengi huwafanya watoto wao kuwa masikini kwa sababu ya jinsi wanavyowalea kwa maneno au matendo.

Wapo wazazi wanakuwa wakali sana kiasi kwamba mtoto hawezi hata kucheza na baba wala mama. Ukiwa mkali kwa watoto wako haitawasaidia kuweza kuwa wabunifu wa miradi wala utalaam. Kama tunataka watoto wetu watueleze kila kitu kinachowasibu sirini au popte pale ni lazima tuwalee katika upendo na ukarimu ili waweze kujisikia raha na amani kutueleza lolote au ndoto zao. Tuwaache watoto wetu wawe huru kujieleza mbele yetu ili kuwajengea uwezo wa kujieleza hata mbele ya watu wengine.

Kumbuka unamlea mtoto wako kuwa bilionea hata kama wewe siyo bilionea leo, lengo lako wewe ni kuwaona watoto wako wakiwa mabilionea. Huwezi kuwa bilionea ambaye hawezi kujieleza mbele ya watu. Kumbuka kuwa bilionea ni mtu amabaye anaheshimika sana katika jamii na kwa hiyo muda mwingi atakuwa anakutana na watu wengi wenye mamlaka

serikalini na hata makundi ya watu wengi kitaifa na kimataifa wakiwa wanataka kumsikia ushauri wake. Kwa hiyo mtoto wako anatakiwa kujengewa uwezo wa kusema mbele ya watu wachache na hata mbele za watu wengi ili hapo baadaye akishakuwa bilionea asije kushindwa kuongea mbele za watu wengi. Kwa hiyo, wazazi tujitahidi sana kubadilika tusiwe wakali kwa watoto wetu kupindukia ili tusiwazuie watoto wetu kuimarisha vipaji vyao.

Mbinu ya -28-

Wafundishe Watoto Kuitazama Kesho yao

Kuna wazazi wengi wanaishi kama vile hakuna kesho. Wengi wanaoishi hivyo, wakipata pesa wanazitumia kwa fujo kama vile dunia inaisha kesho au kama vile dunia inafikia kiyama kesho. Utamaduni huu ni utamaduni mbaya sana. Wazazi haipendezi kame kuwalea watoto katika malezi yasiyowafanya watoto kuelewa kwamba hapa duniani wamekuja kufanya nini. Usiwalee watoto katika utamaduni ambao wakipata pesa wao wanachojua ni kuzitapanya na kuzifuja zote mpaka zinapoisha.

Kama tunataka watoto wetu waweze kumiliki utajiri mkubwa sana ni lazima tuwafundishe kuwa maisha yanaendelea. Tuwafundishe watoto wetu wajue kuwa maisha hayana mlango mmoja wa kutokea.

Tuwafundishe watoto wetu kujua kuwa mlango mmoja wa mafanikio unapofungwa Mungu atafungua mlango mwingine tena wa kuendelea kupata mafanikio. Watoto wetu wasifikirie kwamba maisha yao ya kesho yanazimika kwa sababu tu mradi mmoja umekufa. Kama unafanya mradi mmoja na mradi huo ukashindikana haina maana kwamba kesho yako ndiyo imezimika. Kila mara kumbuka kuwa mlango mmoja unapofungwa kuna mlango mwingine Mungu atakufungulia na utapata mafanikio makubwa kesho ikiwezekana hata kuzidi mafanikio uliyokuwa unayapata kwenye mlango namba moja uliokuwa unautegemea.

Katika kitabu hiki swala la kuitazama kesho ninataka kumaanisha kwamba watoto au vijana wetu tuwafundishe kujua pande mbalimbali za maisha. Nataka kuhamasisha msomaji wangu kuwa kama huwafundishi watoto wako kuiona kesho

yao kwa jicho kubwa sana tangu wakiwa wadogo, utashindwa kuwawezesha kujua maana ya maisha. Ukweli ni kwamba maisha yanaleta maana kama kesho imeandaliwa vyema. Maisha tunayoyaishi leo yamejengwa kwenye msingi imara au dhaifu uliowekwa jana na wazazi wetu au juhudi zetu wenyewe. Hakikisha kuwa watoto wanafundishwa kutotumia pesa au mali yoyote waipatayo bila kiasi. Wafundishe watoto wako kuwa na kiasi. Wawe na kiasi kwenye kutazama televisheni. Wawe na kiasi katika kupenda michezo ya kuigiza. Wawe na kiasi katika kupenda filamu au maigizo. Hapa ninamaanisha kuwa wasiwe watumwa wa jambo lolote ambalo litawafanya wasahau majukumu mengine.

Mtoto awapo na umri wa kuanzia miaka 2 afundishwe na azoezwe kutokuwa na ulevi wa kitu chochote ambacho chaweza kuathiri maisha yake ya baadaye. Watoto wasiwe malimbukeni wa mitandao ya simu. Watoto wako wasiwe walevi wa Facebook, Wasiwe walevi wa filamu za kwenye televisheni, wasiwe walevi wa muziki hata kama ni muziki wa dini, wasiwe walevi wa mitandao kama Twitter, Viber, Whatsapp, nk. Wakiwa walevi wa maswala hayo watashindwa kuitazama kesho yao na kujikuta wanashindwa kufaulu masomo yao, watashindwa kufanya majukumu ya familia. Watashindwa kutimiza majukumu yao kwa jamii na hatimaye taifa zima linakuwa kama limegoma.

Mbinu ya -29-

Epuka Kuishi na Mtoto wa Umri wa Miaka 21

Mbinu hii ni ya muhimu sana kama unataka kuwalea watoto wako kibilionea. Njia pekee ya kukwepa kuishi na mtoto wako mwenye umri wa zaidi ya miaka 21 ni kumpatia mtaji au mafunzo yenye kumuongezea elimu na ujuzi au miradi ya kufanya. Ni aibu sana iliyoje kuishi na watoto wako watimizapo umri wa miaka 21. Umri wa miaka 21 ni umri wa mtu mzima ambaye anapaswa kuanza kujitegemea na Kuzalisha mali kwa faida ya wananchi wengine. Hakikisha kuwa unawawezesha watoto wako kuishi kwenye nyumba zao ili wawe na uhuru wa mtu mzima. Haifai kuishi na watoto wenye umri mkubwa nyumbani wakati wanaweza kujitegemea kabisa.

Inasikitisha kuona kwamba bado kuna wazazi wanadhani kwamba kuishi na watoto wao ni upendo. Wanadhani kuishi na watoto wao hata kama wameshakuwa wakubwa ni upendo. Kwamba kama unawapenda watoto wako kwa nini usikae nao bwana. Lakini ukweli ni kwamba kanuni za maisha ya wanadamu ni kwamba kila mtu awapo mkubwa kwa mwili na kwa akili anapaswa ae na uhuru wake. Kuishi na watoto tena wenye umri mkubwa wakati mwingine waliokwishaingia kwenye ndoa ni kuwanyima amani na raha pamoja na ufaragha unaotakiwa kuwepo kwa watu wote.

Mtoto ambaye bado anaishi pamoja na wazazi wake, hata kama ameshapata kazi ya kumpatia kipato inamfanya mtoto awe na fikra finyu sana za kimapinduzi. Mtoto hawezi kuwa na uhuru wa kujiamulia maswala yanayomuhusu kindoa, kimapenzi na mwenzi wake, kifedha, kiuchumi, nk kwa sababu yuko chini ya utawala wa baba au mama yake. Mtoto awapo chini ya utawala wa wazazi wake hawezi kuwa na maendeleo ya kweli

au makubwa. Mtoto awapo chini ya wazazi wake akiwa tayari mwenye umri mkubwa au akiwa tayari amekwishaoa hataweza kukua kifedha na kimawazo. Hataweza kutatua changamaoto za maisha yake na mwenza wake. Hataweza kuinjoi maisha kwa viwango anavyovipenda.

Mwachie mtoto wako akaishi kwenye nyumba ya kupanga ili ajue changamoto za nyumba za kupanga. Mwachie mtoto wako akakae kwenye nyumba yake binafsi. Mjengee nyumba mtoto wako kwenye ploti yake kama unao uwezo wa kifedha wa kufanya hivyo. Mtafutie ploti yake ya kuishi baadaye atakapokuwa mtu mzima. Hakikisha unanunua ploti za watoto wako tangu wakiwa wadogo na watimizapo umri wa kujitegemea waruhusu wakaishi kwenye nyumba zao. Kama wewe mzazi hauna uwezo wa kuwajengea nyumba za kuishi watoto wako mara watimizapo umri wa miaka 21, jitahidi basi kuwapa uhuru wa kwenda kuishi kwao.

Mbinu ya -30-

Wazoeze Watoto Kutumia Kipato Chao

Jambo lingine ambalo linasababisha watu kuishiwa pesa na kubaki maskini, ni swala la watoto wetu kujiingiza katika utamaduni wa kutumia pesa kama vile dunia inaenda kuteketea kesho. Ni utamaduni wa kutumia pesa kuliko kipato tulichoncho.

Sisi wazazi tunapaswa kuwaeleza watoto kuwa matumizi yao hayapaswi kuzidi kipato chao. Hata kama ni bilionea, tumia pesa chini ya kipato chako. Kama kipato chako ni shilingi milioni moja hakikisha matumizi yako ni chini ya shilingi milioni moja.

Utamaduni wa kutaka kuishi jinsi watu wapendavyo badala ya upendavyo wewe ni utamaduni wa kitumwa. Acha kuishi kwa kufuata watu wanasemaje. Wewe unatakiwa uishi kwa kufuata ndoto yako ya maisha uliyonayo. Kama hadi sasa unaposoma kitabu hiki hauna ndoto yoyote maishani mwako nakusihi sasa uwe nayo kuanzia leo.

Na kama hujui jinsi ya Kuweka ndoto yako ya maisha itakayokuongoza kuishi upendavyo na sivyo watu watakavyo, nakudokezea kidogo tu hapa maana ya ndoto ya maisha yako: Ndoto ya maisha yako ni ile dira au taswira uliloyonayo moyoni mwako au kwenye fikra zako za jinsi unavyopenda uwe baadaye wewe na familia yako. Ndoto ya maisha ni picha unayokuwa nayo wewe peke yako kichwani mwako na watu wengine hawawezi kuiona wala kuiondoa kichwani mwako.

Picha hiyo unaweza kuipata wakati ulipokuwa mdogo kulingana na malezi uliyoyapata kwa wazazi wako au unaweza kuipata kutoka kwa watu wengine wanaokuzunguka au unaweza kuipata kutokana na vitabu au mafundisho unayoyapata mara kwa mara.

Mfano wa picha au ndoto unayoweza kuwa nayo ni hii:

1. Miaka kadhaa ijayo nataka na mimi niwe na mume wangu wa kuishi naye mpaka kufa kwetu.
2. Miaka ijayo nataka niwe na mke wangu mwenyewe wa kuishi naye kwenye shida na raha
3. Miaka ijayo nataka niwe na nyumba yangu binafsi nzuri sana yenye kuvutia mtaani kwangu.
4. Siku zijazo nataka na mimi ninunue gari zuri la kutembel ea mimi na mwenzangu, tuwe tunaenda pamoja sokoni, mjini, kanisani, matembezini, nk.
5. Siku za baadaye nataka nisome mpaka nipate digrii
6. Miaka ijayo nataka niwe rubani wa ndege ndiyo maana na soma sana masomo ya sayansi.
7. Miaka ijayo kama kumi hivi nataka niwe bilionea mkubwa Afrika.
8. Miaka ijayo kama 8 hivi nataka niwe nimeshamaliza masomo yangu ya Udaktari niweze kuwa daktari bingwa wa magonjwa ya moyo.
9. Nataka niwe bilionea miaka kumi ijayoili baadaye nije ku wasaidia wazazi wangu watoke kwenye maisha magumu nao waishi kwenye nyumba nzuri sana kama watu wengine.
10. Nataka nianzishe kampuni zangu binafsi za biashara ili nije kujiajiri mwenyewe ndiyo maana nasoma masomo ya fedha na biashara.
11. Nataka miaka ijayo niwe mchungaji wa Kanisa kubwa lenye watu wengi sana mjini na niwe Askofu.
12. Nataka nije kuwa na simu nzuri sana ya Ipad au ya smart phone ili niwe na mimi naitumia kwenye kupata taarifa za muhimu kutoka kwenye mitandao.

Hizo ndizo zaweza kuwa mfano wa ndoto za maisha ya mtu anayelenga kupata mafanikio au kupata jambo zuri miaka ijayo. Kwa hiyo, kama kwa sasa wewe hauna ndoto yako mwenyewe

ujue kuwa utaendeshwa na watu wenye ndoto zao. Narudia, kama hauna ndoto yako unayoichuchumilia iweze kutokea maishani mwako kuanzia leo na siku za baadae ujue kuwa utakuwa unatumikishwa kutimiza ndoto za watu wengine.

Hakikisha kuwa watoto wako hawatumikishwi kutimiza ndoto za watu wengine. Wazoeze watoto sasa kutumia kipato chao na wawe na uzoefu wa kutumia pesa inayolingana na kipato chao. Wasinunue vitu vya burudani visivyolingana na kipato chao. Wasifanye mambo ambayo yanazidi kiasi wanachopata. Wasiishi kwenye mkumbo wa watu wengine. Wasivutwe huku na kule kutimiza ndoto za watu wengine bali watulie kuhakikisha ndoto zao za maisha zinatimizwa.

Mtoto asipozoezwa kutumia pesa kulingana na kipato chake atajikuta anatumia pesa vibaya tangu akiwa mdogo na kujikuta tabia hiyo anaendelea nayo ukubwani. Mzazi ndiye anayepaswa kumwelekeza na kumzoeza jinsi ya kupanga bajeti ya mahitaji na kuzoeza kupanga Kununua vitu vya lazima dhidi ya vitu muhimu.

Mtoto afundishwe kujua kuwa siyo kila kitu ni cha lazima maishani hata kama amekiona kwa watoto wengine. Mkataze mtoto Kununua kila kitu anachoona kizuri akingali mdogo. Mfano uwapo na mtoto matembezini au kwenye maduka usikubali kumununulia kila kitu anachoomba kwako. Mwambie kwa nini haununui kitu hicho.

Mwambie ni kwa nini unakatalia kupenda kila kitu anachoona kizuri. Sababu kubwa iwe kwamba siyo kila kitu kinamfaa mwilini mwake au maishani mwake. Mfundishe kujikana nafsi yake kwa kumkatalia Kununua kila kitu nafsi yake inataka. Kama anataka pipi au biskuti mwambie kuwa biskuti inaharibu meno na afya yake. Mwambie kuwa akila sana biskuti na pipi meno

yake yatadondoka na abaki kibogoyo. Mpatie mifano ya watoto unaowajua wameharibu meno yao kwa kula pipi na biskuti.

Mkatalie kabisa kula biskuti na pipi. Kamwe wewe mwenyewe usimpe pipi, jojo, biskuti au peremende kwani zitamharibia meno yake yote. Kwa kumlea mtoto hivyo akiwa bado mdogo atazoea kabisa na kuwa huru kujua lipi la muhimu kwake na lipi siyo la muhimu. Hata akiwa bilionea atakuwa anatumia pesa kulingana na ndoto yake na misingi aliyopewa na baba yake.

Mbinu ya -31-

Wajulishe Watoto Kuwa Maisha ni Mapambano

Kama unataka watoto wako wawe mabilionea, hakikisha kuwa unawazoesha kuyaona maisha kuwa ni mapambano na siyo burudani na starehe. Wakumbushe kila siku kuelewa kwamba wasipopambana kufa na kupona tangu wawapo shuleni na wawapo mtaani maisha yatawashinda.

Watoto waelimshwe kila mara kwamba kazi yenye kutoa kipato chenye tija ni heshima. Watoto wajue kuwa kazi ni wajibu wa mwanadamu awapo hapa duniani. Watoto wajulishwe kuwa kufanya kazi siyo mateso wala utumwa.

Kuchapa kazi na kupata mapato ya kweli ndiyo pekee itakayowawezesha watoto kujiwekea mazingira ya kuendelea kuwa matajiri wa baadaye. Waelezwe kwamba ni ama wapambane na umaskini kufa na kupona waweze kuwa mabilionea au wasipambane na umaskini waishi maisha ya kimaskini milele.

Mzazi usiwazoeze watoto kwenda kwenye matamasha ya nyimbo na muziki. Usiwazoeze watoto kwenda kwenye baa za vilevi usiku. Usiawapeleke kamwe kwenye majengo ya starehe na burudani. Mzazi ukifanya hivyo ukawazoeza hivyo usitarajie kuwaona watoto wako wakiwa wachapa kazi.

Usitarajie kuwaona watoto wako wakiweza kudumu kwenye utajiri. Wafundishe kutenganisha muda wa burudani na muda wa kazi. Wafundishe watoto kujua saa ya kazi na saa ya burudani. Hii itawasaidia kujua kutenganisha starehe na kazi.

Katika kizazi cha sasa ambacho watu wengi wanashabikia starehe na ngono au pombe na mziki na kustarehe tu bila kazi haiwezekani watoto wetu wakapata utajiri wa kudumu kama

hawatadumu katika kuwa na utamaduni wa kuchapa kazi. Kama wato to watapenda starehe ngono na burudani zaidi ya wanavyojali kazi na wajibu hakika hawatadumu kwenye utajiri. Watafilisika mapema kabisa.

Watoto wasiozeozwa kuwa wachapa kazi wakingali wadogo watakuwa wavivu na wabaguzi wa kazi. Hawatakuwa na juhudi za kujituma bila kusukumwa kufanya jambo. Hawataweza kufanya kazi zenye tija kwa ajili ya kujipatia mamilioni ya pesa. Watakuwa mazezeta tu.

Mbinu ya -32-

Usiwazoeze watoto Kudhani Maisha ni Sherehe

Kuna watu hudhani kuwa maisha ni sherehe. Kila sherehe wanatamani wawepo. Wataenda kila mwisho wa wiki kwenye sherehere za watu mbalimbali. Wakiaalikwa hawakosi kwenye sherehe kama hizo.

Mara sherehe za kuzaliwa (birthday parties), mara wako kwenye sherehe za harusi, wiki ijayo utawakuta wako kwenye sherehe za "sendo-offs", wiki nyingine utawakuta wapo kwenye sherehe za harusi, nk. Katika malezi ya kimilionea ya watoto haina mantiki kuwalea watoto katika mitazamo na misingi kama hiyo. Watoto ukiwakuza katika mtazamo au mazoea ya kufanya tafrija na sherehe za mara kwa mara watajikuta bongo zao za ukubwani zikiwatafsiria kwamba maisha ni starehe. Watayaona maisha kuwa ni burudani tu.

Watoto hujikuta wanayatafsiri Neno starehe hutumiwa kwa maana na makusudi tofauti kulingana na mahali au mada husika inayozungumzwa. Kwa mfano; maandiko matakatifu yanasema Mungu alipomaliza kazi ya uumbaji "...alipumzika na kustarehe...". hata hivyo katika jamii yetu wapo watu wanaotafsiri au kujua kuwa kustarehe ni kula sana chakula kizuri sana, kunywa pombe na kulewa sana, kufanya ngono na wanaume au wanawake, kucheza muziki, kucheza bao, kucheza pool, kwenda vilabuni usiku, kulala sana, kwenda kuogolea, kwenda disko, nk.

Hayo ndiyo yanayotazamwa na jamii ya watu wetu kuwa ndiyo maana ya starehe. Ukiambiwa kuwa watu wako kwenye starehe zao ujue wako wanafanya moja ya mambo hayo. Katika kuhamasisha watoto wetu waweze kujikomboa kiuchumi hadi

waweze kuwa mabilionea wa ukweli ni lazima watoto wetu wawapo bado wadogo kuanzia mwaka 0 hadi 15 tusikosee kuwazoeza kushiriki starehe kama hizo.

Wazazi wengi wenye kipato kikubwa wanakosea kwa kudhani kwamba ndiko kuwapa uhuru watoto. Wapo wazazi wanaoenda baa na watoto wao wa miaka 5 au miaka 8 na kukaa nao mpaka saa za usiku. Kwakweli huu ni uhuni na malezi ya kijinga. Kama mzazi huwezi kwenda peke yako kwenye maeneo ya kunywa pombe.

Mbinu ya -33-

Wazoeze Kufikiria nje ya Sanduku

Pamoja na mambo mengine mengi, sababu nyingine inayofanya Afrika kuzidi kuwa maskini ni kwa watu wake kuendelea kufanya mambo kwa mazoea, kufanya kazi kwa njia zile zile za kila mara kwa fikra zile zile. Watoto wako ili waweze kuwa matajiri wa baadaye lazima mzazi uwazoeze mapema kuwa wadadisi, wachambuzi, wanaojihoji na wenye uwezo wa kuhoji. Waruhusu waweze kujitambua kifikra na kiroho. Wawezeshe kujielewa kibayolojia na kimaumbile. Watoto wako wakijitambua kwa upana sana hawatakuwa watu wa kuenenda bila utaratibu katika jamii.

Watoto wanaojitambua vyema ni rahisi kuwa na fikra huru zenye uwezo wa kufikira nje ya sanduku au kama wazungu wanavyosema “thinking outside the box” ikimaanisha kuwa mtu anapaswa kuwaza nje ya mazoea yake. Kama mtu amezoea kufanya jambo fulani kwa njia fulani na kwa mtindo fulani hawezi kupata matokeo tofauti mpaka abadilishe mbinu na jinsi ya kutekeleza mambo yake hatafanikiwa.

Mzazi ukiweza kuwalea watoto katika mfumo ambao unawaruhusu kuuliza maswali mtu yeyote, ukawaruhusu kukuuliza wewe mwenyewe maswali kama mzazi yaani wakuulize swali lolote kuhusu lolote analolitaka hakika watoto wako watakuwa wadadi kuanzia wakiwa wadogo hadi wakiwa watu wazima.

Hakikisha kuwa watoto wako waulizapo swali lolote hata kama hulijui jibu lake, wewe watie moyo watoto wako wala usiwakatishe tama. Hata kama mtoto anauliza swali bovu au swali la kijinga kwa mtazamo wako wewe usimcheke wala kumgombeza.

Mtoto anayeuliza maswali kuanzia akiwa nyumbani akiwa mdogo ataendelea hivyo hadi akiwa mkubwa na atakuwa mtu anayewaza nje ya mazoea au nje ya sanduku la mazoea. Kila mara hakikisha kwamba mtoto wako wewe mwenyewe unamuuliza maswali mengi kadri uwezavyo. Muulize maswali yoyote kuhusu lolote. Muulize maswali ya shuleni. Muulize maswali ya ufahamu. Muulize maswali ya kanisani. Muulize maswalii ya msikitini.

Kila mara hakikisha unamzoeza kujibu na kujiuliza maswali. Hii itamfanya mtoto aweze kuwa mtu huru mwenye uwezo wa kuhoji, mwenye uwezo wa kujibu. Mwenye ari ya kufanya kazi nje ya mazoea. Mtoto azoezwe kujisomea majarida yenye mada mbalimbali. Majarida yenye kufikirisha sana. Azoezwe kusoma majarida yenye kumfanya kuwaza kwa kina. Mtoto azoezwe kusoma vitabu vyenye kumfanya kuwaza zaidi nje ya mazoea. Mtoto akizoea kusoma vitabu vyenye kumfikirisha hakika atakuwa mdadisi asiyefanya mambo kwa mazoea. Atakuwa tajiri mbunifu anayekwenda na mabadiliko ya wakati na teknolojia. Atakuwa tajirianayewaza nje ya sanduku.

Mbinu ya -34-

Epuka Kumtukana Mtoto anaposhindwa Masomo

Sababu nyingine inayowafanya watoto wasifanikiwe maishani mwao, ni kasumba ya wazazi na walimu wengi katika shule na vyuo wengi kuwalea watoto kwa kudhani kwamba elimu rasmi ndiyo suluhisho pekee la maisha bora maishani mwa watoto wetu. Ukweli ni kwamba siyo kila mtu anayefeli masomo rasmi ya shule au chuo anakuwa amefeli na kifedha maishani.

Ni bahati mbaya kwamba mifumo ya shule zetu za Tanzania haimwandai mtoto kuwa anachotaka maishani mwake. Kwa kiwango kikubwa mifumo yetu ya elimu rasmi humwondoa mtoto kwenye mstari wa ndoto yake na kumpeleka mahali ambapo hakupataka kabisa au hapakuwa ndoto yake.

Mifumo ya shule zetu haimwandai mtoto kuwa milionea au bilionea. Humwandaa tu kuwa mtumishi wa watu. Humwandaa mtoto atakapomaliza shule atafute ajira siyo asababishe ajira kutokea. Shule zetu huwandaa wahitimu kuwa madaktari, wauguzi, wahasibu, walimu, madereva, wahandisi, n.k. hatuna mfumo wa elimu unaoweza Kuzalisha watu watakao miliki viwanda vya chuma, watakaofungua viwanda vya kusindika mazao ya kilimo. Hatuna mfumo wa elimu utakaotoa wahitimu ambao watasababisha mambo yatokee.

Bali tuna mfumo wa elimu unaotoa wahitimu wanaoshangaa yanayotokea. Hali hii inasababisha kila kijana anayehitimu atamani kwenda miji mikubwa kama Dar Es Salaam, Mwanza, Arusha, nk ili akashangae kwanza miji hiyo na maghorofa yake. Nimeona nikupatie maelezo hayo ili ujue kuwa elimu itolewayo mashuleni siyo suluhisho la maisha ya watoto wetu. Kama unapata ripoti ya mtoto wako kuwa amepata daraja baya

darasani na ukaanza kumgombeza na kumtukana, unakosea sana. Mtoto akipata daraja lisilokuridhisha masoni wewe kama mzazi wake siyo muda mwafaka wa kumtukana na kumwambia kuwa hana akili, hana bidii, hasomi, hazingatii anavyoambiwa, nk. Ni vyema kujua kuwa hata mtoto mara nyingi hafurahii kupata daraja baya darasani. Kama inatokea mtoto wako amepata daraja baya masomoni pamoja na bidii zake zote, wewe mtie moyo na uendelee kumwonyesha kwamba siyo mwisho wa dunia. Mweleze mtoto asife moyo. Mweleze mtoto kuwa bado maisha yanaendelea na maisha yake yatakuwa mazuri tu kama atafanya bidii zaidi siyo tu kwenye masomo bali pia kwenye maisha.

Kuna wazazi wanapaswa kujitambua na kubadilika. Haileti tija kumgombeza mtoto wako kwa sababu amepata alama mbaya usizozipenda wewe. Hii ni kwa wote wenye watoto wa kike au kiume. Epuka kmtukana mtoto wako kwa sababu hapati alama kubwa sana. Epuka kumkwaruza kwa maneno au vitendo. Hata kama mtoto wako kapata alama ziro kwa masomo yote. Wewe usimgombeze hadi akakuona kuwa hufai. Ukimgombeza mtoto kwa sababu wewe hukufurahishwa na alama zake, utakuwa unamwonea tu.

Mbinu ya -35-

Mfundishe Mtoto Kutopoteza Muda

Tatizo kubwa Afrika ni kupoteza muda. Unaweza kukutana na mtu akakwambia , “niko napoteza muda hapa”. Yaani mtu anajisikia fahari kusema yuko anapoteza muda kidogo kwa kunywa pombe, kunywa kahawa, kutembea bila mpango, kupiga soga, na mengine mengi.

Kupoteza muda ni dhambi. Watoto wakifundishwa kwa maneno, nadharia na vitendo kutoka kwa wazazi hakika hawatapoteza muda. Hawatapoteza muda kwenye vijiwe vya uongo na umbea. Hawatapoteza muda kwenye shughuli zisizo za maana maishani. Wazazi tunapaswa kuwasaidia watoto wetu kwa kuwaonesha kuwa muda ni rasilimali isiyoweza kupatikana tena ikishapotea.

Huwezi kuipata dakika moja iliyopotea. Kama kizazi kijacho kitakuwa kina mwamko wa kutunza na kukomboa wakati, kitakuwa kizazi chenye kufanya maendeleo. Kizazi kitakuwa chenye fedha nyingi. Kizazi kitakuwa chenye furaha na amani. Muda ni mali. Kupoteza muda ni kupote mali. Mwandishi mmoja anasema kuwa muda siyo mali tu bali ni uhai wa mtu.

Mzazi ni vyema akamfundisha mtoto kujali kila chembe ya muda. Mtoto akiwa bado hajawa mkubwa azoezwe kutunza kila sekunde. Ifahamike kuwa kila sekunde huunda dakika. Kila dakika hutengeneza saa. Kila saa hutengeneza siku. Kila siku hutengeneza wiki. Kila wiki huunda mwezi. Kila mwezi huunda mwaka. Na kila mwaka hutengeneza muongo mmoja na muongo mmoja hutengeneza karne moja. Kwa kutambua hilo, kila mtu anapaswakuzoezwa kutunza muda ikiwa ni kila sekunde. Kama vile mtu anavyoumia kwa kutokwa na mtu ampendae vivyo hivyo ni vyema kuumia kwa kupotea kwa dakika au saa bila

kuitumia kwa faida yoyote kiuchumi. Kama mtoto atazoezwa kwa maneno na kwa vitendo, hakika atakuwa mtunzaji mzuri wa muda na atakuwa anaweza kufika kwa wakati kwenye vikao, mikutano, ibadani, na kazini.

Mbinu ya -36-

Mfundishe Mtoto Kuchukua Hatua za Hatari

Mwandishi maarufu wa vitabu duniani Prof. Benson Idahosa anasema, “ni hatari kuchukua hatua za hatari lakini ni hatari sana kutokuchukua hatua za hatari” Watalaam wa maswala ya ujasiriamali wanaeleza kuwa mjasiriamali ni mtu anayeweza kuchukua hatua za hatari. Hatua za hatari ni kama vile Mkulima anavyokuwa jasiri kupanda mbegu za maharage au mahindi huku akijua kuwa hana maharage au mahindi ya kutumia kwenye chakula. Kule kuzika mbegu zote ardhini huku akiwa hana chakula kingine nyumbani ni hatua ya hatari sana.

Lakini ukimchunguza mkulima huyo utagundua kuwa ujasiri wake anaupata kwenye imani yake ya asili aliyonayo kuwa atapata njaa kwa muda wa miezi 2 tu na baada ya hapo njaa itakuwa historia kwake. Baada ya kuvuna mazao yatokanayo na mbegu aliyopanda mkulima husahau kabisa mateso aliyoyapitia wakati anasubiri mavuno. Huko ndiko kuchukua hatua za hatari.

Mfano mwingine wa kuchukua hatua za hatari ni huu hapa. Kama mtu akipewa pesa kiasi cha shilingi milioni tano (5,000,000) na akaamua kuzitumia zote kwenye biashara inayomlipa baada ya miezi 3 au 6, ni dhahiri kuwa kufanya hivyo huku ukiwa huna pesa nyingine ya kukuwezesha kutatua changamoto za kifedha kwa miezi 3 au 6 ijayo kabla ya kuanza kupata faida, ni kuchukua hatua ya hatari.

Usemi wa Profesa Benson Idahosa mwandishi maarufu wa vitabu duniani kuwa “ni hatari kuchukua hatua za hatari lakini ni hatari sana kutokuchukua hatua za hatari” humaanisha kuwa kabla ya kuchukua hatua yoyote ya hatari hakikisha kuwa umepata ushahidi wa kutosha bila kuacha mashaka kuwa hatua

utakazozichukua zitaleta matokeo makubwa baada ya muda. Ni hatari kubwa sana kutokuchukua hatua za hatari kwani matokeo yake yatakuwa mabaya zaidi kwako mwenyewe. Mkulima akiogopa kuchukua hatua ya kuzamisha mbegu za maharage au mahindi ardhini au udongoni badala ya kupata shida ya kukosa chakula kwa miezi miwili tu atateseka zaidi kwa njaa kwa zaidi ya mwaka mzima.

Mjasiriamali aliyepewa shilingi milioni tano (Tshs 5,000,000) akaamua kuzitumia zote kwa mahitaji aliyonayo kwa sasa, atakumbana na ugumu wa maisha kwa miaka yake yote iliyobakia kwani alipaswa kuchukua hatua ya hatari ya kukosa mahitaji ya fedha kwa muda kitambo ili baada ya miezi 3 aanze kufurahia faida ya biashara yake.

Mtoto anaweza kufundishwa kuchukua hatua za hatari kwa vitendo. Mtoto anaweza akaelezwa kuchukua hatua za hatari kwa maneno au nadharia. Mtoto anapaswa kuzoezwa kuchukua hatua za hatari ili ubongo wake uzoezwe kuchukua hatua kubwa ambazo kwa muda kitambo huweza kuhesabika kama za hatari lakini matokeo yake kwa kipindi kifupi kijacho hatua hizo huleta matokeo makubwa.

Mbinu ya -37-

Mtoto aelimishwe kuwa Fedha ni Jawabu la Mambo yote

Kama mzazi unataka watoto wako wakiwa wakubwa wawe mamilionea hakikisha kuwa unaujenga ubongo wao kuwa ubongo mkubwa. Wazazi wenye akili kubwa hutamani hata watoto wao wao na ubongo wenye akili. Wazazi tufahamu kuwa ubongo wenye fikra pana kwa mtoto unajengwa tangu utotoni.

Ukweli ni kwamba usipomjenga mtoto wako kuwa na ubongo unaoelewa maana halisi ya fedha na umuhimu wake maishani hataelewa akiwa mkubwa tayari. Mtoto hatajua fedha zinapatikanaje. Hataelewa fedha zina nguvu gani. Hatajua kwa nini atafute fedha maishani mwake. Hataelewa mbinu za kutafuta fedha kama ubongo wake haukuzoezwa kuelewa sababu za kutafuta fedha. Maandiko matakatifu yanasema, "……fedha huleta jawabu la mambo yote…" (Mithali 10:19).

Ukweli ni kwamba fedha huleta jawabu la mahitaji yote ya mwanadamu. Hilo ndilo linapaswa kuwa jambo la kumweleza mtoto kila mara unapomweleza swala la fedha. Ubongo wake ujengwe kuelewa kuwa kila unapopata fedha unawekeza ili baadaye fedha hiyo izae fedha tena baadaye. Kama mtu anahitaji gari zuri la kutumia kwa usafiri atahitaji fedha ya kulinunua.

Kama mtu anahitaji nyumba ya kifahari lazima awe na fedha ya kutumia kujenga au Kununua nyumba hiyo ya kifahari. Kama unataka kula chakula kizuri, kuvaa vizuri, kutumia simu nzuri, runinga nzuri ya nyumbani, kusafiri huku na kule, kunywa maji safi na salama; lazima kuwa na fedha ili yote hayo na mengineyo mengi yawezekane.

Mtoto anapaswa kujengewa fikra chanya kuwa fedha ni kifaa cha kupata vitu au huduma unazohitaji. Mtoto ajengewe uelewa mpana kuwa fedha ni jawabu la mambo yote katika mtazamo kuwa fikra sahihi, mawazo sahihi, matendo sahihi kwa wakati sahihi ndivyo huleta fedha. Kwa hiyo, fedha inapaswa kutazamwa kuwa ni nyenzo. Nyenzo ya kupata kila kitu.

Mtoto akumbushwe kuelewa tofauti ya "fedha ni jawabu la mambo yote" na "fedha ni kila kitu". Kuna kasumba ya kudhani kuwa fedha ni kila kitu badala ya kusema fedha ni jawabu la mambo yote. Kama watu wataelewa vibaya tofauti ya dhana hizi mbili, watu wataendelea kutafuta fedha kama kitu cha kutumia badala ya fedha kuwa nyenzo ya kuleta jawabu la mambo yote. Nyenzo ni kitu kitumiwacho kurahisisha kazi. Mfano, gari ni nyenzo ya kusafiria kutoka eneo moja kwenda eneo lingine. Kisu ni nyenzo ya kukatia vitu kama nyanya, vitunguu, nk. Simu ni nyenzo ya mawasiliano. Kuna aina nyingi za mifano ya nyenzo. Fedha kama nyenzo, inapaswa kutafutwa kwa kila namna kwa nia moja tu, kuitumia kama nyenzo ya kupatia majawabu ya mahitaji ya mwanadamu.

Mtoto ajengewe fikra hiyo kuwa fedha ndiyo nyenzo kuu duniani inayoweza kuleta jawabu la mambo anayoyataka duniani. Mtoto ajulishwe kuwa fedha siyo nyenzo ya kuleta furaha ya mwanadamu kwa asilimia mia moja, bali furaha ya mwanadamu huletwa na matokeo ya kazi ya mikono yake. Kwamba ukifanya jambo jema duniani na akili yako ikapendezwa nalo na jamii inayokuzunguka ikafurahishwa nayo, hilo ndilo chimbuko la furaha ya mwanadamu.

Mbinu ya -38-

Mwandae Mtoto Kuwa Bilionea Akingali Tumboni Mwa Mama Yake

Mbinu hii ndiyo kiini cha kitabu changu hiki. Nadhani umepata taaluma ya kutosha kuhusu kuwalea watoto wako kibilionea. Maandalizi ya kuwafanya watoto wako kuwa mabilionea yanapaswa kufanyika mtoto akiwa bado na umri wa miaka 0 hadi 15. Usisubiri kamwe hadi mtoto wako atomize miaka ya ujana yaani kuanzia miaka ya kubarehe au kuvunja ungo ndipo uanze kumwambia mtoto wako maswala ya fedha.

Usiogope kumweleza mtoto wako mada yoyote ihusuyo pesa hata kama bado ni mdogo. Usidhani kuwa mtoto haelewi. Ukweli wa kisayansi ni kwamba mtoto anaweza kuelewa mambo ya fedha au mambo kadhaa hata akiwa bado tumboni mwa mamaye. Mtoto wako awapo tumboni mwako anza kumtabiria mambo makubwa ya kifedha. Anza kumwambia kauli za ubilionea. Mwambie hivi, “mwanangu nataka ukizaliwa ukue vyema hadi uwe bilionea.” Unaweza kumwambia, “nataka uje duniani uwe bilionea wa mabilionea, sitaki uje kuwa hohehahe maishani mwako.”

Ukweli wa kisayansi ni kwamba kauli nzuri za mzazi kwa mtoto anazipokea kwenye ubongo wake tangu akingali tumboni. Mzazi wa kike na wa kiume wanapojaaliwa kupata mtoto wajitahidi kusema naye akiwa bado tumboni mwa mama yake. Wewe tamka tu hata kama bado yuko tumboni. Endelea kumtakia mafanikio na kumwandaa kisaikolojia zaidi kuweza kumiliki uchumi. Hata kama wewe siyo bilionea, mwandaliea ubilionea. Lazima ukatae kuwalea watoto wako katika mweleko wa kifukara. Wazoeshe kutamka mamilioni ya pesa. Wazoeze

kushika pesa nyingi wakiwa bado wadogo. Wazoeze watoto wako kufanya kazi. Wazoeze kumiliki miradi na biashara kubwa. Waoneshe kwamba wamezaliwa kwa ajili ya kumiliki pesa na mali za mamilioni popote Tanzania na duniani kote.

Mbinu ya -39-

Mfundishe Mtoto Kuwa na Mtandao Mpana wa Biashara Kubwa

Waandishi wakubwa duniani kama Robert Kyosaki wa nchini Marekani wanafafanua kwamba watu watakaoendelea kuona mafanikio makubwa kifedha na kiuchumi ni wale tu watakaoendelea kufanya biashara kwa kutumia mfumo wa biashara ya mtandao. Katika karne hii ya digitali Waliojiajiri kwenye biashara ndogo au wale wanaofanya kazi za kawaida wasitegemee kuona wakivuka hatua kubwa za kifedha. Kama tunataka watoto wetu hapo baadaye wawe matajiri wakubwa, tuwafundishe kuunda mitandao mikubwa ya watu wa kufanya nao biashara. Wazazi tujifunze soko la biashara ya mtandao kwani mfumo huo ndio mfumo wenye kuweza kuwapatia watu fursa kubwa kifedha na kiuchumi na kielimu.

Makampuni mengi duniani yanayoendesha biashara zake kwa mfumo wa mtandao yanaendelea kuku asana duniani. Mara nyingi Makampuni yanayofanya biashara zake kwa mfumo wa biashara ya mtandao ndiyo yanayoweza kuvuka vikwazo vingi vya kukua na kutanuka sana. Makampuni ambayo yanatumia mfumo wa biashara ya mtandao hayajikuti yakilazimika kupunguza watumishi au Wafanyakazi wake. Hii ni kwa sababu Makampuni hayo hutumia watu kusambaza bidhaa zake badala ya matangazo na Wafanyakazi wengi.

Mzazi unapaswa kumwandaa mtoto wako kisaikolojia na kimtazamo ili aweze kuwa mtoto anayejitambua akingali mdogo sana. Mimi ninayeandika kitabu hiki nimefanikiwa kwa kiwango kisichokuwa kidogo kuhakikisha kuwa watoto wangu nawazoeza kujifunza kutoka kwa wengine. Ukitaka kujifunza zaidi kuhusu biashara ya mtandao unaweza kujifunza kutoka

zaidi ya Makampuni 100 duniani yanayofanya biashara ya mtandao yaliyoko kwenye intaneti kutoka kwenye "Google" hakika utajifunza makubwa sana. Ukitaka kufanya biashara kubwa lazima ujifunze kwa watu wenye biashara kubwa. Huwezi kuwa na biashara kubwa kama hutumii mtandao mkubwa wa biashara. Wazazi tujifunze na kufuatilia faida za biashara ya mtandao. Kampuni nyingi zinazotumia mifumo ya biashara ya mtandao inasmekana kwamba zitaendelea kupaa sana kibiashara ikilinganishwa na kampuni zitakazoendelea kutumia mifumo ya kale ya biashara.

Makampuni kama vile Vodacom, Tigo na Airtel ni mifano ya Makampuni yanayotumia mfumo wa biashara ya mtandao. Makapuni kama vile GNLD, Forever Living Products, Ogano Gold Ltd, Amyway, Tianshi, Dynapharm na mengine mengi yanatumia mfumo wa biashara ya mtandao. Hayo Makampuni ni nadra sana kusikia kuwa yamefilisika au yamepunguza Wafanyakazi. Kwa hiyo watoto wetu ni vyema tukawaeleaza kuwa kuna fursa kama hizo ili wakue wakijua kuwa wanayo nafasi ya kutajirika baadaye endapo tu watakuwa tayari kutumia fursa zipatikanazo kwenye mifumo ya biashara ya mtandao.

Wazazi tuwarithishe watoto wetu biashara zetu kubwa kama tunazo. Endapo mzazi unayesoma kitabu hiki huna biashara kubwa za kuwarithisha watoto wako basi warithishe mawazo makubwa kama haya. Hakika hawatakusahau hata kama hautawaachia biashara kubwa sana. Kuwaachia mawazo makubwa ya mbinu za kujitawala na kujitegemea kifedha na wakaweza kuendesha biashara zao kubwa kutegemeana na wazo la mfumo wa biashara ulilowapa hakika huo utakuwa urithi usisahalika kwa watoto wako. Wazazi wengi wanadhani kuwa kuwasomesha watoto ndiyo urithi mkuwa wa kuwaachia watoto, ukweli unaweza ukabakia kuwa kuwapa watoto wako elimu ya kawaida ya shuleni haitawasaidia kamwe endapo mzazi

hatafanya juhudi ya kumfundisha mtoto wake kuwa elimu nje ya mfumo rasmi wa shule haumfundishi mtoto kufikia ndoto zake za umilionea. Wazazi tanapaswa sasa kuhakikisha kuwa watoto wetu wanaelimishwa kuhusu biashara kubwa zinazoweza kumtoa mtu kwenye umaskini. Watoto wetu waelezwe kwamba kama wanataka kuwa matajiri wakubwa baadaye wasiogope kuwa na biashara kubwa. Biashara za mabilioni. Wasiogope kuwa na Makampuni makubwa ya biashara ya gesi, biashara kubwa za mafuta ya petroli na dizeli. Watoto wetu wasiogope kumiliki vituo vya televisheni, wasiogope kuwa na viwanda vya vipuri vya magari. Watoto wetu wasiogope kumiliki viwanda vikubwa vya biashara kubwa za magari au vipuri vyake.

Watoto wetu tuwaambie wasiogope kuwaza mapinduzi ya viwanda. Wamiliki mitandao mikubwa ya biashara kubwa. Wafungue matawi ya Makampuni yao mpaka nje ya nchi. Tuwafundishe watoto wetu wasiwe na mawazo mgando. Wasiwe na mawazo finyu ya kujichimbia humu nchini Tanzania peke yake.

Tuwahimize kinadharia na kivitendo kumiliki mtandao mkubwa wa biashara kubwa ya chaguo lao. Tuwahimize watoto wetu waende kote Tanzania na nje ya Tanzania wakaanzishe mtandao mkubwa wa biashara yao. Watoto wetu tuwapandikizie mbegu za mawazo chanya kuhusu biashara kubwa zenye pesa kubwa. Mtoto aweze kuwa na biashara kubwa inayoweza kumuingizia pesa kubwa hata kama ni shilingi bilioni moja au bilioni mbili kwa mwezi.

Mzazi kama nilivyosema sehemu nyingi ndani ya kitabu hiki, usiache kumwambia mtoto wako maswala yatakayomwezesha kufikiria tofauti na wewe. Hata kama wewe ni maskini, mwezeshe awaze tofauti ili maisha yake yaje yawe tofauti na ya kwako. Mzazi ni vyema kufanya hivyo kwa mtoto wako akiwa bado mdogo.

Usisubiri akue. Usisubiri mtoto amalize elimu ya msingi au ya sekondari ndipo umwambie kile unachoona kinamfaa maishani mwake. Yale unayomwambia ukiwa naye hapa na pale, yale unayoongea naye ukiwa unakula mezani, stori unazoongea na mtoto wako mkiwa mnacheza mpira, mkiwa mko pamoja ndani ya gari lako, mkiwa mnaenda kanisani kusali, yale unayoongea na mtoto wako popote pale akiwa ametulia au ukiwa umeenda kumununulia chipsi, hayo ndiyo yanayomjengea misimamo na mitazamo ya maisha ya mafanikio au kutofanikiwa.

Unachoongea na mtoto wako hakikisha kuwa kinamsaidia mtoto wako kuwa mkubwa sana maishani mwake. Unachoongea na mtoto wako kiwe kile kinachomfikirisha mbali zaidi. Epuka kumwongelesha mtoto stori za kipumbavu na zisizo na mantiki kwa maisha yake. Ukifanya hivyo mtoto atakuwa na uwezo wa kuwaza mbali sana. Atakuwa na ndoto za kuwa na mawazo ya mtandao mkubwa wa kazi zake hapo baadaye atakapokuwa mkubwa kwa umri wake.

Mbinu ya -40-

Mfundishe Mtoto Kuwa Mwekezaji Mkubwa

Kama ambavyo nimekuwa nikifafanua kuwa kitabu hiki hakiwahusu wazazi ambao wameshakuwa mamilionea peke yao, narudia kusema hapa kuwa hata kama wewe mzazi hukujaaliwa kuwa milionea hadi unaposoma kitabu hiki, haimaanishi kuwa watoto wako hawawezi kuja kuwa matajiri wakubwa. Ni swala tu la kufikiri tofauti. Ukifikiri tofauti inawezekana. Ukiacha kujibana kichwa chako kwenye historia yako mbaya utaweza kufanikiwa. Achana na mambo mabaya yaliyopita yasiyoweza kurudi tena leo hii. Epuka kuwaza mambo yaliyopita na ambayo yamekufanya wewe usifanikiwe maishani mwako hadi leo. Mfundishe mtoto awe tofauti na wewe.

Makosa uliyoyafanya wewe usiyarithishe mwanao. Udhaifu wako katika kutafuta mabilioni ya fedha usitake na watoto wako wawe nao. Fikiri tofauti. Fanya malezi yako kwa watoto yawe ya tofauti pia. Hata kama kupata shilingi elfu kumi kwa siku inashindikana kwako, wewe mwambie mtoto ajitofautishe na wewe atakapokuwa mkubwa. Mwambie hivyo kabla hajawa mtu mzima yaani kabla hajatimiza umri wa miaka 15. Huko ndiko kukomaa na kuitwa mtu mzima. Mfundishe yeye ajiepushe na makosa uliyoyafanya wewe mpaka ukashindwa kupiga hatua kubwa za kifedha.

Mweleze historia yako ya zamani iwe nzuri au mbaya ili aitumie kujipanga kuepuka makosa ya kwako na yeye aweze kuwa tajiri bilionea. Jitahidi kumwambia ukweli wa maisha kuwa wewe hukufanikiwa sana hadi sasa unapomlea mtoto kwa sababu wazazi wako wewe hawakukulea kwa misingi ya kutafuta kuwa milionea au bilionea. Lakini yeye anayo nafasi na fursa tele ya kufanya mabadiliko katika maisha yake na akawa

mwekezaji mkubwa sana badala ya mfanyakazi wa kuajiriwa tu au mfanyabiashara za kawaida. Sisi wazazi tunapaswa kuelewa kuwa kama hatutawafumbua macho watoto wetu kuhusu umuhimu wa kuwa wawekezaji wakubwa ndani nchini mwao na nje ya nchi hakika watoto wetu wataendelea kuwa watumishi wa wawekezaji wengine tena kutoka nje ya nchi. Kuwa mwekezaji mkubwa ndiyo mpango mzima wa karne hii ya digitali.

Watu wasiowekeza watajikuta ndiyo wao wanaowekezwa. Badala ya wewe kuwekeza utajikuta watu wenye fikra chanya za kuelekea utajiri mkubwa na uwekezaji watakuwa ndiyo wanawatumia watoto wako kwenye kutumikia kampuni zao. Kuwekeza ninakokushabikia hapa ni kule kufanya pesa ikutumikie wewe badala ya wewe kutumikia pesa. Ni kule kuwekeza kwenye miradi yenye tija ambayo inaendelea kumwaga pesa kwako hata kama umesinzia usingizi. Ni miradi mikubwa ambayo wewe hata ukiwa haupo duniani watakaoendelea kuishi duniani wataendelea kula pesa miaka mingi sana.

Watoto wetu wanapaswa kuelezwa kuwa watakapokuwa wakubwa waje wawe wawekezaji wakubwa. Duniani kote matajiri ni watu wanaowekeza. Wakati watu maskini hutumia pesa yote wanayoipata kwanza na ndipo wanawaza kuwekeza zaidi, watoto wetu tuwafundishe kufikiria kuwekeza kabla ya kuwaza kutumia pesa. Baada ya kukua na kuwa watu wazima watoto wetu tuwafundishe na kuwaruhusu kuwa wawekezaji wakubwa.

Watoto wetu waje wawe wawekezaji wakubwa. Wawekeze kwenye majengo makubwa, kwenye hisa za Makampuni makubwa, kwenye biashara kubwa za mazao ya kilimo na mifugo.

Mwisho kabisa, nikutakie kila la kheri katika kuwalea watoto wako kaufikia malengo yao na ndoto zao watakazopata kutokana na vile wewe utakavyowalea. Kama kweli tutawalea watoto wetu kimilionea bila kujali kuwa sisi tumeshakuwa mamilionea ama la, hakika watoto wetu watajengeka akili zao katika mtazamo wa umilionea na ubilionea. Fanya kila linalowezekana kwenye akili yako kutekeleza kile kilichosimuliwa ndani ya kitabu hiki.

Waambie wengine wanunue kitabu hiki. Usikae na habari njema kama hii nyumbani kwako. Waambie wengine kuwa kitabu hiki ni hazina kwa wazazi na watoto wetu wa sasa hadi kwa kizazi kitakachofuata. Mwenyezi Mungu akubariki sana. Hongera sana kwa kusoma kitabu hiki mpaka mwisho.

++++++++++++

End.

VITABU VINGINE VILIVYOANDIKWA NA MWANDISHI HUYU AMBAVYO HUPASWI KUVIKOSA NYUMBANI KWAKO NI:

1. MBINU ZA KUPATA PESA NYINGI HADI KUWA BILIONEA (2014)

2. MBINU ZA KUFUGA KUKU NA KWARE WENGI HADI KUWA MILIONEA (2015)

3. SIRI NZITO WANAZOTUMIA MABILIONEA KUE NDELEA KUWA MABILIONEA (2015)

4. JINSI YA KUTOA SADAKA HADI KUWA MILIO NEA

REJEA

Hale, M. 2008: Become Rich By Making The Most of Your Money, Published in Kenya.

Kiyosaki R. T, 2000: Guide to Investing: What Rich people invest in and Poor people do not, Business Plus, New York.

Kiyosaki, R.T. 2002: Rich Dad Poor Dad, New York, USA.

Kiyosaki, R.T: Be Rich and Happy, Published by; Vishal Paperbacks, East Rohtash Nagar Shahdara, Delhi-32.

Nangoli, C.M, 2004: How to Make Money, Holy Star Books, USA.

Samoja, Elizabeth 2015: Graduate With Plan B in Mind, BBIP Publishers Ltd, Dar es salaam.

Shigongo,E.J, 2015: 26 Secrets How to Defeat Enemies and Make Millions Dollars. Global Publishers Limited, Dar es Salaam.

Tenganamba, G. 2014: Kichwa Chako ni Dhahabu ya Utajiri; Niim Computers&Graphics, Dar es Salaam.